Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Ishirini na Sita – Tarehe 18 Julai, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 217

**Hitaji la Kuigawa Kata ya Isansa**

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE (K.n.y. MHE. GODFREY W. ZAMBI)** aliuliza:-

Kata ya Isansa yenye vijiji 12 na idadi ya wakazi 40,000 ndiyo Kata kubwa kuliko zote katika Wilaya ya Mbozi.

Je, Serikali itakuwa tayari kuigawa kata hiyo ili kusogeza huduma kamili kwa wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, noamba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ugawaji wa maeneo ya utawala katika Kata unazingatia vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria ambavyo ni ukubwa wa eneo ambalo ni kilomita za mraba 500, idadi ya vijiji vilivyosajiliwa visivyopungua vitano (5), uwezo wa Halmashauri kumudu gharama za ongezeko la maeneo ya utawala na idadi ya watu isiyopungua 10,000.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kata ya Isansa imetimiza vigezo vyote vya kuigawa. Aidha, Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi katika kikao chake cha tarehe 27 Juni, 2008 kiliridhia kuigawa Kata hiyo. Tatizo lililopo ni utaratibu unaoitaka Halmashauri kupitisha mapendekezo hayo kwenye vikao vya Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Mkoa, ambapo bado pendekezo hilo halijapitishwa na vikao hivyo.

Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI iliandikia Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi Barua Kumb. Na. CBC.239/265/01/2 ya tarehe 7 Oktoba, 2011 kuitaka ikamilishe taratibu hizo, lakini hadi sasa Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa haijapata taarifa hizo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Isansa itagawanywa baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi kukamilisha taratibu na kuwasilisha taarifa za vikao vya Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Mkoa OWM – TAMISEMI.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri na fasaha ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninamwomba sasa ajibu swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, kumekuwa na maombi mengi sana hapa nchini ya kugawa Kata mbalimbali ambazo ni kubwa sana ili ziweze kutawalika vizuri.

Je, Serikali imeweka mkakati gani wa jumla ili kuhakikisha sasa maombi mbalimbali ambayo yametolewa Serikalini yaweze kutekelezeka?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Hilda Ngoye na uzuri ni kwamba amewahi kuwa Mkuu wa Mkoa, kwa hiyo nikieleza hizi taratibu ninazozieleza hapa sipati tatizo kabisa katika kuelewa kwamba analielewa jambo hili tunalolizungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikiambie kikao chako kwamba kama kuna zoezi ambalo liliwahi kufanyika kwa uadilifu na kwa utaratibu mzuri ulikuwa ni kuzipitisha Kata wakati ule 2,000 zikaenda mpaka 4,000 na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza, ninalisema hili kwa sababu Wabunge walio wengi hapa ni wageni. Alisimamia mwenyewe na akasema leteni orodha yote ya Kata zote zilizoundwa ipewe Wabunge humu ndani, wewe Mheshimiwa Spika, ukapewa na ukaangalia orodha ukaangalia na Kata zako na kila mtu akaangalia.

Kwa hiyo, hilo zoezi nataka nithibitishe hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba lilifanyika vizuri.

Mheshimiwa Spika, kweli kama anavyosema Mheshimiwa Cynthia Ngoye, kwamba pamoja na hayo bado zimeendelea kuwepo Kata nyingine ambazo zimejitokeza ambazo nazo zimekuwa zinaomba nafasi hiyo.

Mkakati tulionao ni kwamba huwezi uka-*deal* na Kata mojamoja hivi, hiyo kazi itakuwa ni ngumu hujapata kuona. Ninachoweza kusema ni kwamba sisi tunakusanya maombi yote na kwa kufuata taratibu hizi zilizosemwa hapa. Tukishapokea tunaangalia na tunatuma watu wetu mpaka kwenye hizo Kata ambazo zinapendekezwa na tunaangalia kama kweli wanachosema ni kweli.

Mheshimiwa Spika, hii habari ya kuwa na utaratibu wa kupitisha kwenye *DCC* na kupitisha katika *RCC* ni muhimu kwa sababu unagawa maeneo ya utawala ya watu bila kuwahusisha. Sasa kama hawakusema wao wenyewe ndiyo! ndiyo tunapata hizo sokomoko mnazozisikia za mipaka na mambo mengine.

Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelekeza na ameagiza kwamba kila wakati tunapoombwa ni lazima tutume wataalamu waende wakakague na kusema kwamba habari inayosemwa pale ni ya kweli. Ninataka niwathibitishie kwamba wakishakamilisha hayo sasa maombi yote yanachukuliwa kwa nchi nzima kwa pamoja na kwa wakati muafaka ndiyo tunatoa maamuzi. (*Makofi*)

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ni kweli kama alivyosema Waziri, lakini kulikuwa na maombi mengi kama alivyosema mwenzangu ambayo yaliletwa sijui kama hayo maombi ambayo yaliletwa yaandikwe mengine au yatafikiriwa mapendekezo ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, sisi tunazo r*ecords* zote za watu wote ambao wameomba kuunda maeneo mapya ya utawala, hii ni Halmashauri itakayokuwa na Kata mpya, inataka kuwa Mtaa mpya na Mamlaka ya Mji Mdogo *records* zote tunazo.

Kama Mheshimiwa Mwanjale anavyozungumza hapa anayo maombi ambayo alishayaleta hapa basi anione mimi na mimi nitakwenda kucheki na nisipokuta nitamwandikia kwa maandishi kwamba maombi haya sisi hatujayaona. Kwa hiyo, kama kuna Mbunge yeyote ambaye ana wasiwasi na maombi lakini tunachosema ni kwamba yakishafika hapa hatu-*deal* na ombi mojamoja bali tuna-*deal* na maombi ya nchi nzima.

Na. 218

**Ajira ya Wazanzibar Katika Asasi za Muungano**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Lengo mojawapo la Serikali ya Jamhuri ya Muungano ni pamoja na kuongeza ajira ya Wazanzibar kwenye Asasi mbalimbali za Muungano hasa ikizingatiwa kuwa wapo baadhi ya Wazanzibari wenye sifa wamechukuliwa kwa njia ya Mkataba na kufanya kazi katika Serikali ya Muungano.

(a) Je, kwa wale wafanyakazi walioajiriwa kwa Mkataba na wameshatimiza miaka 10 ya kazi na bado wapo kwenye ajira wanapostaafu watalipwa kiinua mgongo au *gratuity* pekee?

(b) Je, kitendo cha kuwalipa *gratuity* pekee wakati ametumikia miaka 10 ya kazi pamoja na umri wa kustaafu siyo chanzo cha kusababisha maisha magumu kwa mhusika na Serikali inasema nini katika hali hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fhakaria Khamis Shomar, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, malipo yoyote yanayohusiana na ajira Serikalini yanafaywa kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu pamoja na miongozo mbalimbali inayowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi katika Utumishi wa Umma Na. 2 ya mwaka 1999, Mtumishi akifanya kazi kwa Mkataba wa miaka 10 hawezi kulipwa pensheni bali atalipwa *gratuity* au kiinua mgongo. Ili mtumishi aweze kulipwa pensheni chini ya sheria hiyo ni lazima mhusika awe ametimiza masharti yafuatayo;

(i) Awe na ajira ya kudumu katika masharti ya pensheni;

(ii) Athibitishwe kazini katika ajira hiyo;

(iii) Awe ni mwanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii;

(iv) Achangie Mfuko kwa 5% na mwajiri wake 15%;

(v) Achangie kwenye mfuko mfululizo kwa kipindi kisichopungua miaka 15; na

(vi) Astaafu kwa umri wa miaka 55 au 60.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia vigezo hivyo ni dhahiri kuwa mtumishi anayetumikia kwa miaka 10 ya kazi hastahili kulipwa pensheni kwa vile hajatimiza masharti yaliyoainishwa katika Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Kazi katika Utumishi wa Umma. Aidha, haitarajiwi kwamba maisha ya mhusika yatakuwa magumu kwa sababu atakuwa amelipwa haki yake anayostahili.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, kwa wafayakazi ambao ni wa kudumu na kisheria wamemaliza miaka 15 na wanatakiwa kupata pensheni. Je, watapokelea wapi? Bara au Visiwani?

Pili, ningependa kujua ni wafanyakazi wangapi ambao kutoka Zanzibar ni wa mkataba na wangapi ni wa kudumu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Fhakaria, kama ifuatavyo:-

Kama mtumishi atakuwa ameyatimiza masharti yote niliyoyaeleza ya kuchangia mfululizo miaka 15 katika mfuko na kutimiza umri ambao unastahili ili aweza kustaafu basi atalipwa katika mfuko aliouchangia, kama ni wa Tanzania Bara kwa sababu tunayo mifuko mingi, kama atakuwa amechangia *PSPF* atalipwa na *PSPF* na kama atakuwa amechangia *LAPF* atalipwa na *LAPF.*

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili, siwezi sasa hivi kuwa na takwimu za watumishi wangapi wameajiriwa kwa mkataba na wangapi wako katika ajira ya kudumu kwa sababu suala hilo halikuwepo katika maswali ya msingi.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona.

Kwa kuwa swali la msingi linahusiana na wafanyakazi wa mkataba Serikalini, ninapenda kufahamu ni watumishi wa aina gani ambao wanalazimika kupata mkataba baada kustaafu wakati vijana wengi wapo wamesoma na wana uwezo wa kufanya kazi? Kwa hiyo, naona kama kidogo mnabana ajira.

Je, ni watu wa aina gani ambao wanatakiwa kupata nafasi hiyo kwa mkataba?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mhonga kama ifuatavyo:-

Watumishi ambao wanastahili kupata utumishi kwa njia ya mkataba kwanza ni wale wanaoajiriwa baada ya kuwa wamefikisha zaidi ya miaka 45 kwa sababu unaweza kuwa kijana ukahangaika kutafuta kazi usiipate, utakapokuwa umeajiriwa kuanzia miaka 45 au 46 utapewa ajira ya mkataba kwa sababu hutaweza kutimiza ile miaka 15 ambayo unastahili kuchangia mfuko ili uweze kupata pensheni.

Lakini pia zipo kada ambazo tuna matatizo yaani tunao watumishi wachache sana Serikalini mfano Madaktari, Walimu na baadhi ya taaluma ambazo kwa kweli katika soko la ajira zipo taaluma chache sana kuwapata watumishi. Kwa hiyo, maeneo hayo ndiyo ambayo watumishi tunawapatia au tunawaajiri kwa mkataba hata baada ya kustaafua.

Na. 219

**Kujenga Chuo cha Ufundi (VETA) Tarime**

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA (K.n.y. MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE)** aliuliza:-

Wilaya ya Tarime ni miongoni mwa Wilaya za Tanzania ambazo hazina chuo hata kimoja cha Ufundi.

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha Ufundi *(VETA)* Wilayani Tarime ili kuwawezesha vijana kuboresha maisha yao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa kuwa na chuo cha ufundi stadi katika kila Wilaya nchini, Serikali itajenga vyuo vipya au kutumia vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(Folk Development Colleges (FDCs)* kutoa mafunzo ya ufundi stadi katika ngazi ya Wilaya.

Aidha, katika kutekeleza mpango huo, kipaumbele kinatolewa kwa kuanza na Wilaya ambazo hazina vyuo vya Ufundi Stadi hata vya binafsi au Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Wilaya ya Tarima ina Chuo cha Maendeleo ya Wananchi *(Tarime FDC),* Serikali itakarabati na kukiwezesha chuo hicho kutoa mafunzo ya ufundi stadi ngazi ya Mkoa sambamba na majukumu yake ya sasa ya kutoa elimu ya wananchi badala ya kujenga chuo kipya.

Aidha, naomba kuwashauri wazazi na vijana wa Wilaya ya TArime kutumia Chuo cha Ufundi Tarime *(Tarime VTC)* kupata huduma ya chuo cha ufundi stadi wakati Serikali ikiendelea na juhudi za kutafuta fedha za kukiwezesha Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Tarime kutoa mafunzo ya ufundi stadi.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa, sasa inaonekana Tarime kuna wawekezaji wengi ambao wangeweza kusaidia kufanya huu ukarabati wa chuo hiki ulichokisema ili uweze kwenda kwa haraka na hii ni kwa sababu vilevile Tarime kuna matatizo ya ajira. Lakini vilevile kuna ugomvi kati ya ya Koo na Koo.

Je, ni lini Serikali itawahusisha wawekezaji hawa ili hiki chuo kiweze kuanza mara moja?

Pili, kwa kuwa tatizo hili la *VETA* ni la kitaifa na mimi kwangu Wilaya mpya ya Buhingwe tuna tatizo la Chuo cha *VETA.*

Je, ni lini Chuo cha *VETA* nacho kitajengwa Wilaya mpya ya Buhigwe?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Tarime kwamba kuna wawekezaji wengi na vijana wengi ambao wamemaliza elimu ya Msingi na Sekondari bado hawajapata chuo kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba tunawashauri vijana hawa waweze kutumia chuo cha *FDCs* ambacho kipo Tarime wakati Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuweza kukikarabati.

Taarifa ya furaha ni kwamba tayari Serikali ina fedha shilingi bilioni 4.2 ambazo zipo kwenye Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa ajili ya ukarabati wa vyuo hivyo vya *FDCs.* Kwa hiyo, chuo cha Tarime pia kitakarabatiwa.

Swali la pili, kwamba suala la kujenga *VETA* kwa kila Wilaya ni suala la kitaifa na ni kweli kabisa kwamba Wilaya nyingi bado hatujaanza kujenga na kama nilivyosema kwamba mwaka wa fedha 2010 na mwaka 2011 tumeanza chuo cha Wilaya Makete na mwaka wa fedha 2012 mkitupitishia Bajeti tumeandaa kujenga vyuo vinne kama nilivyosema juzi kwenye jibu langu na hata Wilaya hii ya Buhigwe sijaijua kwa sababu ni Wilaya mpya na unapotaka kuanza kujenga vyuo vya *VETA* kwanza ni lazima ufanye stadi za kazi kwenye Wilaya hiyo.

Kwa hiyo, Wilaya mpya zilizoongezeka Wizara itafanya utaratibu wa kuvipitia ili kuweza kufanya stadi mbalimbali za vijana waliopo ili tuweze kuona ni lini tutaweza kuvijenga vyuo hivyo katika Wilaya mpya.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, matatizo ya Wilaya ya Tarime yanafanana kabisa na matatizo yaliyopo Wilaya ya Chunya isipokuwa tu Tarime wana Chuo cha Maendeleo ya Wananchi.

Je, Serikali imejipangaje kujenga Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Chunya?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja dogo la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, Wilayani Chunya juu ya kujenga chuo cha *VETA* Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Wilaya ya Chunya haina hata chuo kimoja hata cha *FDCs.* Katika Bajeti ya mwaka huu katika Wilaya nne ambazo Serikali itajenga labda nizitaje kwamba ni Wilaya ya Kilindi, Namtumbo, Chunya na Ukerewe.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwambalaswa, Wilaya ya Chunya ipo katika Bajeti ya kupata chuo cha *VETA.*

**SPIKA:** Wenzenu wamepata na nyie mnataka mpate! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Dustan Mkapa!

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Malocha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkapa. *(Kicheko)*

**MHE. DUNSTAN DANIEL MKAPA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Sambamba na matatizo ya Tarime, wilaya ya Nanyumbu nayo haina chuo cha ufundi Stadi wala cha Maendeleo ya Jamii. Ningependa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi anieleze, Nanyumbu vijana wanateseka, hawana ajira, ni lini watajenga chuo cha *VETA?*

**SPIKA:** Wakipata fedha. Mheshimiwa Naibu Waziri! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Dunstan Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, utaona tu hata Wabunge wengi wanasimama sana juu ya masuala haya ya *VETA* kwenye wilaya zao. Kwa pamoja tu niseme kwamba, Serikali katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) iliahidi kwamba itajenga vyuo vya *VETA* kila Wilaya.

Kila siku huwa nasema hapa kwamba chuo kimoja kukijenga mpaka kukikamilisha inachukua gharama ya karibuni bilioni sita(6). Tayari Serikali inaendelea kuandika maandiko mbalimbali kwa lengo la kutafuta fedha hizo.

Lakini mwaka huu kama nilivyosema kwamba katika Bajeti ya ndani, moja kwa moja kwa fedha za Serikali tutaanza kwa kujenga vyuo vinne (4), mwaka kesho tutapanga hivyo hivyo, mwaka kesho kutwa tutapanga hivyo, wakati tukisubiri maandiko yetu yaweze kukubaliwa kwa ajili ya kupata fedha kwa ajili ya kujenga vyuo vya *VETA.*

Lakini wilaya hizi tumepanga kwa makundi; kuna wilaya 29 kwa awamu ya kwanza na Wilaya 15 kwa awamu ya pili. Wilaya ya Nanyumbu iko katika awamu ya Pili ya kujengewa vyuo vya *VETA,* baada ya kumaliza zile wilaya 29. *(Makofi)*

Na. 220

**Kuchelewa Kutolewa Hukumu Kwa Kesi Nyingi Nchini**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Je, kwanini kesi nyingi zinazowakabili watuhumiwa mbalimbali nchini zinachukua muda mrefu kutolewa maamuzi (hukumu) inayopelekea manung'uniko mengi kwa wananchi (husika) na wakati mwingine kusababisha unyanyasaji na wahusika kukata tamaa ya maisha yao?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa zinazochangia kwa kesi kuchukua muda mrefu bila kutolewa hukumu ni nyingi. Miongoni mwa sababu hizo ni uchache wa Mahakimu unaosababisha baadhi ya Mahakama kufanya kazi kwa kutumia Mahakimu wanaotembelea Mahakama zaidi ya moja na Mahakimu wachache waliopo vituoni kuzidiwa na wingi wa kesi na hivyo kuchelewa kukamilisha usikilizwaji wa kesi na kutoa hukumu.

Lakini pia ni sababu nyingine ni uchache wa wapelelezo unaoathiri kasi ya kukamilishwa kwa upelelezi, kutokuwepo kwa ofisi za mashtaka katika ngazi za Mahakama za Mwanzo, Wilaya na Mikoa kunakosababisha askari Polisi waliopo pia kufanya kazi za kupeleleza na kuendesha mashtaka.

Vile vile uchache wa vitendea kazi unaoifanya Mahakama na Wapelelezi kuchelewa kukamilisha uchapaji wa Hukumu na majalada ya upelelezi, kukosekana kwa mafungu ya fedha za kulipa gharama za mashahidi ambako kunasababisha kesi kuahirishwa kwa kushindwa kulipa gharama za mashahidi.

Vilevile kutokuwepo kwa huduma za Mahakama Kuu kila mkoa kunakosababisha kesi nyingi zikiwemo zile za mauaji kutosikilizwa na Mahakama hiyo mara kwa mara na hivyo kusubiri vikao maalum vya Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, aidha, wadau mbalimbali wamekuwa hawapendi kutua njia mbadala za kutatua migogoro kama vile usuluhishi kwa kutumia msuluhishi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa sababu za msingi zinazochangia kuchelewa kusikilizwa kutolewa hukumu kwa kesi, napenda pia kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba ukamilishwaji wa kesi hutegemeana na mazingira ya kila kesi kwani zipo kesi ambazo zinachukua muda mfupi kama pande zote mbili zinazohusika zinakuwa tayari kuendelea.

Mheshimiwa Spika, aidha, maboresho yanayoendelea kwa sasa yanazidi kuimarisha mazingira ya utoaji wa huduma za sheria na haki nchini.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Watuhumiwa wengi hukaa rumande zaidi ya miaka mitano, sita, saba, bila kupatiwa hukumu na kwa kuwa wanapopatiwa hukumu zao wengi wao huonekana hawana hatia. *(Makofi)*

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati mwafaka wa kuwalipa fidia wale watuhumiwa wambao wakati wa hukumu huonekana hawana makosa? (*Makofi*)

(ii)Kwa kuwa kuna baadhi ya wafungwa Wanawake wanapokwenda jela huwa ni wajawazito na wengine hupata ujauzito humo humo wakiwa wamefungwa na kwa kuwa wafungwa wale wanapojifungua baadhi yao wanabakia na watoto wao mle gerezani jambo ambalo ni kinyume cha haki ya mtoto.

Je, Serikali haioni kuwa haiwatendei haki watoto hao? Na kama haiwatendei haki watoto hao ina mpango gani wa kuwapatia haki watoto hao kwa sababu huwa wanakaa gerezani kama na wao wametenda makosa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar.

Katika swali la kwanza ameelezea kero ya watuhumiwa mbalimbali kukaa rumande kwa muda mrefu bila ya kupata hukumu. Ni kweli wengi wamekuwa wakikaa, lakini kama nilivyoeleza katika jibu la msingi suala hili linatokana na sababu mbalimbali ambazo nimeishazieleza.

Lakini Wizara haijakaa kimya, inayo mipango mbalimbali na hata katika Bajeti ya Wizara yetu tulieleza. Mfano kama hivi sasa tumeishaanza kutenganisha shughuli za upelelezi na shughuli za uendeshaji mashtaka. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo inasaidia wapelelezi kubakia na shughuli zao za upelelezi na waendesha mashtaka kuendelea na shughuli zao za uendeshaji wa mashtaka.

Mfano faida ndogo tu ambayo tumeipata kuanzia tulipoanza kuchukua jukumu ya uendeshaji wa mashtaka kupitia kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka, kuanzia mwaka 2007 Mahakama ya Kisutu ilikuwa inakabiliwa na takribani kesi 2055. Lakini hadi kufikia tarehe 10 Julai, 2012 yaani mwaka huu, kesi zinazofunguliwa Kisutu ni 170 tu. Kwa hiyo, utaweza kuona kuwa mwisho watu wengi wataweza kupata hukumu zaoi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika swali la pili Mheshimiwa amependa kujua Serikali ina mipango gani kuhakikisha kwamba, Wanawake wajawazito ambao wanajifungulia katika magereza watoto wao wanapata haki ili na wao wasigeuke kuwa wafungwa.

Mimi mwenyewe nimeishashuhudia, hata juzi tu Jumamosi nilikuwa katika Gereza Kuu Isanga, wapo watoto wadogo watano (5) na tunalifanyia kazi suala hilo kuhakikisha kuwa watoto hawa hawawezi kukaa muda mrefu kwani Sheria hairuhusu watoto wale kukaa zaidi ya miaka miwili katika magereza haya. Kwa hiyo, tunalifanyia kazi kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, ili kuhakikisha watoto hawa wanatengewa sehemu

maalum au ikiwezekana wapelekwe katika familia zao. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, umeishamaliza?

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa majibu ya Serikali kila siku katika utaratibu huu wa ucheleweshaji wa kesi na upelelezi ni kwa kwamba wapelelezi ni wachache. Serikali haioni kwamba, ucheleweshwaji huu ambao unasababishwa na tatizo la kiserikali unawadhalilisha wale ambao ni watuhumiwa na hawajatiwa hatiani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Amehoji iwapo Serikali haioni kwamba ucheleweshaji huo wa upelelezi unawadhalilisha watuhumiwa. Kwanza kabisa utaona kwamba, shughuli za upelelezi zinafanywa na taasisi zaidi ya moja, na ndiyo maana kuepuka hilo sasa sisi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tumeamua kuchukua jukumu na dhamana hii.

Hata ukiangalia Ibara ya 86 ya Ilani ya Uchaguzi wa CCM inataka pia tuanzishe ofisi za Waendesha Mashtaka hadi katika ngazi za chini kabisa za Mahakama na tunaamini katika siku chache zijazo

kadiri tutakavyopata Bajeti tutaweza kufungua ofisi nyingi zaidi katika Mahakama za chini kabisa na tunaamini upelelezi utachukua muda mfupi kwa sababu wapelelezi watafanya kazi yao ya upelelezi na waendesha mashtaka watafanya kazi yao ya uendesha mashtaka.

Na. 221

**Malipo ya Waliokuwa Wafanyakazi wa MUTEX**

**MHE. VICENT J. NYERERE** aliuliza:-

Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara iliamua kusaidia kumaliza kero ya waliokuwa Wafanyakazi wa *MUTEX* kwa kuwalipa mafao yao stahiki:-

Je, hatua hiyo imefikia wapi?

**SPIKA:** Ahsante sana. Mimi pia niliwahi kuwa Mkurugenzi wa *MUTEX* zamani. Haya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vicent J. Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha *MUTEX* kilibinafsishwa kwa utaratibu wa mufilisi na jukumu la usimamizi wa malipo ya mafao stahiki ya wafanyakazi hao linasimamiwa na Shirika Hodhi la *CHC* lililo chini ya Wizara ya Fedha kwa utaratibu unaopendekezwa na Mfilisi na wala si Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo Wizara yangu katika kufuatilia suala hili inaonekana kwamba, wakati wa ufilisi kiwanda kilikuwa na jumla ya Wafanyakazi 935 ambao mafao yao yalikuwa yameandaliwa na Mfilisi aliyeteuliwa na *Loans and Advances Realization Trust (LART).*

Wafanyakazi wote walitakiwa kuchukua mafao yao kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizowekwa, lakini wafanyakazi 512 tu ndiyo waliojitokeza kuchukua mafao yao. Wafanyakazi 423 waliobaki hawakuchukua mafao yao na badala yake mwaka 2007 walifungua kesi Mahakamani na hukumu ilitolewa dhidi yao ambapo walishindwa.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi hao hawakuridhika na hukumu hiyo ya mwaka 2008, waliamua kukata rufaa mwaka 2010 ambayo ilitupiliwa mbali na wakashauriwa kuchukua mafao yao yaliyoandaliwa na Mfilisi lakini hawakufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwezi Februari mwaka huu 2012, Wizara yangu iliwasiliana na Mwenyekiti wa Wafanyakazi hao 423 Bwana Maengera D. Mashana kwa lengo la kuwashauri kufanya mawasiliano na Shirika la *Consolidated Holding Corporations (CHC)* ili

walipwe mafao yao ambayo yamehifadhiwa katika Benki ya *NBC,* Tawi la Musoma chini ya uangalizi wa Mfilisi.

Orodha ya majina ya wafanyakazi hao na malipo yao stahiki ninayo. Iwapo Mheshimiwa Mbunge atapenda kujua namna malipo yalivyofanyika tunaweza tukaonana baada ya kipindi hiki. *(Makofi)*

**MHE. VICENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa orodha hii nilikwishaiona na fedha za hawa wafanyakazi 423 hazitoshi hata kuwarudisha makwao na aliyekuwa Waziri wa Wizara hii aliahidi kuwasiliana na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuona kama wanaweza kuongeza. Swali ni kwamba, Je, Waziri ataendeleza mazungumzo haya na Wizara ya Fedha ili wafanyakazi wale waongezewe na waweze kupata malipo stahiki?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vicent J. Nyerere, kama ifuatavyo.

Napenda kumhakikishia kwamba, kwa kipindi hili tulichonacho na orodha ile niliyoiona na ndiyo maana nimemshauri Mheshimiwa Mbunge tuonane baada ya kikao hiki kwa sababu hata katika yale makato yalivyokatwa inaonekana kuna tofauti zimejitokeza pale. Nina hakika tukiishakubaliana hilo wanaweza wakaongezwa kidogo mafao yao.

**SPIKA:** Nani anauliza kwa niaba ya Mheshimiwa Salome Mwambu? Hilo swali sasa litaachwa!

Na. 222

**Kuboresha malipo ya Mafao ya Wastaafu**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. SALOME D. MWAMBU)** aliuliza:-

Kuanzia mwaka 2005 Wastaafu wanalipwa kwa mkupuo wa miezi sita sita na pensheni yao ya miaka mitatu na kwamba hulazimika kufuata mlolongo mrefu wa kujaza fomu na kuzifuatilia Dar es Salaam.

(a) Kwanini Serikali imeweka tofauti katika kulipa mafao?

(b) Je, ni lini Serikali itaondoa mlolongo mrefu wa kusogeza shughuli hizo mikoani?

(c) Je, ni lini Serikali itatambua kuwa kiwango wanacholipwa wastaafu kimepitwa na wakati na hivyo kufanya marekebisho?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome D. Mwambu, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inawalipa wastaafu pensheni zao kupitia akaunti binafsi za wastaafu hao kwa vipindi vya miezi mitatu mitatau kuanzia Januari mwaka 2012 kama Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inavyolipa.

Asilimia 20 ya mchango wa mwanachama inatumiwa na mifuko yote. Hakuna tofauti ya muda uliopo katika kuwalipa pensheni wastaafu isipokuwa kuna tofauti ya vigezo (*package factors*) vya kukokotoa mafao kati ya Serikali na Mifuko mingine kama *NSSF* na *PPF.* Aidha, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (*Social Security Regulatory Authority (SSRA)* kwa kushirikiana na Benki Kuu imefanya tathmini ya kuangalia namna ambavyo kila mfuko utatumia kikokotoa linganishi na mfuko mwingine katika kutoa mafao kwa Wastaafu bila kuathiri ukuaji wa mifuko. *(Makofi)*

Matokeo ya tathmini hii yatawasilishwa kwa wadau wa masuala ya pensheni siku ya Ijumaa tarehe 20 Julai, 2012 kwa ajili ya kujadiliwa na kupokea mapendekezo kwa ajili ya hatua za kuandaa Waraka kwenda Baraza la Mawaziri kwa ajili ya idhini. Hivyo, ni imani ya Serikali kuwa suala la kutumia vikokotoa vipya na linganishi kwa mifuko yote ya pensheni litakamilika mapema na kuanza kutumika na wadau wote wa pensheni.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuzitumia Hazina Ndogo kuratibu huduma za pensheni kwa kila Mkoa na kulipa pensheni zao kupitia akaunti zao za benki unawawezesha wastaafu kupata pensheni zao huko huko walipo na hivyo sisi Serikali tunadhani utaratibu huu bado unakidhi mahitaji ya wastaafu.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kiwango cha pensheni wanacholipwa wastaafu hakikidhi mahitaji yote ya lazima. Serikali imekuwa ikiongeza kiwango cha pensheni pale ambapo uwezo wa kufanya hivyo unaruhusu. Kwa mara ya mwisho Serikali iliongeza kiwango cha chini cha pensheni kutoka shilingi 21, 601/= kwa mwezi hadi shilingi 50,114/= kwa mwezi Julai, 2009. kiwango cha shilingi 21,601/= kilianza kutumia kuanzia Julai, 2004 hadi Juni mwaka, 2009. Serikali itaangalia uwezo wake wa kumuda ongezeko la kima cha chini cha pensheni na itakapoona uwezo upo na ni endelevu haitasita kuongeza pensheni hizo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Pamoja na utaratibu mzuri wa Serikali unaotumika kulipa pensheni wastaafu lakini bado kuna tatizo kubwa la pensheni hizi kuwafikia wastaafu kwa kuchelewa sana. Unakuta mstaafu ameandikiwa atakuwa anapokea fedha kupitia akaunti kila baada ya miezi mitatu au sita, lakini mpaka hivi ninavyozungumza wako wastaafu ambao hawajapata

pensheni zao zaidi ya miezi ambayo imepangwa kwenye utaratibu wao wa kawaida?

(ii) Kwa kuwa wastaafu hawa wamechangia kwa kiwango kikubwa sana taasisi zetu hizi, *NSSF, PSPF* na nyinginezo na kwa kuwa taasisi hizi zina miradi mingi sana ya fedha. Je, kutokana na faida kubwa ambazo taasisi zinapata wastaafu hawa wanapata gawio gani kupitia miradi mbalimbali inayoendeshwa na taasisi hizi ambazo walizichangia kwa kiwango kikubwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)**

Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge maswali yake mawili ya nyongeza. Kwanza fedha zinachelewa sana pengine kutokana na utaratibu wa kibenki, kwa sababu fedha inaweza ikawekwa benki lakini kutokana na taratibu za kibenki inawezekana hizo fedha zinachelewa kwa sababu hiyo.

Lakini hata hivyo, Mheshimiwa Mbunge naomba utupatie hiyo orodha ya wastaafu ambao hawajapata pensheni zao kwa muda mrefu ili tuangalie na tulitatue tatizo hili. Hizi ni fedha zao na wana haki kabisa ya kupata fedha zao kwa wakati unaohitajika. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge tukutane ili anipe orodha ya hao wastaafu na benki zao ili tujue ni nini kinafanyika hapa katikati na kwa nini wanaathiri upatikanaji wa fedha kwa wakati.

Lakini suala la gawio kutoka katika mifuko kama nilivyosema katika swali langu la msingi kwamba kuna tofauti yaani *package factors* ya mifuko tofauti tofauti. Kwa hiyo, mwanachama anapokwenda kujiunga na Mfuko anakuwa anakubaliana kabisa kutokana na zile *package factors* zilizopo. Kwa hivyo, sina uhakika kama hii faida ya gawio ndiyo inaingizwa katika *package factors*. Lakini vilevile kama nilivyowambia mifuko tofauti inatoa vivutio tofauti kutokana na mchango wa wanachama.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, nataka kumwuliza swali dogo la nyongeza. Kwenye mifuko yetu ya pensheni yote *formula* za kukokotoa pensheni zipo tofauti unaweza kukuta Mkurugenzi anatoka Ofisi moja ambaye anachangia *PSPF* na *PPF* siku analipwa pensheni yao tofauti yao ni kubwa sana umesema Serikali inatafuta taratibu za kuoanisha hizo formula. Sasa mkishaoanisha *formula* wale waliokuwa wanapata zaidi na wale waliokuwa wanapata kidogo mnafanya nini sasa kama Serikali namna ya kuoanisha hayo mapato?

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi. Ni kweli baada ya kuanzisha mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Hifadhi ya Jamii sasa hivi Mifuko yote Mamlaka imekwishaipitia na imeanza kutoa ushauri kuhusiana na zile *formula* na kama alivyosema Mheshimiwa Peter Serukamba kazi ya *CRA* ni kuhakikisha kwamba sasa ina *harmonize* hizi *formula* ili wale waliokuwa wanapata kiasi kikubwa kama *PSPF* na wale waliokuwa wanapata

kiasi kidogo *formula* hizo zitarekebishwa na Mifuko hii itawashauriwa ili waweze sasa kutoa kiasi kikubwa kwa wastaafu wao lazima watumie *formula* fulani. Kwa hiyo, hiyo kazi inafanyika na baada ya sheria hii kuwa imetiwa saini sasa haya Mashirika yataanza kutoa pensheni kwa kutumia hizi *formula*. *(Makofi)*

Na. 223

**Viwango vya Pensheni za Wastaafu wa JWTZ**

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kabla ya kujibiwa swali langu naomba nifanye marekebisho kidogo kwenye sehemu ya (b) badala ya kusomeka posho isomeke pensheni.

Askari wa JWTZ wameonesha ukomavu na nidhamu kubwa tangu kuanzishwa kwa Jeshi hilo, ambapo wametumika ndani na nje ya mipaka ya Tanzania katika kutafuta uhuru wa nchi mbalimbali:-

(a)Je, Serikali inafahamu kuwa wengi wa wastaafu wa JWTZ wana hali ngumu ya maisha na kuna haja ya kuwaongezea kiwango cha pensheni wanazopewa?

(b)Je, ni nini kinazuia Serikali kupandisha pensheni za wastaafu hao kila mara wanapopandisha vima vya chini vya mishahara ya wafanyakazi?

**SPIKA:** Ni mabadiliko makubwa, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri jibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwa wengi wa wastaafu wa JWTZ, pamoja na wastaafu wengine wana hali ngumu sana ya maisha. Kiwango cha chini cha Pensheni cha sh. 50,144.00 kwa mwezi ambacho kinacholipwa na Serikali ni kidogo sana kulingana na hali halisi ya maisha ya sasa.

Hata hivyo, Serikali kwa kulitambua tatizo hilo itaendelea kuongeza kiwango cha pensheni kwa wastaafu wote kwa kadri hali ya mapato itakavyoruhusu.

(b) Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali haifurahi kuona raia wake wanapata taabu kwa sababu yoyote ile. Hata hivyo, malipo yote ambayo Serikali huyafanya hutegemea sana matokeo ya ukusanyaji wa mapato.

Aidha, pensheni ni malipo yanayotokana na mchango wa mstaafu kutoka kwenye mshahara wake wakati akiwa kazini pamoja na mchango wa mwajiri wake.

Utaratibu huu hautoi fursa kwa wastaafu kuongezewa viwango vya pensheni pindi viwango vya chini vya mishahara ya wafanyakazi vinapoongezeka. Hata hivyo, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa wanajeshi hawana utaratibu wa kuchangia kutoka kwenye mishahara yao. Kwa hivyo, malipo wanayopata ni *grant* kutoka Serikalini. *(Makofi)*

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana tuliyoyapata kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba Askari Wanajeshi huwa hawachangii katika Mifuko ya Jamii na hivyo kupelekea kupata matatizo kama haya na kwamba nyongeza za pensheni zinakuwa siyo zenye taratibu ambazo ni za kawaida.

(a) Je, Serikali haioni kwamba sasa wakati wa umefika angalau kwa kuzungumza na Mashirika haya ili waweze na wao kupatiwa mikopo ya nyumba au dhamana nyingine zitakazoweza kuwasaidia baada ya wao kustaafu?

(b) Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba haiko tayari kuona raia wake wanapata tabu kimaisha kutokana na kipato wanachokipata, lakini juu ya hivyo Askari hawa ni Askari wa akiba baada ya kustaafu hivyo Serikali kukaa muda mrefu mbali na hali ya uchumi kuwa mbaya kutokuwaongezea viwango vya pensheni zao ni kuwanyima haki za msingi.

Je, Serikali haioni sasa kwamba wakati umefika kila baada ya miaka miwili au mitatu kuwaongezea angalau asilimia 25 ya pensheni zao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Spika, kupata mikopo kwa wanajeshi ama wastaafu hakuendani sambamba na kuchangia kwao. Kwa hiyo, mtu yeyote kama atakidhi vigezo vya Mashirika ambayo yanatoa mikopo basi anaweza kupata mkopo wa aina yoyote ile. Kwa hiyo, hivyo haviendani sambamba.

Lakini swali la pili, kwa nini viwango basi haviongezeki kila baada ya miaka miwili labda kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba inategemea sana sana hali ya mapato ya Serikali. Lakini hata hivyo, kwa hao wanajeshi kuchangia moja kwa moja katika Mifuko kunatokana na sheria ambazo zipo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tayari mwenyewe yupo hapa anasikia labda atakavyoona kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuweza kubadilishwa hizo sheria ili wanajeshi nao wakaweze kuchangia katika hiyo Mifuko, basi akiona ipo haja hiyo naye atafanya hivyo. Ni Waziri mwadilifu, Waziri mwenye hekima na Waziri ambaye ame-*determine* hasa kuendeleza mbele Wizara hiyo. Kwa hiyo, anasikia na naamini kwamba atalifikiria suala hilo. (*Makofi*).

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa wastaafu wengi wa Majeshi hasa kwa upande wa Zanzibar wamekuwa wakifuatilia mafao yao na wastaafu hawa wanakopa fedha za nauli za kufuatilia mafao yao Tanzania Bara na hawajafanikiwa mpaka leo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atahakikishaje wastaafu hawa nao wanapata mafao yao kwa wakati muafaka?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)**: Mheshimiwa Spika, kama basi hiyo *list* ya hao wanajeshi ambao wanafuatilia mafao yao na wanapata tabu sana katika kufuatilia mafao yao basi naomba Mheshimiwa Mbunge anipatie hiyo orodha ili tuweze kuangalia suala hilo tutalirekebisha vipi.

Nilisema katika jibu langu la msingi kwamba Serikali ama Wizara kwa kuona usumbufu sana imeweka haya mafao katika Hazina ndogo katika kila Mkoa. Kwa hiyo, kama pia kuna watu kule Zanzibar wapo na wanapata tabu hii naomba tuonane na Mheshimiwa Mbunge anipe orodha yao ili tuangalie ni utaratibu gani ambao tunaweza kufanya siyo lazima wao waje Tanzania Bara, lakini tunaweza tukaangalia utaratibu wao kuweza kupata mafao yao wakati wakiwa Zanzibar. *(Makofi)*

Na. 224

**Upungufu wa Wataalam Katika Zahanati - Tandahimba**

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Mpango wa MMAM ni kujenga zahanati kila kijiji na Kituo cha Afya kila Kata, Wilaya ya Tandahimba yenye Kata 30 na vijiji 157 ina zahanati 30 lakini hakuna wataalam wa kutosha kwenye Zahanati hizo.

Je, Serikali imejipangaje kumaliza tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tandahimba ni kati ya Wilaya ambazo zina uhaba wa watumishi wa fani mbalimbali za afya. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imefanya jitihada za kulitatua tatizo hili kwa kuwapangia wahitimu wa kada za afya kutoka Vyuo vya Mafunzo katika Halmashauri ya Tandahimba kulingana na maombi ya Wilaya hiyo kama ilivyoidhinishwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kama ifuatavyo:-

Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Wilaya ya Tandahimba iliomba na kuidhinishwa jumla ya nafasi 37, kati ya nafasi hizi hadi kufikia Juni, 30, 2012 jumla watumishi waliopelekwa kwa ajili ya ajira mpya ni 32. Aina ya kada na idadi yao ni:- Maafisa Wauguzi Wasaidizi 13, Wauguzi ngazi ya cheti 10, wateknolojia 2, wateknolojia wasaidizi 1, mhudumu 1, Tabibu wasaidizi 5 na nafasi 5 za Tabibu Wasaidizi hazikujazwa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Tandahimba ina jukumu la kuainisha mahitaji ya watumishi kulingana na mahitaji yake na kufuata utaratibu uliowekwa ili Wizara iweze kuwapatia watumishi husika. Wizara ipo tayari kupeleka watumishi kulingana na nafasi zilizoidhinishwa na Idara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Aidha, ni jukumu la Halmashauri hiyo kuweka vivutio ili watumishi hawa wasiondoke. Vilevile, Wizara imetekeleza mikakati kadhaa kwa lengo la kutatua tatizo la watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya ikiwemo; kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya mafunzo mwaka hadi mwaka.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, Halmashauri ya Tandahimba imekuwa ikiainisha mahitaji ya watumishi kila mwaka, lakini kwa bahati mbaya huwa wanapewa wachache wasiomaliza tatizo. Pia wakati mwingine wale tunaowahitaji kwa umuhimu sana huwa hawapatikani. Kwa mfano, kwa sasa hivi tuna tatizo kubwa la

mtaalam wa X-ray pale kiasi cha kuonekana *X-ray* iliyopo pale ni pambo tu.

(a) Je, Serikali sasa inaweza kutoa kibali maalum kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba kutafuta wataalam pamoja na hawa watalaam tunaoletewa na Wizara lakini ikatafuta wataalam wake ili kuziba pengo hilo?

(b) Kwa nini nafasi tano za Maafisa Tabibu Wasaidizi hazikujazwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mtaalam wa *X-ray* na wataalam wote kwa ujumla wake katika Wizara hii kwanza mahitaji ni makubwa kuliko uzalishaji wa wataalam hawa.

Kinachojitokeza pamoja na nafasi za ajira kuwepo lakini uzalishaji bado umekuwa siyo kama vile ambavyo tunavyojaza kwenye vituo vyetu. Kwa mfano, kwenye mwaka 2007 kwenye Idara yote uzalishaji ulikuwa wataalam 1,320 ambao waliweza kuingia kwenye hivyo Vyuo.

Lakini mwaka 2011 wanafunzi ambao waliingia kwenye vyuo takribani 5,600 hili ni ongezeko kubwa. Lakini ongezeko hili limeenda sambamba na ongezeko la Vituo vya Afya vyenyewe kutoka 4,000 mpaka 6,000. Kwa hiyo, ongezeko la vituo vya Afya pekee yake yaani vituo vyote vya kutolea huduma ilikuwa takriban vituo 1,555.

Sasa pamoja na upungufu wa vituo vilivyokuwepo mwanzo na uwezo wa kuendeleza kujaza mapungufu hayo lakini pia kumekuwa na ongezeko la vituo vya afya vipya ambavyo pia vinahitaji kuongezewa watumishi.

Kuhusu mtaalam wa *X- ray* kusema kwamba wapate ruksa ya kuweza kuajiri kama mtaalam yupo tafsiri zile za kupata ajira zikiwepo na nafasi ipo basi hakuna tatizo la kuweza kumpata huyu mtaalam na kuweza kumwajiri.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Tatizo la ukosefu wa wataalam katika Wilaya ya Tandahimba ni sawa na tatizo lililopo katika Wilaya ya Kasulu.

Je, ni lini Serikali itapeleka wataalam katika Wilaya ya Kasulu ukizingatia kuwa Wilaya hiyo ipo pembezoni? (*Makofi*)

**SPIKA:** Haya kama unajua jibu kama hujui basi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, suala la kujaza nafasi za utumishi zinachukuliwa katika maeneo yote kulingana na Wilaya kama ilivyowasilisha maombi yake. Kama Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu itakuwa imewasilisha haya maombi na Wizara yetu kuwapangia na kupata idhini ya Utumishi wa Umma hakutakuwa na tatizo la kujaza.

Kwa hiyo, mimi nafikiri ni suala la kufuatilia ule upangaji na uzalishaji wetu utakapokuwa umeweza kutosha hizo nafasi basi nafikiri Kasulu ni moja katika Wilaya ambazo zitaweza kupata watumishi hao.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa ugonjwa unapotokea hauna muda unaweza ukatokea wakati wowote. Lakini katika Zahanati zetu na Vituo vya Afya vinafanya kazi kwa saa tisa yaani kuanzia saa 1.00 mpaka 9.00. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kuziwezesha Zahanati na Vituo vya Afya kufanya kazi kwa saa 24 hasa vijijini ili kuweza kuokoa wananchi kule kwa sababu wengi wao wako mbali sana na hospitali za Wilaya hata Mikoa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Zahanati na Vituo vya Afya na maeneo yote ya vituo vya kutolea huduma vinahitajika kufanya kazi takriban masaa 24 kwa sababu mtu anapokuwa anaugua anaweza kuugua wakati wowote tu. Kinachojitokeza kikubwa ni idadi ya watumishi ambao wanakuwepo pamoja na uwezo wa hicho kituo kuweza kutoa huduma kwa saa hizo 24.

Changamoto iliyopo hapa ni kwamba kadri unavyoweza kuongeza jukumu zaidi la utendaji wa kazi ndivyo unavyohitaji zaidi watumishi wa kuweza kutekeleza kazi hiyo pamoja na huo muda wa nyongeza. Kwa sasa vituo vingi vya Afya na zahanati vina watumishi wachache na wote tunafahamu.

Lakini vilevile jitihada za Serikali ni kuviongezea watumishi kadri hali inavyoruhusu na itakavyowezekana ili angalau hizo huduma ziweze kupatikana katika hatua ya watumishi kuwepo kuwa anaitwa au anakuja kwenye kipindi ambacho mgonjwa anaweza kujitokeza baada ya saa za kazi.

Na. 225

**Vitendo vya Kikatili vya Wauguzi na Wakunga**

**MHE. PHILIPA G. MTURANO** aliuliza:-

Kumekuwepo na malalamiko mengi katika jamii juu ya vitendo vya kikatili vinavyofanywa na Wauguzi na Wakunga katika Hospitali mbalimbali Nchini:-

(a) Je, Serikali itahakiki lini vyeti vya taaluma hiyo ili kuona kama wanakidhi vigezo vya kazi yao?

(b) Je, Serikali haioni kwamba umefika muda wa kutunga sheria ya kuwashitaki na kuwafukuza utumishi wale wote watakaohusika na vitendo hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philipa Geofrey Mturano, Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inatambua kuwepo kwa baadhi ya Wauguzi na Wakunga, wasiozingatia maadili wanapotoa huduma.

Aidha, Wizara imeendelea kuwahimiza watumishi wote wa Sekta ya Afya kuzingatia maadili ya taaluma zao wakati wakitoa huduma. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 Baraza la Uuguzi na Ukunga limesikiliza tuhuma dhidi ya Wauguzi na Wakunga 8 na hatua za kinidhamu zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kuonywa, kusimamishwa kwa muda na wengine kufutiwa usajili kwa mujibu wa kifungu (6)(j) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010.

Ili kuthibitisha uhalali wa Wauguzi na Wakunga hapa nchini, Baraza la Uuguzi na Ukunga limeendesha zoezi la kuhakiki vyeti vya Wauguzi wote hapa nchini na kuwapatia leseni.

Zoezi hili lilibaini kuwepo kwa takribani Wauguzi 132 ambao hawakuwa Wauguzi halali. Hatua za kisheria zimechukuliwa dhidi ya watuhumiwa hawa ambapo baadhi yao wamefikishwa Mahakamani wengine uchunguzi bado unaendelea na baadhi yao walitoroka kwenye vituo vyao vya kazi baada ya kubainika na juhudi za kuwatafuta zinaendelea.

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria ya "*The Nursing and Midwifery Act*, 2010" inayosimamia taaluma hizi, inavyo vifungu vinavyobainisha makosa ya Jinai kuhusiana na kufanya kazi kama Muuguzi au Mkunga

bila kusajiliwa na adhabu zinazotakiwa kutolewa. Aidha, Watumishi wa Umma wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 na Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika hospitali zetu kuna Mabaraza ambapo waathirika ama wahanga wa vitendo vibovu huwa wanakwenda kuripoti. Lakini akinamama wajawazito wanapotendewa vitendo vya kikatili wakienda kuripoti pale huwa wanatishwa. Sasa sijui Mheshimiwa Waziri hili analizungumziaje?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa suala hili la uzazi linagusa maisha ya mtu ama maisha ya watu moja kwa moja. Mheshimiwa Waziri anawaambia nini wanawake wa Tanzania, anatoa tamko gani dhidi ya hivi vitendo vya kikatili ambavyo wamekuwa wakifanyiwa na hawa baadhi ya Manesi na Wakunga?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwanza watumishi hawa ambao wanafanya kazi kwenye vituo vyetu na hasa Manesi ambao wanawasaidia akinamama katika kujifungua wengi wao wanafanya kazi nzuri. Lakini baadhi yao katika maeneo ya kazi wanatumia hizo lugha ambazo sio nzuri pamoja na kutofanya kazi vizuri na kukiuka maadili yao ya kazi.

Tatizo linapotokea mhusika anapotakiwa kwenda kuwasilisha malalamiko yake na akaona hajasikilizwa, Mkuu wa Kituo kile anaweza akawepo na kama hakuna huyo Mkuu wa Kituo kwenye hilo eneo basi nafikiri ngazi ya juu yake katika utoaji wa huduma pia inaweza ikafikisha. Lakini hata Mheshimiwa Diwani katika eneo hilo pia anaweza akapewa hizo taarifa na yeye mwenyewe akaweza kuwasilisha kupitia njia ambazo zinafahamika.

Tamko la Serikali kwa watumishi wote ni kuwataka na kuwasihi sana kwamba majukumu waliyopewa kuhudumia maisha ya watu au kutuhudumia sisi wananchi wote kwa ujumla wetu ni jukumu kubwa, zito na linahitaji nidhamu katika utendaji wake. Tunawaomba wote washiriki katika kufanya kazi hizi kama walivyokuwa wameomba kufanya kazi kwa uadilifu na kuhakikisha kwamba wanatekeleza wajibu wao kama ulivyozingatiwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha pia muda umekwisha.

Napenda kuwatambua baadhi ya wageni walioko humu ndani ya Ukumbi wa Bunge. Kwanza kabisa yupo Lizzy Tailor Mkuu wa Kitengo kinachosimamia Sekta ya Elimu, Afya na Maji cha *DFID.* Ambao *DFID* mwaka huu ndio Mwenyekiti wa *General Budget Support* kwa upande wa wahisani hapa Tanzania. Yupo hapa Dodoma kukutana na Kamati ya Huduma za Jamii kwa ajili ya kujadili masuala ambayo yanahusiana na mambo ya sekta ya Afya na Elimu. *So* Bi Lizzy yuko wapi asimame. *Okay, thank you very*

*much.* Wageni wengine ni walewale tuliowatangaza jana wageni wetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa sababu Wizara yao inaendelea leo. Halafu nina Mwenyekiti wa Kijiji cha Mkajenga Itigi Manyoni, sijui yuko wapi Mwenyekiti huyu anaitwa Bwana Malale Salum. Yupo Balozi wa Kijiji cha Mkajenga Itigi, Manyoni ambaye anaitwa Bwana Timbo Gundi. Ahsante sana karibuni wazee tunafurahi kuwaoneni hapa Bungeni. (*Makofi)*

Halafu wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo, hao ni wanafunzi 70 pamoja na walimu wao kutoka Shule ya Msingi ya Nkuhungu, Dodoma. Naomba wasimame wanafunzi na walimu wao. Ahsante sana naomba msome kwa bidii nashukuru sana. Yuko mgeni mwingine anaitwa Bwana Bashir Abdallah, kutoka Tarime, Mkoa wa Mara, sasa anakuja kama mgeni wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA) lakini hakueleza ni nani, sasa ni vizuri tukawa tunajua kwa sababu kanuni yetu inataka tueleze hawa watu ni watu gani?

Tangazo la kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 mchana kutakuwa na mkutano wao kwenye chumba Namba 231. Kwa hiyo, anaomba wahudhurie. Baada ya hapo sina tangazo lingine tunaendelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa 2012/2013
### Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge makusudio yetu leo ni kumaliza hii shughuli, kwa hiyo atakayeanza kuchangia wa kwanza asubuhi hii ni Mheshimiwa Rebecca Mngodo, atafuatiwa na Mheshimiwa Naomi Mwakyoma Kaihula, atafuatiwa na Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, atafutiwa na Mheshimiwa Salvatory Machemli, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati, hawa wanatosha kwanza. Lakini naomba nimtambue uwepo wa Mheshimiwa Joseph Selasini. Ahsante sana. (*Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge hata unapotaja jina nywele zinasisimka kwa sababu kweli amepata matatizo makubwa sana na ni kudra ya Mwenyezi Mungu kwamba leo tumeweza kukaa naye hapa maana yeye mwenyewe amepata matatizo. Mpaka sasa hivi mke wake nadhani bado yuko hospitali.

Lakini katika ajali iliyompata alipoteza mama yake mzazi, mama mkwe, shangazi yake na nafikiri alipoteza dada yake, kama watu watano nafikiri waliondoka kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, tunamshukuru Mungu kwamba yupo na tunamwombea mke wake apate afya njema na sisi wote tunafurahi kuwepo kwake. *(Makofi)*

Kwa sababu hiyo naomba nimwite Mheshimiwa Selasini kabla ya Mheshimiwa Rebecca. Ahsante sana.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hoja iliyo mezani. Kabla sijatoa mchango wangu napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuninusuru katika ajali mbaya iliyotokea tarehe 24 Mei, 2012.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mwenyezi Mungu anafanya kazi kwa kupitia wanadamu naomba nichukue nafasi hii niweze kuwashukuru baadhi ya Watanzania ambao walikuwa pamoja nami na familia katika kipindi hiki kigumu na kwa kweli wanaendelea kuwa nasi hadi sasa. *(Makofi)*

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muugano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alisikia kuhusu ajali hii na kwa kweli alinipigia simu nikasikia sauti ya Kiongozi aliye na uchungu na maneno ya faraja kutoka kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakuweza kufika kwenye misiba kwa sababu alikuwa safarini Angola nadhani, lakini alimtuma mwakilishi wake Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa William Lukuvi, ambaye alishiriki pamoja nasi katika mazishi, lakini pia Waziri Mkuu alivyorudi katika ziara yake alifika kutuhani pamoja na kutuona pale hospitalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, naye alitutembelea pale hospitalini alitupa maneno ya kutufariji kwa kweli tulifurahi sana. Nawashukuru Mawaziri wote kabisa kwa namna mbalimbali kwa njia ya simu, kwa njia ya ujumbe mfupi walinifariji na walitufariji, lakini pia walituma wenzao katika mazishi ya mama, namshukuru kama nilivyosema Mheshimiwa Lukuvi, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, alikuwepo pamoja nasi katika ibada na katika shughuli zote za mazishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru baadhi yao waliofika hospitalini, Mheshimiwa Nchimbi, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Mheshimiwa Gregory Teu, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara na wengine wote siwezi kukumbuka wote na muda ni mfupi basi naomba hao wachache basi iwe ni kama ishara ya kushukuru na kuwataja wote waliofika.

Nawashukuru viongozi wote watendaji wa Serikali ngazi ya Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Hai pamoja na Wilaya ya Rombo kwa kazi nzito waliyoifanya katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani zangu Serikalini ningependa kukushukuru wewe binafsi kwanza kwa maneno uliyosema asubuhi hii ya leo. Lakini ulimtuma mwakilishi wako kwenye mazishi Mheshimiwa Mwenyekiti Sylvester Mabumba alifika. Lakini hata wewe ulipomaliza shughuli zako

ulitutembelea pale hospitalini na kutuhani. Ahsante sana. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Katibu wetu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, nawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Bunge wa ngazi zote kwa jinsi walivyotuuguza na wanavyoendelea kutuuguza hadi hivi sasa. Kwa kweli lazima nikiri na niseme wazi kabisa Mheshimiwa Spika, Ofisi yako imefanya kazi kubwa na endelea kufanya kazi hiyo naomba Mungu awajalie muendelee kufanya hivyo hata kwa viongozi wengine siku zijazo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niwashukuru viongozi wa chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Mheshimiwa Mwenyekiti Freeman Mbowe, Mheshimiwa Katibu Mkuu, Viongozi wa Kamati Kuu na Baraza Kuu, viongozi wa Mkoa wa Kilimanjaro hasa Wilaya ya Hai, Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Hai pamoja na Mwenyekiti wa BAVICHA Wilaya ya Hai walikuwepo wa kwanza katika ajali walitusaidia sana katika shughuli zote. Wote nawaambia ahsanteni sana kazi mliyoifanya Mwenyezi Mungu ndiye atakayewalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru viongozi wa Chama cha Mapinduzi, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Alimtuma mwakilishi wake Mheshimiwa Aggrey Mwanri akatupa salamu za Chama cha Mapinduzi tulifurahi sana. Namshukuru Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-MAGEUZI mdogo wangu James Mbatia naye alikuwepo binafsi katika shughuli zote. Namshukuru mzee wangu Mwenyekiti wa Chama cha

*Tanzania Labour* Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Madaktari, Manesi na watendaji wote wa hospitali ya KCMC, Muhimbili, *MOI* na kule Hai ambako tulikimbilia kwa ajili ya kuokoa maisha yetu. Nawashukuru Maaskofu wa Jimbo Katoliki la Moshi Baba Isaac Amani. Namshukuru pia Askofu wa Jimbo la Same Baba Kimario.

Namshukuru Askofu wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini Askofu Shayo, nawashukuru Ma-*Sister* wa Bibi yetu wa Kilimanjaro wakiongozwa na Mama Phina walifanya kazi kubwa sana ya kuongoza maombezi ili tuweze kupata uponyaji wa kiroho ambao sasa tunao.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Watanzania wote kwa ujumla wao, lakini nimtaje mmoja tu ili kuwawakilisha wengine wote Mzee wetu Reginald Abraham Mengi. Siku ya tukio alipata habari akiwa Uingereza, akiwa safarini kwenda Marekani. Alitupigia simu akatufariji na kesho yake Kampuni yake ya *Bonite* ya pale Moshi ilituletea salamu zake rasmi. Kweli nimeonja upendo wake jinsi ambavyo amekuwa akizungumzwa na Watanzania wengi, namshukuru sana na tunamwombea Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia ukarimu alionao.

Nawashukuru wananchi wote wa Jimbo langu la Rombo kwa uvumilivu ambao wamekuwa wakionyesha hadi siku hii ya leo. Mwisho kabisa ninawashukuru sana dada zangu Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Susan

Kiwanga, Mheshimiwa Maulidah Komu, kwa kazi nzuri ambao wamekuwa wakifanya kwangu na kwa familia yangu hadi leo.

Mheshimiwa Spika, hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni hoja muhimu sana. Mimi kwa sababu nimebakiwa na dakika chache niseme tu yafuatayo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi lina matatizo makubwa sana ya kasma yao ya mafuta ya uendeshaji. Hili nimeliona sana katika mkoa wetu wa Kilimanjaro. Mfano siku nilipopata ajali gari iliyotuchukua majeruhi kutupeleka hospitali iliishiwa mafuta kituoni na namshukuru dereva na namsifu sana alibembeleza mwishoni alitoa hela yake ya mfukoni kwa ajili ya kuweka mafuta katika gari ya Serikali.

Naishauri na kuiomba Serikali iangalie sana jambo hili kwa sababu ni hatari magari haya yanayoshughulika na wahalifu kukosa huduma muhimu kama hii, vinginevyo watu watashawishika kufikiri kwamba huduma hii inapatikana kwa watu ambao sio waaminifu. Hili ni tatizo kubwa katika Wilaya ya Rombo na tatizo kubwa katika mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu huduma kwa askari. Tumekuwa tukisema kuhusu nyumba za askari. Mwaka jana nilisema na nilimwomba *IGP* hapa aende Rombo akaone aibu iliyoko Rombo, askari wanaishi kwenye mabanzi yameliwa na mchwa karibu yanaanguka kulikoni? Nyumba za Magereza zinaanguka wanaishi kwenye

mabanzi hawawezi kufanya kazi kwa morali Mheshimiwa Spika. Jambo hili lazima tuliangalie.

Sasa hivi tunazungumza habari ya Polisi Jamii. Basi ikiwezekana kwa sababu katika Serikali za Mitaa kuna *aspect* ya ulinzi tufanye maamuzi ikibidi tuwashirikishe wananchi. Pale Rombo tunajenga kwa nguvu za wananchi kituo cha Polisi kule Kirongo Samanga, Useri na kingine kule Mahida ikibidi katika *spirit* hiyo ya Polisi Jamii wananchi wahamasishwe tuweze kuwasaidia hao Polisi waondokane na hii aibu waliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ili kengele isinigongee ni kwamba Askari wanalalamika kuhusu vyeo vyao. Hawapandishwi vyeo kwa wakati muafaka na vilevile hawalipwi fedha zao wanapopata uhamisho. Sasa malalamiko madogo madogo yanaweza yakawaondolea morali.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, ni uhamiaji haramu. Nimeshasema na baadhi ya Mawaziri, nimeshawaambia ana kwa ana kwamba Wahamiaji haramu ni tatizo katika nchi yetu na sisi tulio mpakani tunaona, watu wanavushwa kwa njia za kinyemela kwa kutumia pikipiki, kwa kutumia baiskeli na ukikutana nao unaona kabisa hawa sio Watanzania. Ukienda Kariakoo unaona kabisa, hawa sio Watanzania, pale Bungoni unajua hawa sio Watanzania. Nchi yetu unaitumbukuza katika tatizo kubwa sana la ulinzi na usalama siku zijazo. Kama sisi hatujasomea mambo hayo ya kutambua huyu siye, vipi askari wetu? Mimi

naomba hatua zichukuliwe kuweza kudhibiti jambo hili ili lisije likahatarisha amani na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, narudia tena kukushukuru, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa kuendelea kuwa pamoja na sisi na nawahakikishia kwamba afya yangu na ya mke wangu zimeimarika, nina tatizo tu upande wa kushoto, bega halijakaa sawa, lina chuma, lakini mdomo kama mnavyoona, nina uwezo wa kusema. Kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Nassari, kazi ya Bunge siyo kubeba zege, kwa hiyo, wananchi wa Rombo wawe na hakika kwamba nitaendelea kuwawakilisha ipasavyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru sana Mungu kwamba ametupa nchi nzuri yenye utulivu na amani. Ni kweli kabisa kwamba, pasipo amani Taifa letu hatuwezi kupata maendeleo ya kiuchumi. Kwa hiyo, maisha ya wananchi yatakuwa ni duni. Tumeona katika miaka ya nyuma katika nchi jirani, kwa mfano Kenya wakati wa uchaguzi uliopita.

Mheshimiwa Spika, tumeona miaka iliyopita katika nchi za jirani kwa mfano Rwanda mwaka 1994 wananchi wa Rwanda waliweza kuuana na familia kupotezana; na hata Kenya katika uchaguzi uliopita, baada ya uchaguzi, tuliona kukosekana kwa amani, jinsi ambavyo familia ziliweza kutawanyika na watoto kutojua wazazi wao walipo. Napenda kusema

kwamba hakuna kitu chenye nguvu kama maneno. Kuna wakati hapa Bungeni kuna baadhi ya Wabunge wenzetu wamesimama na kusema kwamba vurugu au mauaji yanayotokea katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu yanasababishwa na CHADEMA. Hayo ni maneno ya uchochezi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rebecca, zungumza unayotaka kusema. Tumeshakubaliana hapa tuzungumzie *issues*. Haya maneno mengine yatataka majibu. Naomba tafadhali endeleo kuzungumza, hoja zako zitakuwa nzuri tu na unaweza kujenga hoja bila kuchokoza mtu.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kusema kwamba katika nchi yetu tumeweza kuona kwamba amani imekuwa ikipotea na nina kumbukumbu ya tarehe 5 Januari, 2011 pale Arusha ambapo vijana watatu waliuawa na askari. Ningependa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akihitimisha atuambie, wale askari ambao waliwapiga wananchi na vijana wa Arusha wamechukuliwa hatua gani? Kwa taarifa ya uhalifu wa Jeshi la Polisi ya mwaka 2012 inaonyesha kwamba hali ya uhalifu hapa nchini dhidi ya binadamu na mali zao inaongezeka kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kunukuu kwamba, kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2011 makosa dhidi ya binadamu yameongezeka kwa asilimia 14.5 na taarifa hizi zinaonyesha kwamba uhalifu dhidi ya binadamu ambao umeongezeka ni wizi wa mifugo na Mkoa unaoongoza ni Mkoa wa Mara kwa matukio

zaidi ya 24. Ujambazi Mikoa inayoongoza ni Mwanza, Shinyanga, Temeke na Tabora, kwa imani za kichawi matukio 127 Shinganya, matukio 105 Mwanza na Mbeya yalitokea kwa kipindi cha mwaka 2011. Napenda kuhoji, ni kwanini matukio haya yameongezeka kwa kiwango kikubwa wakati tunao Maaskari wa Jeshi la Polisi ambalo ni wajibu wake kulinda raia na kulinda mali zao?

Pia kwa kiwango cha imani za uchawi, ningependa kujua wale ambao walihusika kuwaua wanawake wazee wenye macho mekundu, walichukuliwa hatua gani, kama kuna upelelezi wowote ulifanyika? Pia napenda kujua walichukua hatua zipi, kwa sababu hatua hizo zinaweza zikasaidia wengine kuacha kufanya matukio hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna wizi wa kawaida ambao umeongezeka, ambao ili kuchukuliwa hatua upelelezi unahitajika. Lakini katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri tunaambiwa kwamba wapelelezi wapo wachache. Kwa hiyo, ningeshauri sana Jeshi la Polisi wapelelezi waongezeke, na kuna taarifa kwamba Maaskari wengine hushirikiana na wananchi kufanya wizi. Hivyo, ningetoa wito kwamba hali hii ichunguzwe na iangaliwe kama ni kweli kwa sababu kwa miaka ya hivi karibuni tumeona kwamba hakuna hali ya amani au hali ya kirafiki kati ya wananchi na Maaskari na hivyo wananchi wamekuwa na hofu kwenda kutoa taarifa za wizi unapotokea kwa kuogopa kwamba huenda Maaskari wana mahusiano na wale watu ambao wamefanya wizi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ningependa kuongelea kuhusu uhamiaji haramu hapa nchini. Uhamiaji haramu hapa nchini umeonekana kwamba kuna makundi mawili. Wanaofanya *transit* kwenda *South Africa* kupitia nchini kwetu na Malawi na wahamiaji ambao wanakuja na kukaa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia wahamiaji wanaoingia nchini na wanajihusisha na kazi kwa ajili ya kujiongezea kipato au wanaojihusisha na ujambazi na wizi na hivyo kurudi katika nchi zao.

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni tumesikia kwamba kwa kipindi cha mwezi mmoja tu, zaidi ya wahamiaji 420 wameingia nchini na kati ya hao, 42 wameonekana katika Mji wa Himo Mkoani Kilimanjaro. Pale Himo ninavyojua, kuna zaidi ya *guest house* 1,000. Kwa utafiti uliofanyika kupitia *UNDP* na *programs* ambazo zilirushwa katika televisheni, kuna *guest house* zaidi ya 1000 na hapa wamekamatwa wahamiaji haramu kutoka Ethiopia na Somalia. Ningependa kujua, kuna mikakati gani ambayo imewekwa na Wizara hii ili kuimarisha ulinzi na usalama katika mipaka yetu. Kwa sababu hatuwezi kuendelea kuishi kwa hofu, wasiwasi na mashaka kwa sababu ya wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ukienda Arusha katika mahotel mengi, hata pale Dar es Salaam kuna wahamiaji wengi kutoka Kenya ambao wanafanya kazi hapa nchini, na sielewi kikosi chetu kinachohusika na kutambua watu wanaoingia nchini kiholela wanafanya nini. Napenda watu hao wachunguzwe na

wachukuliwe hatua kwa sababu Watanzania wengi hasa vijana wanahitaji ajira na siyo kuwaruhusu wengine kuingia kiholela nchini na kuendelea kufanya kazi bila vibali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea kuhusu Mahabusu ya watoto iliyoko pale Upanga Dar es Salaam. Hali ya Mahabusu hii ningeomba ichunguzwe na Wizara kwa sababu ni mbaya. Watoto wamewekwa pale kwa muda mrefu, watoto wamechanganywa umri tofauti, wakike na wakiume. Naomba wale watoto wagawanywe, wasiwekwe pamoja wakike na wakiume. Au ikibidi, wale waangalizi basi waongezwe. Kwa sababu nilipofika pale, niliona kwamba wengi wameathirika kisaikolojia. Ukizungumza nao wengine wamefika pale kwa kusingiziwa na mama wa Kambo, Polisi akapewa chochote na watoto wamewekwa pale Mahabusu kwa muda mrefu. Naomba Idara inayohusika ifuatilie jambo hili ili watoto wale waweze kuondolewa pale ambao hawastahili kukaa pale kwa muda mrefu, waendelee na masomo yao.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kushauri kwamba badala ya kuwa Mahabusu ambapo watoto wanakaa na kucheza, kula na kulala, kitengo kile kibadilishwe kiwe kama sehemu ya mafunzo ili watoto wale wanapokuwa mahali pale, kabla ya kuondoka waendelee na masomo kama kawaida ili wasikose haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kusema kwamba siungi hoja mkono. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Si umeona hotuba yako umejadili vizuri, ukataka kuiharibu tu! Jamani msiharibu hotuba zenu, *natural* zinapendeza masikioni mwa watu. Hii ya mwisho ni *very natural*, nzuri kabisa. Sasa namwita Mheshimiwa Naomi Kaihula, atafuatiwa na Mheshimiwa Bahati Abeid.

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ili niweze kuzungumzia kidogo katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwanza kabisa, napenda kusema kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ni moyo wa nchi, ni moyo wa Watanzania, ni maisha yetu. Kwa hiyo, tunaitegemea sana katika mambo mengi ambayo yanaendelea; yenyewe iwe macho. Kutokana na hayo, napenda kusema kuiambia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwamba, "Haki huinua Nchi."

Mheshimiwa Spika, haki huinua nchi, haki huinua Watawala, haki huinua watu wote na kwa hiyo, nchi ikabaki na amani kama inavyosemwa ingawa sivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya hili, naomba nizungumzie suala moja katika hii Bajeti. Katika Bajeti hii naona kwamba kwa mwaka huu 2012/2013 fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni nyingi sana kuliko zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo. Ukiangalia ukurasa wa 19 utaona kwamba hela

iliyotengwa kwa matumizi mengineyo ni Shilingi bilioni 159 na iliyotengwa kwa ajili ya maendeleo ni Shilingi bilioni 11. Sasa Shilingi bilioni 159 za matumizi ambayo ni mengineyo, maana hayapo *specific* na wala hayaeleweki. Mimi nataka nieleweshwe hili baadaye. Lakini pia katika mchango wangu, nitazungumzia hili la kuweka fedha kiduchu kwenye mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, wakati huu lazima twende na hali halisi. Sisi kama sehemu ya dunia ya utawandawazi ni lazima tutenge fedha nyingi kwa ajili ya maendeleo. Nikisema maendeleo, ninamaanisha kwamba ni lazima *facilities* za Polisi anayelinda maisha yetu ya ndani, yaani uhai wetu, ni lazima awe na *facilities* ambazo ni *sophisticated*. Awe na vifaa ambavyo ni vya kisasa ambavyo vitamwezesha yeye kulinda wananchi. Mimi nasikitika sana kuona kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani badala ya kuwa na vifaa kama vile kuangalia mwizi anapoingia kwenye duka au anapoingia kwenye nyumba ambapo katika nchi nyingi zilizoendelea ndizo zinafanya, badala ya kusubiri mpaka mwizi aingie amwibie mtu, aondoke halafu ije ichukue muda mrefu kufanya upelelezi. Imefika wakati wa kuwa na vitu ambavyo vinazuia zaidi uhalifu kuliko kungojea mpaka uhalifu ukiwa umetendeka. Kwa hiyo, hili naomba tuelezwe wakati tutakapokuwa tunapatiwa majibu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni matumizi ya nguvu ya Polisi. Unakuta Polisi ni ndugu zetu, ni rafiki zetu, tunapaswa tusiwe tunawaogopa. Lakini kusema ukweli, sasa hivi Polisi wanaogopewa badala ya watu

kuwafuata, kwa sababu wenyewe wanapokwenda kukamata mwizi au mtu yeyote, wanatumia silaha kali za moto. Kwanini inakuwa hivyo? Polisi ni rafiki, angalia kwenye nchi zilizoendelea, hata kwenye nchi za wenzetu, kwa kweli Polisi wako tayari kutoa maisha yao kuliko kutoa ya mtu mwingine ili mradi waweze kumkamata vizuri kwa amani kuliko kutumia nguvu nyingi. Kumpiga risasi, tena nashangaa Polisi wetu huwa hawapiti Shule na Vyuo vya kuonyesha mahali pa kupiga. Kwa kawaida, Polisi huwezi kumpiga mtu unamlenga kwenye moyo utegemee kwamba atapona. Huyo ni Polisi gani? Ndiyo maana nasema, Polisi hawa lazima watengewe fedha za maendeleo, wapewe vifaa ambavyo vitawasaidia, anapokwenda kushughulika na vurugu, asiwe kama anashughulika na jambazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu anakwenda kusimamia pengine maandamano, anakaa na silaha ya moto! Uliona wapi? Huwezi ukakaa na silaha ya moto ukaona mtu atapona. Polisi tunawaomba, katika kushughulika na sisi wananchi, tunawategemea wasiwe na vitu vya moto vitakavyotuua, kwa sababu roho ikishatolewa, hairudi tena. Jamani kuna duka la roho? Haya matukio tumekuwa tukiyaona katika sehemu nyingi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la Polisi na siasa. Ndiyo maana sisi kwenye sera ya CHADEMA inataka kutenganisha Serikali na Chama kwa sababu Mawaziri ni Serikali, Wakuu wa Wilaya ni Serikali, Wakuu wa Mikoa ni Serikali, sasa sisi tunataka hawa watenganishwe na dola, yaani *oppressive instrument of the state* kwa sababu wanaweza wakatumika

vibaya. Kumekuwa na *tendency* sasa hivi, unakuta Polisi, watu wanavyoona wanakuwa kama wanaegamia kwenye Chama fulani. Kiwe ni Chama kinachotawala ama Chama ambacho kinatarajia kutawala. Sasa hili jambo siyo zuri, linaleta tishio. Ni tishio kwa nchi, amani ile tunayoisema itatoweka. Utakimbilia kwa nani? Maana haijaandikwa kwamba huyu Polisi ni wa CHADEMA, CCM au NCCR au Chama Fulani.

Kwa hiyo, watu wanakuwa na wasiwasi. Hiyo siyo kazi ya Polisi, Polisi, tunawaomba wakati wanaposhughulika na kazi zao hasa wanapokuwa wanasimamia maandamano ya aina yoyote, tafadhali sana, wajaribu ku-*keep aloof,* wajitenge kabisa na wasionyeshe kwamba wapo upande fulani. Lakini hasa wasiwe na vyombo vya moto vinavyoua. Unasimamia maandamano, kwanini unakuwa na silaha ya moto? Hapo umemlenga nani kwamba utamuua? Hii imetokea, na ni jambo ambalo ni baya, linaonyesha sura mbaya kwenye anga za Kimataifa. Kwa hiyo, hili tujitenge nalo. Haya mambo tulikuwa tunayachukia sana wakati ule wa *apartheid* kule *South Africa.* Wakati ule chombo cha dola kilitumika na watawala na wale waliwapa chombo cha dola mamlaka ya kuua, kupekua na kufanya chochote. Lakini mbona tulilaani sana hiki kitu? Sasa kinakuja kinyemela hapa, Polisi anakuwa na mamlaka ya kufanya anavyotaka. Tunapozungumza hivi, mnaelewa tunazungumza nini kwa matukio mbalimbali ambayo hatuwezi kuyasema ambayo yako Mahakamani. Inavyoelekea matatizo yenyewe ni haya ambayo yako sasa.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuzungumzia zimamoto. Zimamoto yetu inatuchekesha sana. Ninawakilisha Mkoa wa Mbeya, Mkoa wa Mbeya umepata majanga makubwa ya kuunguliwa masoko, nyumba kila wakati, lakini utakuta kila mara wale Zimamoto wanakuwa na tatizo la kutokuwa na maji, watakuwa na tatizo la kutofika, watakuwa na tatizo la aina fulani. Kutokana na bajeti hii, mimi naona tatizo lao kubwa ni kwamba hawana vyombo vya kisasa *(modern facilities)* vinavyokwenda na wakati na kuweza kufika mapema na kuweza kuzima moto. Kwa nini wategemee maji kila wakati? Kwani hakuna aina nyingine ya *facilities* kama vizima moto? Kwa mfano, Dar es Salaam majengo yanayojengwa ni *skyscrapers.* Majengo yale yanakwenda juu, lakini zimamoto iliyoko pale ni geresha kwa sababu majengo hayo yakipata tatizo sidhani kama hao zimamoto wanaweza kufanya wokovu wowote wa maana.

Mheshimiwa Spika, hawawezi kufanya wokovu wowote kutokana na kwamba vyombo vyao ni vya zamani, vya ajabu, na kila wakati wanapokuja wanaleta mtafaruku na wananchi wenye hasira kwa sababu aidha, wanakuwa wamechelewa kwa ajili ya Mitaa au hawana maji, wananchi wanapata hasira na kutaka kuwapiga. Kwa hiyo, naomba Zimamoto wawe na *facilities* za kisasa. Kwa nini wasitafutiwe hata *helicopter* ili wawe wanazima moto kwa *helicopter?* Ninatoa wito kwa Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi ifanye kitu hiki haraka kabla hayajatokea majanga na majanga mengine yanayotokea kwenye meli kama walivyoeleza watu wengine, kwamba hizi fedha za maendeleo ndiyo zinapaswa ziwe nyingi, siyo

za matumizi mengineyo. Hayo matumizi mengineyo, Shilingi billioni 159 na hii Shilingi bilioni 11, hivi mnaona kuna usawa hapo? Tunadanganyana!

La mwisho na ambalo ninapendekeza wakati wa kuandikisha raia, napenda chombo cha nje kiwepo katika kufanya *monitoring.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja mpaka majibu yapatikane. *(Makofi)*

**MHE. BAHATI A. ABEID:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Napenda nimpongeze Waziri, Naibu Waziri na Watendaji kwa hotuba hii nzuri, lakini pia napenda niwapongeze Jeshi la Polisi kwa kufanya kazi nzuri sana ya kulinda raia na mali zao. Tanzania yetu iko shwari, ina amani na utulivu, lakini kwenye kizuri, hapakosi kasoro. Yapo maeneo yana matatizo, lakini eneo kubwa la nchi yetu ni amani na utulivu.

Jeshi hili la Polisi wanafanya kazi kwa malengo ya kuimarisha hali ya usalama wa nchi hii, ingawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Naiomba Serikali, Jeshi letu ni dogo sana kulingana na Watanzania tuliopo, lakini wanajitahidi kutafuta kila uwezekano wa kuimarisha hali ya usalama wa nchi hii. Naomba sana Jeshi hili lipewe vitendea kazi kama wenzangu walivyosema. Jeshi hili halina magari ya

kutosha. Hata kama mwananchi akitoa taarifa kwa Askari Polisi kusema kuna tatizo katika eneo fulani, wakati mwingine wanashindwa kuwafuata wananchi wenye matatizo kwa sababu hawana magari, lakini hawana *radio call.* Kwa upande wa Zanzibar hakuna *radio call,* Askari wanatumia simu zao za mikononi na hakuna kifungu chochote kile wanacholipwa na Serikali kwa ajili ya simu zao hizo kama walivyosema wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kitabu hiki cha Waziri, ukurasa wa 22 nimeona malalamiko ya wananchi juu ya rushwa. Rushwa ni adui wa haki. Malalamiko haya ni mengi sana kwa Jeshi letu la Polisi, ni malalamiko 625, matatizo haya 625 yameshughulikiwa na Askari 68 wamefukuzwa kazi. Hawa ni wengi sana. Nchi yetu inatoa mafunzo ya kijeshi kwa vijana wetu hawa wa Jeshi la Polisi, halafu wanakutwa na matatizo kama haya, Askari 68 kufukuzwa. Nchi hii itakuwa inazalisha vijana wenye matatizo ambao wamepatiwa mafunzo ya kijeshi. Leo hii Askari 68 wamefukuzwa, ni wengi sana kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vijana hawa wameshapata mafunzo ya kijeshi, leo hii wanafukuzwa katika Jeshi la Polisi. Walipokuwa ndani ya Jeshi walikuwa na mazingira magumu ya mishahara na posho, leo wanatoka nje ya Jeshi wakiwa wamepata mafunzo ya kijeshi. Mimi nimewaza sana, lakini nimejiuliza, tatizo ni nini? Tatizo ni mishahara mibovu ya Jeshi hili, tatizo ni kukosa posho! Kama nilivyozoea kusema katika Bunge hili, kuwa Askari hawana muda wa kufanya miradi mbadala, ni lazima kile tunachopitisha hapa Bungeni

kama ni posho wapewe, lakini sitaki niseme posho tu, nasema waongezewe mishahara. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Rais wangu Jakaya Mrisho Kiwete ni wakati muafaka sasa kuangalia uwezekano wa Jeshi hili la Polisi kuwaongezea mishahara kiaina yake ili wanapostaafu waweze kupata kiinua mgongo cha kuwawezesha kufanya biashara endelevu.

Mheshimiwa Spika, Askari wetu wadogo wanapata mishahara midogo sana, hata wakistaafu, kiinua mgongo ni kidogo, hawawezi kufanya biashara endelevu, matokeo yake tunawaonea huruma. Askari hawa wanatoka kwenye Jeshi, wanalinda kwa kutumia silaha, lakini utawakuta wanalinda mali za watu kwa kutumia marungu, wanadhalilika, lazima tuwaangalie kwa jicho la huruma sana, wanafanya kazi kubwa. Mimi nashangaa, Mbunge anasimama hapa anasema ooh, Askari wanapokwenda katika maandamano haya, wasichukue silaha wakati wananchi wengine wanakuwa wameweka visu mfukoni, wameweka mapanga kiunoni, Askari anakwenda kulinda nini na maandamano mengine yanakuwa ya vurugu, tumeshuhudia Askari wetu kukatwa vichwa; Askari afanye nini? Alinde kwa rungu? Haiwezekani Askari waendelee kuchukua silaha na waendelee kufanya kazi zao. Raia mwema akienda kwenye maandamano hachukui silaha! Askari waendelee kufanya kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, fedha za ukarabati hatuoni zikifanya kazi. Mkoa wangu wa Kaskazini tangu Ukoloni, kuna majengo hayakarabatiwi, kwa mfano Mkokotoni, kuna majengo hayakarabatiwi. Lakini kuna

Kituo kikubwa cha Polisi pale Mjini Ziwani. Kituo hiki ni Makao Makuu ya Polisi kule Zanzibar, kinafanyiwa mafunzo pale, kina silaha, lakini uzio wa kituo hiki kila pembe kuna matundu ya kupitia watu, kuna ulinzi gani wa kuona pale ni wakati gani mtu mbaya anaingia, wakati kituo hiki kina silaha kubwa? Naomba pesa za ukarabati zikajenge uzio, tena wa ukuta kwenye kituo hiki kikubwa ambacho ni Makao Makuu pale Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linajitahidi kuajiri vijana wetu. Nasema wakati umefika sasa tuajiri vijana kuanzia *Form Four,* lakini vijana hawa wasomi, wenye *Diploma* na *Degree* na kuendelea, waajiriwe kwa wingi. Dunia imebadilika, tunakwenda na sayansi na teknolojia, matokeo mengi Wizarani yanajitokeza; haiwezekani Askari umemwajiri miaka kumi na kuendelea, unakuja kumkata mshahara miezi mitatu, minne na kuendelea bila kosa lolote, hujamtuhumu, hujamwonya, unamkata mshahara bure. Wafanyakazi wamezeeka, hapo ajirini wenye kujua kutumia kompyuta. Kama komputa ina *virus,* imefuta, hao Askari wasiopata mishahara haiwezekani, ajirini wataalam, ajirini vijana, kwani vijana wengi wapo Mitaani hawana ajira na wamesoma. Waajirini hao!

Mheshimiwa Spika, nasema, nitasema kidogo tu, mengi yameshasemwa, sipendi kurudia. Baada ya hayo machache, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, nisikupotezee muda kwa kurudiarudia. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nadhani uko sahihi, kwa sababu Kanuni ya 60 (9) inasema, kwa Mbunge ni marufuku kurudiarudia maneno aliyoyasema mwenzake. Naona wote mnaendelea, mishahara na nini, na nini, kila mtu akisimama ni mishahara na nyumba mbovu, bila hata kusoma kanuni. Sasa namwita Mheshimiwa Salvatory Machemli.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimikwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii adimu. Kwanza, awali ya yote nitoe pongezi za dhati kabisa kwa wapigakura wa Jimbo la Ukerewe walioko ndani na wale walioko nje, lakini kwa Wakerewe kwa ujumla kwa *support* yao wanayonipa namwomba Mwenyezi Mungu awajalie afya njema waendelee kuniombea afya njema. Naendeleza kauli yangu, wanaifahamu kwamba mimi ni sauti ya wasiosikika *(voice of voiceless)* lakini leo Wakerewe wanasikika ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Jeshi la Polisi ni kulinda usalama wa raia na mali zao, lakini kauli hii imekuwa na tafsiri na maana nyingine tofauti kabisa kwa wananchi wa Tanzania kwa leo. Nita-*base* kwa wananchi wangu wa Jimbo la Ukerewe kwa kuwa umetuambia ni marufuku kurudia maneno ya watu wengine, mimi ninakuja kivyangu kwa sababu ni sauti ya Wakerewe kwa ujumla. Jeshi la Polisi kwetu Ukerewe lina tafsiri mbaya sana na Wakerewe wanaendelea kukosa imani na Jeshi la Polisi. Kuna matukio mengi ambayo kwa idhini yako naomba niyataje kwa kifupi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009 kulitokea mauaji katika Kisiwa cha Izinga, watu 15 raia wasiokuwa na hatia walipoteza maisha yao katika Kisiwa kile. Silaha iliyotumika ni silaha ya kivita, ni silaha ya kijeshi *SMG* Jeshi la Polisi kwa namna moja au nyingine lilihusishwa. Wananchi wa Jimbo la Ukerewe wanao ushahidi wa kutosha kabisa uliowahusisha Askari wa Jeshi la Polisi, na kilichofuatia pale baada ya Askari wale kuhusishwa, waliokuwa kwenye Kituo cha Nansio baada ya wiki moja walihamishwa. Nauliza kwa kuwawakilisha Wakerewe kwamba hizo pesa zilizotumika kuwahamisha wale Askari wa Kituo cha Nansio akiwemo *OCD* Kwayu zilitoka wapi kwa ghafla kiasi kile? Wakerewe tunahitaji majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukio lingine lilitokea mwezi wa Desemba, 2010 katika Kisiwa cha Namanga. Hawa watu waliouawa mbele ya *OCD* walihusishwa na ujambazi katika Kisiwa cha Ukara. Hawa watu walihusiana na Askari Polisi aliyejulikana kwa jina moja la Ismaili, aliyekuwa kwenye Kituo cha Ukara walifanya ujambazi, waliwadhalilisha wananchi, waliwavua nguo na waliwakata mapanga. Matokeo yake, baada ya kufikishwa kwenye Kituo cha Polisi, Polisi walioandaa mashtaka hawakuwahusisha hawa watuhumiwa, wakaachiwa huru. Wananchi wenye hasira waliwateremsha kwenye gari la Polisi wakawateketeza wote wane. Hii ni kwa sababu wananchi hawakuwa na imani tena na Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, juzi tarehe 15 mwezi wa Saba, silaha kali tena aina ya *SMG* zimetumika kupora mashine 15 katika Ziwa Victoria katika Visiwa vya

Ghana, Izinga na Kamasi. Jeshi la Polisi limehusishwa tena! Ni kwa nini Askari Polisi ambao tunawaamini, wanalipwa mshahara wetu, leo wanatumia silaha zetu ambazo tunatumia na kununua kwa kodi zetu kwenda kuangamiza maisha yetu? Tunaomba Waziri mwenye dhamana aliangalie kwa makini sana, kwa wale Askari anaowaelekeza kwenda kulinda mipaka yetu, kwenda kulinda usalama wa raia, ndio wanaohusika kwenda kuondoa maisha ya raia wetu. Baada ya kusema hayo, naomba sasa nihamie kwa Askari wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai.

Mheshimiwa Spika, nina wasiwasi sana na Askari hawa juu ya ufahamu wao au juu ya uelewa wao, kama siyo kufanya makusudi, wanapoandaa mashtaka ya makosa ya jinai. Ninalolitambua, mimi sio Mwanasheria sana, lakini ninachokifahamu, Askari wanapoandaa makosa ya jinai, yanahusisha pande mbili kuu. Yanahusisha mlalamikaji kwa maana ya *complainer* na yanahusisha mlalamikiwa kwa maana ya *accused.* Hapo ndipo Askari anapokwenda kusikiliza pande zote mbili, anajua kosa hili lime-*base* upande gani. Je, ni kosa la kudhuru mwili baada ya kumsilikiliza *complainer?* Je, ni kosa la shambulio la mwili au ni *attempted murder?*

Mheshimiwa Spika, cha ajabu ambacho kinanipelekea mpaka nianze kutoa malalamiko dhidi ya hawa watu, na kuwa na wasiwasi na ufahamu wao wa kuandaa mashtaka ya jinai ni pale ambapo wanasikiliza upande mmoja, halafu kesi inakwenda Mahakamani, inatia wasiwasi, tumekuwa na makosa mengi ya jinai ambayo leo yako Mahakamani, na sisi

tunazuiwa kuhoji kwa mujibu wa Kanuni zetu. Tukasemee wapi, kama siyo hapa? Tukio la tarehe 31 Machi, ambalo mimi ni muhanga, sijawahi kuitwa na Jeshi la Polisi kuhojiwa kwamba nimejeruhiwa kiasi gani, na sehemu gani, na wapi, au nikawatambua wale watu waliohusika kama walalamikiwa. Leo kesi ipo Mahakamani, nisihoji nani amewatambua wale! Kuna kitengo gani ndani ya Jeshi lile kinachoweza kutambua au wana *DNA* gani inayotambua mimi niliguswa na nani katika mwili wangu? Huku ni kutunyima haki ya kuhoji.

Mheshimiwa Spika, naomba wakati mwingine tuachiwe wazi tulihoji Jeshi la Polisi kwa kile wanachokifanya. Hatuhoji Mahakama, tunahoji Jeshi la Polisi katika kuandaa mashitaka ya jinai.

Mheshimiwa Spika, kwa haya yanayotokea kwa Jeshi la Polisi kuandaa shitaka kwa kuangalia upande mmoja, ndiyo yanayopelekea wananchi kuchukua sheria mkononi, kwa sababu hawaridhiki na Jeshi la Polisi jinsi linavyoandaa mashitaka.

Mheshimiwa Spika, kulingana na matukio mengi yanayotekea katika Ziwa Victoria nina wasiwasi na utendaji kazi wa Kitengo cha *Police Marine*. *Police Marine* wana vifaa vya kutosha katika Ziwa Victoria, lakini hawajawahi kukamata hata mtuhumiwa mmoja, bali huja nyuma baada ya majambazi kuwa yameshachukua mali, yameua watu, ndiyo wanatokea. Huenda ukawepo ushirikiano kati ya *Police Marine* na majambazi. Naomba kitu kimoja kupitia Wizara hii. *Police Marine* wasikae nchi kavu, wahalifu

wanakwenda majini. Rudisheni hiki kitengo Ukerewe kwa sababu ndiyo katikati ya Ziwa Victoria na boti ya doria ikae katika Ziwa Victoria, nikimaanisha Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, Askari wa Usalama Barabarani wamekuwa wakikamata wahalifu wa makosa ya barabarani na kuwatoza faini kwa kuwapa *notification.* Naiomba Wizara kupitia Jeshi hili, kama mmewaamini kuwapa tochi, mkawaamini kuwapa silaha za kulindia wahalifu, waaminini na kuwapa stakabadhi za vitabu ili mtu anapokosea, wasimpe *notification*, wampe stakabadhi ili watu walipe kihalali. La sivyo, tutaendeleza rushwa. Tuwape na kamera zinazoonesha picha. Unapita, unakutana na Askari wa Usalama Barabarani Kituo 'A', ukienda ameshamkamata mtu aliyepita mwenye gari 'B', anakuonesha kwamba ulikuwa *speed* 75. Nitatambuaje kama ni gari yangu? Nikioneshwa gari ya jamaa aliyepita! Hapo wanachotaka ni kuchukua hela. Naomba kupitia Wizara hii, watafutieni Askari kamera zenye picha, zinazoonesha gari namba fulani ilikuwa *speed* kadhaa, ili kuondoa rushwa katika Jeshi hilo.

Mheshimiwa Spika, nimewasikia Wabunge wengi wakiomba kupanuliwa kwa Magereza…

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Silvester Kasulumbayi na Mheshimiwa Khatib Said Haji na Mheshimiwa Haji Khatib Kai pia ajiandae.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi na nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri, Watendaji na Makamanda wote wa Jeshi la Polisi. Siwezi kuwa nimemtendea haki nisipomshukuru *RPC* wetu wa Mkoa wa Iringa - Kamanda Michael Kamhanda. Kwa kipindi kifupi ameonesha umahiri wake, nafikiri hata Mheshimiwa Waziri anajua.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli japokuwa umesema kwamba Kanuni haziruhusu, lakini tusipowasemea Askari wetu wa Mkoa wa Iringa hawatatuelewa. Kwanza kabisa, naomba nianze na majengo ya Polisi.

Mheshimiwa Spika, nilishaleta hata swali hapa Bungeni, nimekuwa nikikereka sana na jinsi Askari wetu wanavyoishi kwa shida katika majengo yao. Kuna Kikosi cha Kihesa, majengo yao ni mabovu sana, Kikosi cha Mjini wanaishi kwa mazingira magumu sana, hata ukienda Wilaya ya Mufindi bado majengo ya Polisi ni mabovu sana. Ukienda Wilaya ya Kilolo, haijajengewa hata ofisi katika Makao Makuu. Makao Makuu ya Polisi yapo *TAZAMA pipeline*. Kwa kweli hatuwatendei haki wananchi wa Kilolo, kwa sababu kuna wananchi

wanaotoka maeneo ya mbali ambao wanatakiwa wasafiri kwenda Makao Makuu ya Polisi, Taasisi zote zimeshajenga Makao yao Makuu katika Wilaya, isipokuwa Jeshi la Polisi. Kwa nini Jeshi la Polisi halipewi kipaumbele katika mambo mengi sana? Ukifuatilia hotuba kuanzia jana, Waheshimiwa Wabunge wote tunalalamikia jambo moja. Naomba sasa hivi tuwape kipaumbele hawa Askari wetu kwa sababu wamekuwa wakitulinda na wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana, usiku na mchana wanatulinda.

Mheshimiwa Spika, ukienda katika majengo ya Askari kuna vitu vingine ningevisema, lakini naona aibu. Wale Askari wanarudi nyumbani wamechoka, anashindwa hata kukandwakandwa na mama, chumba kimoja anakaa na watoto wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, linguine, Iringa *Police Post* zipo chache mno. Naomba kwa kweli hili jambo liangaliwe. Kuna ujambazi mdogo mdogo unafanyika Iringa Mjini. Nililalamikia hata nilipokuwa naongea kwenye hotuba ya Waziri Mkuu kwamba kuna msitu wa Kihesa - Kilolo, kumekuwa na matukio madogo madogo ya ujambazi na watoto wamekuwa wakinyang'anywa mpaka ada zao za shule. Ukitoka Nduli hakuna Kituo cha Polisi, ukienda Kihesa hakuna Kituo cha Polisi, sasa hawa watoto tunawaweka katika mazingira gani? Naomba pesa iongezwe katika Mkoa ule na Vituo vya Polisi viweze kujengwa kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, tumejengewa barabara nzuri sana ya Ruaha, ile barabara chini yake kunakatiza, lakini sasa hivi hakuna amani. Wanasema ni shamba la

bibi, kuna ujambazi mdogo mdogo, wanakabwa roba kwa sababu hakuna Kituo cha Polisi. Ipogolo kulikuwa na Kituo cha Polisi, lakini kutokana na ukosefu wa nyumba za Askari, wamekigeuza sasa wanakaa Askari. Kwa hiyo, ningeomba pesa ziongezwe, apewe Kamanda wetu wa Mkoa wa Iringa ili aweze kufanya kazi yake kwa umahiri.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie pia kuhusiana na vifaa. Kwa kweli Askari wetu wamekuwa hawana vifaa vya kisasa. Ukienda hata katika Vituo vya Polisi, utakuta wananchi wanatakiwa wachangie mafuta ili waweze kushughulikiwa kesi zao. Hili jambo linawafanya Askari waonekane kama vile wanaomba rushwa, lakini kumbe sasa wafanye nini? Askari ili aweze kufanya kazi yake vizuri, anatakiwa awekewe mafuta, gari linatakiwa liwepo *standby* kwa ajili ya matukio mbalimbali, ziwepo karatasi za kuandikia kesi, lakini watu wanachangia mpaka karatasi. Wakiombwa hela ya karatasi, wanaambiwa kwamba hiyo ni rushwa. Tunawaweka Askari wetu katika mazingira gani?

Mheshimiwa Spika, naomba Askari wetu waongezewe posho za kutosha, waongezewe mishahara ya kutosha ili wafanye kazi zao vizuri, hata nyumbani kusiwe na matatizo. Anapokwenda kazini ajue kweli nina pesa ya kutosha, hata akina mama wenzetu wale ambao sisi tunawawakilisha, wanalalamika kwamba hawaachiwi chochote nyumbani.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu dawati la kijinsia. Nashukuru sana kwamba pale Iringa nilifanya ziara nikatembelea Kituo cha Polisi nikakuta kuna dawati, lakini nilipoongea na akina mama wa Mufindi na sehemu nyingine, kwenye Vituo vingine bado havijawekewa dawati la kijinsia. Kuna matukio mbalimbali yanafanyika kwenye maeneo mbalimbali ambayo wanashindwa kuyaripoti. Niliuliza swali hapa siku moja na nikaambiwa kwamba matukio mengi hayaripotiwi kwa sababu wanawake wanaona aibu kwenda kuyasema kwa wanaume. Kwa hiyo, naomba hata huko Wilayani, hili dawati liende sehemu zote, na kwenda sehemu hizo maana yake ongezeni bajeti katika Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu Jeshi la Magereza. Jeshi la Magereza hali yake ndiyo hivyo hivyo. Ukiangalia nyumba zao zinasikitisha kwa kweli. Makazi yao ni mabaya, wanaishi kwenye mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie pia kuhusiana na ukosefu wa Mahakama za Watoto na Magereza. Watoto wetu wamechanganyika Magerezani na watu wazima. Gereza la Iringa nafikiri linaweza kuchukua watu kama 510, lakini kuna watoto 11 wamechanganyika na watu wazima. Hawa watoto tunawaweka katika mazingira gani? Hawa watoto wanajifunza nini?

Mheshimiwa Spika, mnaona vitendo wanavyofanyiwa kule ndani Magerezani? Wanalawitiwa, wanafanyiwa vitendo vya ukatili! Sasa hawa watoto tunakwenda kuwafundisha au tunakwenda kuwafanya nini? Kwanini hata wasifungwe vifungo vya nje ili waweze hata kufanya usafi, kufanya kazi za jamii, ili baadaye hawa watoto waendelee kusoma?

Mheshimiwa Spika, hili linatia uchungu sana. Ukiangalia, hata historia za hawa majambazi sugu wengine walifungwa kwenye hivi vituo, wakitoka pale wanakuwa wamechanganyikiwa. Hii nchi tunaipeleka wapi? Tunataka tuwe na watoto ambao ni majambazi sugu?

Mheshimiwa Spika, mimi ni mama, hili linanisikitisha. Naomba ufanyike utaratibu, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu atuambie hawa watoto ambao wamefungwa kwenye jela za watu wazima wanawekewa mpango gani?

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Faida alipozungumzia mpango wa watoto ambao wanazaliwa Magerezani. Wale watoto nao wanakuwa wamefungwa pia, hii inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, kule Magerezani kuna watu wana taaluma zao, kuna wajenzi, na kadhalika. Kwanini wasitumike kujenga majengo yetu? Mbona nchi nyingine wanawatumia halafu baadaye wanakuja kupewa ile mishahara? Maana yake wanapotoka wanakuwa hawana kitu chochote,

wanatoka na wameugua tu, hawana kitu chochote. Kwa nini kama watalaam wapo, tusiwachukue? Kwani wana makosa gani? Utakuta wengine ni kwa sababu hawana uwezo wa kupata Wakili wa kuwatetea kesi zao.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kueleza kuhusiana na upelelezi kuchukua muda mrefu sana katika Magereza yetu. Utakuta mahabusu wanatelekezwa katika Mahakama za Wilaya kwa sababu ya kukosekana magari. Kwa kweli itafutwe gari nzuri ambayo inawachukua na kuwarudisha. Utakuta mahabusu anashinda kutwa nzima hajala chochote, ametelekezwa kwenye hizi Mahakama nyingine za Wilaya. Hili naomba pia liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie kuhusiana na kikosi cha Zimamoto. Kikosi cha Zimamoto kila sehemu ni hoi hoi. Ukiangalia Iringa, yale majengo yao, wafanyakazi wenyewe wanasikitisha kwa kweli. Naomba nao wapewe umuhimu na wawekewe fungu la kutosha, mimi nafikiri hata chai huwa hawanywi! Gari la Zimamoto sijawahi kuona linapashwa moto kila siku liko pale. Ndiyo maana hata matukio yakitokea, gari linakuwa halina mafuta, gari halina maji na sijui hata kama mazoezi wanafanya. Kwa hiyo, naomba sana, sasa hivi kumekuwa na matukio mengi sana ya moto, lakini utaona tunatia aibu, vikosi vingine vya kiraia vinakuja kuzima moto, wakati tuna kikosi ambacho tunakitegemea siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spka, ningeomba pia somo la uraia lizingatiwe katika shule zetu. Somo hili likizingatiwa kuanzia elimu ya msingi, watoto wakawa wanakua wanajua elimu ya kiraia, itatusaidia hata kufichua maovu.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba kuzungumzia kuhusu Polisi Jamii. Hawa watoto wanafanya kazi vizuri sana. Kuna kikosi kipo pale Kinodombi Iringa kinafanya vizuri, lakini pia wapo wasomi. Kwenye hizi ajira wapewe ajira kwa sababu wengine ni Kidato cha Nne, Kidato cha Sita na wana sifa. Namwomba Mheshimiwa Waziri aje afanye ziara Iringa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, lakini mpaka Waziri aje atembelee Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mpo Bungeni, acheni habari za kuzungumza kama mpo nje.

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wapigakura wangu wa Maswa Mashariki, nawashukuru sana kwa namna ya pekee wanavyoonesha kulisaidia Jeshi la Polisi katika Wilaya ya Maswa.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuwasifia Polisi walivyo waaminifu na kwa namna ya pekee wanavyotimiza majukumu yao ya kutulinda. Ninaamini kabisa, kama itatokea siku Serikali hii ikajichanganya, ikaamua kuweka hata saa moja tu ya likizo kwa Polisi wote, naamini nchi hii itashuhudia kuona mauaji ya ajabu. Lakini panakuwa na utii, kwa sababu kuna Polisi

wanaotimiza majukumu yao. Tatizo langu ni kwa Serikali inayosema ina usikivu, imethubutu na inasonga mbele, tatizo langu lipo hapo!

Mheshimiwa Spika, kama Serikali hii ingekuwa sikivu kama inavyodai, ninaamini migogoro yote hii inayotokea kwa Polisi isingekuwepo. Polisi wameachwa kama bata. Mtoto wa bata hujitafutia mwenyewe chakula, mama yake huwa hana shughuli naye. Kwa hiyo, hata Polisi makosa yanayoendelea yanatokana na kukosa uelekezi wa mama yake anayeitwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 nilipokuwa nachangia katika Wizara hii, niliweza kuikumbusha Serikali inayojiita Serikali sikivu, nikawaambia, Wilaya ya Maswa ilianzishwa na Wakoloni mwaka 1927, leo ni miaka 85 iliyopita; nikawaambia kwamba kwa bahati mbaya sana Wakoloni walipoanzisha Wilaya hiyo walisahau kutimiza jukumu lao la kisheria la kiserikali la kuwajengea miundombinu Askari Polisi pamoja na Askari Magereza hasa nyumba zao za kuishi. Niliwaambia Serikali kwamba Wilaya ya Maswa Polisi hawana Kituo cha Wilaya cha Polisi, hivi sasa Polisi wanabangaiza kufanya shughuli zao za kipolisi kwenye vijumba vidogo vibovu vilivyokuwa vinatumika kipindi cha Wakoloni kwenye Idara ya Kilimo na Mifugo. Nikasema Mkuu wa Polisi wa Wilaya pamoja na juhudi zake zote anapatikana kwenye Ofisi ndogo sana iliyopo Bomani kwa Mkuu wa Wilaya. Mkuu wa Polisi huyu anafanya kazi katika mazingira magumu sana kulingana na chumba alichopewa. Hawezi kuweka mambo yake vizuri, hawezi kufanya kazi zake za kipolisi

kama Mkuu wa Polisi wa Wilaya kutokana na mazingira magumu na duni.

Mheshimiwa Spika, niliiambia Serikali, kumbukeni kwamba Wilaya ya Maswa ambayo ni Wilaya kongwe haina Kituo cha Polisi, Askari wanapata matatizo makubwa sana wakati wa kutekeleza majukumu yao. Hivyo, kwa kuwa inajiita Serikali sikivu, nikaamini kwenye bajeti hii suala la Maswa sasa litakuwa limepata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kitu cha ajabu, nimeangalia kwenye bajeti, hakuna kabisa sauti iliyosikika. Sasa katika hili Serikali hii inaweza kusema kwamba imeweza, imethubutu, imesonga mbele? Imesonga mbele kuelekea wapi, wakati vikorombwezo vyake imeviacha katika mazingira duni ya kiutendaji? Hii maana yake nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii inatuonesha kwamba Serikali hii ina ubingwa wa kutengeneza maneno matamu ambayo pengine yanawatamanisha wananchi na wanafikiria kwamba ni muda mfupi tu wanaweza wakayafikia hayo maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, naomba, kwa kuwa Serikali inajiita sikivu na wakati huo huo ikashindwa kusikia mchango wangu huu, itambue kwamba Wilaya ya Maswa hawajawajengewa Kituo cha Polisi. Sasa hivi hata vile vibanda vibovu ambavyo wanatumia Polisi sasa hivi, kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Mwigumbi - Bariadi inayoelekea Lamadi, vimeshawekewa ‘X’, vitabomolewa kupisha ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninakuwa na mashaka na masikitiko makubwa endapo Mheshimiwa Magufuli kwa namna ninavyomjua, huwa haangalii kwamba hapa pana nani aliyejenga nyumba hiyo, basi ataamua kubomoa. Itakuwaje siku hiyo? Atakapoamua, maana ni lazima abomoe vibanda hivyo kwa sababu ni mpango umepitishwa, na yeye anasema haangalii cha CCM, haangalii CHADEMA, kama kuna jengo ambalo lipo kwenye eneo hilo, kazi yake ni kutimiza majukumu yake. Ninamuunga mkono kwa sababu ndiyo wajibu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hamjaweka mpango huo, mnategemea watu wa Maswa wataishije? Mbona mnawapa wasiwasi? Kwa nini hamjaamua kuweka kwenye mpango huu mkawajengea Kituo cha kisasa Polisi wa Maswa na wao wakajiona kweli wanahitajika katika jamii hii? Kuna sababu gani ya msingi? Mnataka mpaka muambiwe na nani ndiyo mjue kwamba Polisi wa Maswa wanateseka? Polisi hawana nyumba, Polisi wanaishi kwenye vibanda vya zamani sana vilivyokuwa vinatumiwa na Watemi, kipindi kile inaitwa *Sukuma Land,* Chapa Ng'ombe. Wanaishi mazingira magumu, huwezi hata kunyoosha miguu yako.

Mheshimiwa Spika, siku hiyo nilieleza nikaiambia hii Serikali kwamba kulitokea maafa, akafa Askari mmoja, wakashindwa hata namna ya kumfanyia usafishaji wa Kiislam. Nyumba ni ndogo! Nyumba hizo hazifai hata kuitwa nyumba. Nikaiambia hii Serikali nikaamini kwamba sasa kwa sababu ni sikivu watachukua hatua ya kwenda kuwatengenezea miundombinu ili Askari

wa Maswa waweze kufanya kazi yao vizuri. Kwanza, nawapongeza Askari wa Maswa, wanajitahidi pamoja na mazingira magumu. Niliiambia hii Serikali kwamba Polisi wa Maswa wanafanya kazi yao katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia gari walilonalo gari hivi sasa tairi ni vipara. Huwa nawauliza hata hawa *traffic* wanapowakamata raia wa kawaida wenye magari yenye tairi vipara, kwa nini usianzie wewe *traffic* kukamata gari lenu la Polisi? Kwa nini unakwenda kukamata magari ya raia wa kawaida? Maana raia naye anajifunza kupitia baba yake! Wanasema mtoto akiwekwa mgongoni huangalia kisogo cha mama yake. Sasa inakuaje ninyi mkasi huu unakula upande mmoja tu? Ni msumeno gani huu? Lakini hawana jibu maskini, kwa sababu hali hii hawaisababishi wao, ila Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikazungumza pia kwamba huu utaratibu wa Polisi kulazamisha kufuata mafuta Makao Makuu ya Mkoa ungerekebishwa. Polisi wa Wilaya angeweza kupewa, naye *OC* akapata mafuta yake mwenyewe badala ya kuyafuata. Hivi sasa hulazimika kuyafuata mafuta Shinyanga, anatumia lita 50 kufuata mafuta ambayo amepangiwa lita 200, anarudi na mafuta lita 150. Angalia Maswa ilivyo! Askari huyu anaanza kupata shida sana katika kutimiza majukumu yake. Matokeo yake, Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, kwa ajili ya kutambua umuhimu wa Askari hawa, ndiyo huwa inawasaidia kila wanapoishiwa mafuta. Tatizo linakuja kwenye gari, wakati mwingine Halmashauri gari zake zinafanya kazi, nyingine gari la

Polisi hata kama litapewa mafuta, halina matairi. Lakini ukiangalia Makao Makuu ya Polisi, ambako wakubwa wapo, magari yapo, mengine wanayatumia kwa kuwapa wake zao kuwapeleka kwenda kununua mboga au kupelekwa *salon* badala ya kuyapeleka Maswa na Wilaya nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mimi ni Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tatizo lingine kubwa, nimeliona kwenye Gereza la Igunga. Kama kuna watumishi wa Magereza wanaopata taabu ni watumishi wanaofanya kazi kwenye Gereza la Igunga. Gereza lile limejengwa kwa *full suit* za mabati, tena fupi. Nilivyosimama nisingeweza kusimama. Kwa hiyo, Mkuu wa Gereza la Igunga anapata taabu sana. Niliingia mle wakati tunaongea, yaani unaingia kwa kuinama, mpaka unakaa huwezi ukasimama. Joto hilo, mtu huyu pamoja na majukumu yao, wanaambiwa wavae magwanda ya kipolisi, analazimika kutoa shati mkiwa ofisini, joto kali! Magereza hawa hawawezi kulalamika kwa sababu maadili ya kazi hawaruhusiwi kuilalamikia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa natumia nafasi hii, kama mwakilishi wa wananchi, Polisi na Magereza na wengine wakiwa miongoni mwa wale ninaowawakilisha niiambie hii Serikali, leo mtambue kwamba mnawatesa Watumishi wa Gereza la Igunga kwa kuwajengea mazingira magumu kwa kuwafanya watu hawa waione hiyo kazi ni kama na wao ni wafungwa. Hiyo ni kazi kama zilivyo kazi nyingine, tunapaswa tuwaonyeshe kwamba wanatimiza majukumu yao kwa kazi ambayo ni kweli ipo kwa ajili

ya kuwalinda na kutekeleza na kuifanya Serikali ionekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kumalizia, huu mchezo wa kuwachezea Polisi Jamii; Polisi Jamii waliwekwa Wilaya ya Maswa wanajitahidi sana kutimiza majukumu yao kama ajira yao inavyowaelekeza. Tatizo lililopo, hamjawatendea mafungu ya kuwawezesha hawa Polisi Jamii kufika kwenye vituo walivyopangiwa, halafu baadaye warudi tena kwenye Kituo chao cha sasa. Kwa hiyo, watu hawa pamoja na mishahara midogo, hulazimika kutumia hela zao. Wanawanyima hela watoto wao kwenda shule, kwa sababu anaambiwa akatengeneze taarifa ya kila wiki. Huyu mtu pengine atalazimika kukaa chini ya mchongoma anaandika ripoti ambayo hailingani na hali halisi, kwa sababu hana nauli. Waingizieni *allowance* sasa waweze kufanya kazi zao vizuri. Haiwezekani ukaanza kukata mshahara wako kwa ajili ya kwenda Ipililo kwenda kuchukua taarifa za Kata hiyo ili uweze kurudisha na baadaye umpelekee Mkuu anayehusika. Utakachofanya ni kujikunja na kuandika habari ya kupika. Sasa ili tuepuka hilo, naomba sana tuwajali hawa Askari.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hotuba yako ni *very original,* mpaka inapendeza kusikiliza!

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyo mbele yetu. Kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema siku ya leo ambayo ni siku muhimu ya kujadili Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ambayo ni muhimu kwa usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nataka nianze kwa kusema kwamba leo wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu, awali, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria alijibu swali hapa na katika majibu yake alisema kwamba alitembelea Gereza la Isanga na kukuta watoto sita ambao mama zao ni wafungwa wako Magerezani. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, naomba wakati wa majibu, nimepata shaka kwamba kwa mujibu wa Sheria na Haki za Binadamu wafungwa wa kike hulindwa na Askari wanawake. Sasa wasiwasi ni vipi; aidha, kama itakuwa hawa walifungwa wajawazito, walizaa pale, sina shaka. Lakini kama waliingia mle wakiwa sio wajawazito, ni teknolojia gani iliyotumika mpaka hawa wakapata ujauzito ndani ya Magereza yetu? Naomba hili nipatiwe jibu, maana limeshangaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu. Pia hata hayo Magereza upande wa wanaume kuna jambo ambalo linazungumzwa sana, naomba nalo tupate ufafanuzi wake au tuambiwe, kwa sababu kuna malalamiko sana ya tuhuma za ulawiti katika Magereza yetu. Hili ni jambo ambalo lipo, siyo la kubisha. Sasa tunataka kujua hata kama ni wafungwa kwa wafungwa, lakini wana wasimamizi ambao wanatakiwa moja ya kazi

zao ni kuhakikisha matendo machafu yote hayapatikani katika Magereza yetu. Kwa hiyo, hili nalo pia tunataka tujue. La, kama ni hawa walinzi wa wafungwa nao wanajihusisha na mambo haya, nayo pia Mheshimiwa Waziri naomba tujue na hatua zinazochukuliwa ili kurekebisha tabia hii chafu kabisa na kudhibti maradhi ya Ukimwi ambayo ni tishio kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nielekee kwenye suala la Vituo vya Polisi. Mimi natoka Kaskazini Pemba, Jimbo la Konde ambalo ni karibu na Kusini mwa nchi yetu. Tumepakana sana na Kenya. Kule ni ukanda ambao una Mahoteli ya Kitalii yasiyopungua 50 na hali inaendelea. Katika Kisiwa cha Pemba ni eneo pekee linalobeba Sekta ya Utalii asilimia 90 na zaidi. Lakini hali iliyoko kule na mazingira yanavyoonekana, siku Al-Shabab wakiamua kuja pale, hakuna kinga, wataingia watakavyo, hakuna hatua zozote za kiusalama zinazoonekana kuchukuliwa kule. Eneo ambalo wanaingia watalii na ni eneo ambalo linategemea Kituo kimoja cha Polisi kilichoko Konde, kituo ambacho ni mbali na mazingira ya sehemu yenyewe ninayoitaja hapa.

Kwa kweli naiomba Wizara iangalie umuhimu wa kudumisha hali ya usalama katika maeneo yale, tuko karibu sana na Shimoni Kenya ambao ni jirani sana na Somalia. Matendo yanayofanyika maeneo kama yale, ni maeneo ya kuangalia kwa umakini kabisa. Ni bora kinga kuliko tiba. Hili jambo naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie. Pia ukanda ule wa mahoteli, kuna uwezekano wa wahamiaji au watalii wanaotoka

sehemu za Kenya kuingia katika hali wanayopenda wao kwa sababu hakuna hata Afisa wa *Migration* katika eneo hili. Ni eneo kubwa sana na pana la utalii. Kwa hiyo, naomba hili suala nalo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa sitaki kusema niliambiwa uongo, lakini nadhani nilidanganywa. Kuna siku ya mwanzo tu niliyosimama katika Bunge hili katika ya mambo ambayo ni shida katika Jimbo langu, la mwanzo nililoongea hapa ni suala la Kituo cha Polisi cha Konde. Hiki Kituo kilijengwa enzi za Ukoloni na sidhani kama kuna mwaka ambao kiliwahi kufanyiwa ukarabati mpaka leo. Hali ya pale ni mbaya na nilimwomba Mheshimia Waziri wakati huo afanye ziara ya kuja Konde kuangalia hali wanayoishi Askari wale, kwa kweli nilipewa jibu zuri kwamba Waziri atakuja Konde, na nilikwenda kule nikawaahidi Askari wa Konde kwamba Waziri wenu atakuja Konde na hilo halikufanyika.

Sasa leo najua, kwa sababu ya Waziri huyu makini ambaye yupo sasa, hata yule ni makini lakini kidogo alipitiwa, naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwanza Naibu Waziri, sio mgeni sana wa Konde, nakumbuka aliwahi kuja kuposa japo alikataliwa, naomba akumbuke kuja tena kwa kufikiria. Mheshimiwa Waziri tafadhali Wabunge wa Kaskazini Pemba tumeandaa ziara, nakuomba Mheshimiwa Waziri mtuunge mkono kuja pamoja nasi kuangalia haya tunayolalamika. Leo Askari wa Konde watajua kama kweli Mbunge wao anafanya kazi ya kuwatetea.

Kuna siku Mbunge mwenzangu wa Jimbo lingine hapa alinyanyuka akatetea Kituo hiki kiasi ambacho nilijua na yeye alipita akakamatwa na Askari wa pale wakamwambia angalia hali yetu, kuna hatari ya kuja kuzika hapa kwa bunduki, maana Askari akifa huzikwa na bunduki zinapigwa juu. Sasa yeye alitetea hili. Nafikiri walidhani Mbunge wao hakulisema hili. Nataka niwaambie Askari wa Konde, nililisema hili na leo Waziri kwa furaha aliyonayo najua amekubali, atakuja Konde. Mheshimiwa Waziri nijibu kwenye majumuisho kama utakuja Konde. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linafanyakazi nzuri sana ambayo kama alivyotangulia mzungumzaji aliyepita, ni Mpinzani mwenzangu, nafurahi kama Mpinzani mwenzangu ameiona kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Polisi wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Ni vizuri sana tukawa waungwana kukubali ukweli. Pale penye uzuri tuseme hili zuri. Hata wananchi wa Tanzania watatuelewa vizuri sana kama kile kizuri tunakisifu na kibaya tunakikosoa. Upinzani siyo upinzani wa kupinga kila hata kizuri kinachofanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, mwelekeo wake muda mfupi tu baada ya kuingia katika Jeshi hili tumeona mambo yameimarika zaidi. Namwomba Mheshimiwa Waziri, kama kuna uwezekano wa kunipatia hawa Vijana wa Ulinzi wa Usalama wa Taifa, wakitufuatafuata pia nafurahi zaidi kwa sababu unakuwa na usalama karibu au unapokuwa na Askari karibu, roho yako inakuwa na amani kwamba mimi hapa niko katika maeneo salama. Sasa mimi

nashangaa wengine wanaonana na Askari halafu wanaogopa.

Kwa kweli inashangaza sana hili jambo la kuanza kuwasema vibaya Askari wetu! Siyo mwenendo mzuri hata kidogo! Askari wetu wapo kwa ajili ya kulinda usalama wetu na hakuna historia ya matukio ya Askari wetu kudhuru watu ovyo ovyo. Hili jambo halipo, hata kama inatokea, ni kwa bahati mbaya. Lakini tuwajengee imani Askari wetu, badala ya kuwashutumu na kuwavunja moyo katika kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachosikitisha zaidi ni kwamba wanaotoa shutuma hizo wengine wanategemea kugombea Urais wa nchi hii. Sasa Ikulu hailindwi na filimbi wala mgambo. Ukiwa Rais utalindwa na Askari wa Usalama hao hao. Tusikatae watu wetu, tuache wafanye kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nataka kusema, pamoja na sifa nzuri ya Jeshi la Polisi, kuna tabia ya baadhi ya Askari waliolipaka tope Jeshi hili la Polisi. Katika Wilaya yangu ya Micheweni, mwanzoni mwa mwaka huu lilitokea tukio la raia wawili ambao wanajulikana kwa majina ya Masoud Bawa na Shaabani Khamis waliopatwa na tatizo la kuzuiliwa na Maaskari, na maaskari hawa wakiwa-*hold* katika msitu na kuwaambia mpaka walete rushwa kutokana na kitendo ambacho walihisi ni kosa. Waliwazuia na mmoja wao akapewa ruhusa kutoka aende akatafute hela ya rushwa ambayo ilikuwa hawaitimizi. Bahati nzuri walikuja katika Jimbo langu na kunifuata mimi

mwenyewe na nikatoa fedha zangu kusaidiana na zao waende wakalipe hongo hiyo.

Mheshimiwa Spika, tulifuatilia kwa ajili ya kuwakamata, matokeo yake mtego ulikwenda upande, lakini Askari Polisi wa Micheweni, tulikwenda kumkamata mmoja porini lakini kutokana na hali, inaonekana ni ushirikiano katika lile tukio, Askari yule alipokamatwa porini mmoja hata hakupekuliwa na Askari waliomkamata. Nilichukuliwa ushahidi nikiwa kama Mbunge, kesi ile ilifailiwa pale, huu sasa hivi ni mwezi wa Saba hakuna hatua zilizochukuliwa. Wananchi wale wanalalamika, wamechukuliwa fedha zao, Askari wale wameendelea kufanya kazi, faili liko, malalamiko yapo, mashahidi tupo, mmojawapo nikiwa ni mimi, na hakuna hatua zilizochukuliwa mpaka leo. Hii ni kulipaka matope Jeshi la Polisi.

Naomba Mheshimiwa Waziri, jambo hili mlifuatilie, tatizo kubwa ni kuacha Askari mmoja kufanya kazi katika kituo zaidi ya miaka 10, yanajengeka mazoea na kinachofanyika pale inaonekana ni kitu cha kawaida. Naomba Mheshimiwa Waziri unipe jibu la suala hili na ulifuatilie na hatua zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 wakati nikichangia hotuba ya Wizara hii niliiomba Serikali na Wizara hii kuwapunguzia masharti na ugumu wananchi wa Wilaya ya Micheweni, lakini hasa Jimboni kwangu Micheweni kuweza kupata hati za kusafiria kwa sababu ni wadau wakubwa katika Wizara hii, lakini

pia wanachangia kiasi kikubwa cha fedha katika Idara ya Uhamiaji. Vile vile wanaingiza kiasi kikubwa kila inapofika kuanzia mwezi wa Tisa hadi mwezi wa Tatu.

Mheshimiwa Spika, niliwaombea wananchi wangu kwa sababu Serikali kila siku inasema yenyewe ni sikivu, lakini cha ajabu baada ya kupunguziwa masharti na ugumu, imekuwa ni adhabu, kwani ndani ya Wilaya ya Micheweni, ipo Ofisi ya Uhamiaji ambayo ina uwezo wa kutoa huduma kama hiyo, lakini wananchi wa Wilaya ya Micheweni wanalazimika kwenda Wilaya nyingine kufuata huduma hiyo. Jambo ambalo mimi siliungi mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, aniambie ni kwa nini wananchi wa Wilaya ya Micheweni wafuate huduma kama hiyo Wilaya nyingine wakati kwenye Wilaya yao ya Micheweni Ofisi kama hiyo ipo?

Mheshimiwa Spika, wakati Watanzania wazalendo wakiendelea kuwekewa masharti na ugumu hasa pale wanapoomba hati za kusafiria, wapo viongozi ambao wameaminiwa na Serikali hii, lakini hawaonyeshi uaminifu katika kazi zao. Pale Makao Makuu ya Uhamiaji Dar es Salaam, kuna Kamashina wa Utawala na Fedha ambaye anaitwa Paniel Mgonja. Ofisa huyu alimtaka Ofisa mmoja *in charge* kuwapatia Wanyarwanda wawili *passport* za Tanzania jambo ambalo ni kosa kisheria. Wageni aliowataka Paniel Mgonja wapatiwe *passport* za Kitanzania ni hawa hapa ninao majina yao katika hii taarifa. Kwa sababu muda hautaniruhusu kuichambua taarifa hii,

nitakuomba uchukue taarifa hii, uangalie jinsi Kamishna huyu wa Utawala na Fedha Makao Makuu, jinsi anavyowadhalilisha na kuwakejeli Maofisa wa chini na kuifanya Idara hiyo ya Uhamiaji ni miliki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi ninapozungumza, Ofisa huyu mwenye *Masters,* Ndugu Paniel Mgonja, baada ya kukosa kuwapatia Wanyarwanda hawa wawili *passport*, alimwambia nitakuonyesha na nitakupeleka Mtambaswala kwa sababu huna faida na Idara hii.

Mheshimiwa Spika, sasa nazungumzia kuhusu Askari Polisi. Baadhi ya Askari Polisi wamekuwa wakifanya uhalifu, lakini kinachoonekana hapa, Askari wanalindana, kwa sababu mwananchi wa kawaida anapokwenda kulalamika Polisi, basi huonekana kulindana huko kwa Askari hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu kule Jimboni kwangu Micheweni yupo Askari mwenye namba E3543 kwa jina anaitwa Koplo Ali Faki. Kabla sijazungumzia hili, naomba ni-*declare interest*, Askari huyu alimshawishi mtoto wa mkubwa wangu na akalala naye usiku mzima. Askari huyu baada ya kulala naye msichana huyu usiku mzima, wakati wa alfajiri alimtelekeza msichana huyu na akamwambia nenda zako. Baada ya kwenda zake msichana huyu kwa sababu nyumba aliyompeleka ni ya ghorofa, msichana huyu alikosea *step* akaanguka na kuvunjika mguu. Baadaye asubuhi akapata msamaria mwema akamchukua akampeleka kwa wazazi wake. Baada ya hapo mzazi wake akaenda kulalamika Polisi na baadaye akapelekwa Hospitali na Dakitari

akathibitisha kwamba msichana kafanyiwa kitendo kibaya.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kupata taarifa hiyo, nilipiga simu Kituo cha Polisi kumwuliza *OCD* kuhusu jambo hili, akaniambia linashughulikiwa. Baada ya kuniambia tatizo linashughulikiwa, nikakaa kimya, nikamaliza muda wa mwezi mmoja, nikaona sijapata jibu lolote; ukamalizika mwezi wa pili, wa tatu, wa nne hadi leo wa tano hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kwa Askari huyo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa, aniambie ni utaratibu gani wa Askari Polisi anapofanya uhalifu, ni hatua gani zinachukuliwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, mwaka 2011 vile vile katika kuchangia kwenye hotuba ya Wizara hii, nilisema kwamba Kituo cha Polisi Wilaya ya Micheweni kilifunguliwa mwaka 1979 hadi sasa ni miaka 33, lakini bado Askari hawa wanaendelea kuteseka kwa sababu hawana makazi na hadi sasa hakuna chochote kinachoendelea. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aniambie, ni lini Askari hawa wataweza kujengewa makazi ili na wao waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi zaidi?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja ya bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, jana nilichangia hoja yangu kwa maandishi nikifikiri siwezi kupata nafasi, lakini sasa nakushukuru sana kwa kuipata.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu, Mheshimiwa Waziri atakumbuka nilisisitiza mambo sita ambayo kimsingi Wabunge wenzangu wote wameyatilia mkazo sana, nami naomba sana Mheshimiwa Waziri ayatilie mkazo. Kwa kweli Askari wetu wana maisha magumu, naomba wapate posho zao kwa wakati, *disturbance allowance*s nazo walipwe, mafao yao ya uhamisho pia walipwe na majengo yao yaweze kuangaliwa upya, kwa sababu hata hizo *quarter* ambazo zilijengwa zamani sana, haziendani na maisha ya kisasa. Kuna haja ya kuyaangalia upya.

Mheshimiwa Spika, mimi sina matatizo na Mheshimiwa Waziri kwa sababu katika Wizara hii bado ni mgeni, lakini malalamiko haya yamekuwepo miaka mingi. Nafikiri sasa ifike wakati Mheshimiwa Waziri naye afuate nyayo za Mheshimiwa Mwakyembe kwa sababu kuiga jambo zuri ni kitu kizuri. Afuatilie kuhakikisha kwamba anayatambua mwenyewe matatizo wanayoyapata Askari wetu katika nchi yetu. Askari wetu hawana uwezo wa kulalamika. Katika Sheria na Kanuni za kiaskari, hawana neno ‘hapana’, wao lugha yao ni maneno matano tu; *yes, ok,* ndiyo,

sawa, yah! Hakuna kitu tofauti na hapo. Ni hayo; *ok, yes*, ndiyo, sawa. Atakayesema kinyume na hapo ataonekana ni mtovu wa nidhamu. Kwa hiyo, ili waweze kutendewa haki Askari hawa, wanatutegemea sisi ambao ni wawakilishi wao ambao ndio tutaweza kuwatetea na kuwasemea yale ambayo yanawakabili.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Iringa maaskari wanapata shida sana, kwani makazi yao ni duni mno. Nashukuru kuna jengo la Magareza linajengwa pale la ghorofa, lakini sijui kwa Askari hawa wa kawaida sijui imefikia wapi mpaka sasa, kuna mpango gani ambao Serikali imefikiri itaweza kuwasaidia Askari kupata makazi yaliyo bora?

Mheshimiwa Spika, pia nachukua nafasi hii kuwapongeza Askari wote wa Tanzania kwa ujumla, kuanzia kwa *IGP*, Ma-*RPC* mpaka Askari wote wa chini, na hasa nimpongeze Kamanda wetu wa Mkoa wa Iringa ambaye ametokea Mkoa wa Ruvuma. Nampongeza Kamanda huyu kwa jinsi nilivyoona alivyosimamia haki katika Mkoa wa Ruvuma wakati nikiwa katika uchaguzi wa Kata ya Lizaboni. Mheshimiwa huyu kama sio yeye, kwa kweli damu ingemwagika Songea, maafa makubwa yangetokea pale ambapo kulitokea hali ya kutaka kuchakachua matokeo. Lakini mimi nilimfuata Kamanda, nikamweleza, nilisema katika kampeni zangu zote kwamba nitahakikisha haki inatendeka, kama nitashindwa nitaondoka kimya kimya. Lakini nikishinda, sitakubali, lolote lile itabidi liwe na Kamanda akasema, ukifanya hivyo itakuwa vizuri; lakini kama mtasababisha

fujo, wakati mmeshindwa, hapo sasa mtaona cha moto! Ushindi ulipatikana, nilitembea vituo vyote mwenyewe kujumlisha kura, vyote mpaka saa kumi na mbili kasorobo nimeshapata matokeo yote ya kura za ushindi pale, na nilishinda.

Mheshimiwa Spika, lakini mizengwe iliyokuwa inawekwa kwenye Kituo cha Kuhesabu Kura cha Majumuisho, matokeo yake yakaja kutajwa saa 2.00 za usiku, giza limeingia, baada ya kwamba sasa tunataka kuleta vurugu, kwamba tunataka kuchakachuliwa hatukubali! Kamanda aliingia Kituo cha Kuhesabu Kura na akasema jamani, nataka haki itendeke, msiniletee shida katika Mkoa wa Ruvuma, sitaki lawama za kumwaga damu ya Watanzania. Kwa hili, naomba nimpongeze kwa dhati kabisa Kamanda wangu wa Mkoa wa Iringa, na nimefurahi amekuja Iringa, nina imani kwamba kwa msimamo wake huu wa kutenda haki, haki itatendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amani ni chombo cha kujivunia. Hakuna Mtanzania ambaye anataka awe katika vita, awe katika shida katika nchi yake. Nawapongeza sana Waasisi wa nchi hii ambao waliweza kuitengeneza amani mpaka sasa leo imekuwa ni kitu cha kujivunia katika Taifa letu. Lakini naamini amani hii imetengenezwa, kwa sababu haki ilikuwa inatendeka na haki popote ikitendeka, amani inakuwepo *automatically*. Lakini ukiona mahali popote kuna malalamiko, kudhibitiana, amani inatoweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema haya kwa sababu zifuatazo: Mimi nilifanya ziara katika Mkoa wa Iringa wakati Bunge la mwezi wa Nne limeahirishwa. Tulihamasishwa Wabunge twende tukafanye ziara, tuhakikishe tunawasaidia kufanyika zoezi la sensa katika nchi yetu. Niliamua kujituma kwa makusudi kabisa nikijua umuhimu wa sense, na nikaanda ziara katika Mkoa wa Iringa, nikaanza na Jimbo la Isimani. Nimekwenda Ngweleli, Kinyali, Migoli kufanya Mikutano, lakini kwa makusudi kabisa, Serikali iliamua kuingilia kati kwa kuweka mizengwe katika Mikutano ambayo imeandaliwa kwa dhamira nzuri kabisa. Lakini nilipata vikwazo vingi sana kufanya kazi ile mpaka kuimaliza. Lakini niliifanya kwa sababu mimi huwa sikubali kushindwa pale ninapoamini nafanya kitu cha haki ambacho hakina tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema hayo kwa makusudi kwa sababu, amani ya nchi hii itaanza kuharibikia hapo, na ndipo tutakapopata shida kuingiza Taifa letu katika vita. Tabia ya Serikali hii, narudia hata katika mchango wangu wa mwaka jana 2011 nilisema, nashukuru nilipata bahati ya kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Ndani, nilisema kwamba tabia ya Serikali kutumia vyombo vya dola makusudi kudhibiti Vyama vya Siasa au Viongozi wa Kisiasa wasifanye kazi zao, kutakuja kuleta maafa makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Siasa vinaendesha kazi zao kwa mujibu wa Katiba. Katiba yetu ya nchi hii imeruhusu Mfumo wa Vyama Vingi, imeturuhusu sisi viongozi wa Vyama vya Siasa kufanya kazi zetu za kisiasa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya uraia kwa

wananchi ili waweze kujua wajibu wa Serikali yao na wajibu wao kwa ujumla wao, kwa Serikali yao pia. Lakini tunafanya kazi hii katika mazingira magumu sana. Kinachojitokeza zaidi ni propaganda za kisiasa kuhakikisha mvurugiko wa amani unatokea ili wanasiasa tushindwe kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Demokrasia na Maendeleo kimekubalika nchi nzima. Kina wanachama wengi na wanaikubali kazi inayofanywa na Chama hicho, ndiyo maana tunakubalika kila tunapofanya Mikutano yetu. *(Makofi)*

Mara kadhaa tumekuwa tukizuiwa hata kama tunafanya kazi halali kabisa, kama nilivyotoa mfano wa kuelimisha jamii ili washiriki vizuri katika sensa, tunaelimisha jamii pia tunawaambia hata namna ya wajibu wao kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii kujenga maisha yao; tunafanya kazi hii kuelimisha Umma wa Watanzania ili waweze kuchanganua mema na maovu, ili waweze kujua haki zao za kimsingi ili wao waishi. Lakini tabia ya Serikali kutudhibiti Chama cha Demokrasia na Maendeleo tusifanye kazi, mtaleta shida katika Taifa, na hii siyo chama kimoja tu, Vyama vyote nchini vina haki ya kufanya kazi zao za kisiasa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iwe makini sana kuhakikisha haki inatendeka. Askari wetu pamoja na shida zote ambazo wanazipata, lakini bado wanafanya kazi yao kwa taabu sana kwa sababu wakitenda haki pia wanadhibitiwa. Nina malalamiko ya Askari wengi tu ambao wamehamishwa, wamepelekwa maeneo ya hovyo kwa sababu tu wao

wameweza kutetea labda wakafanya kazi yao kwa haki, Chama cha Upinzani kikashika nafasi fulani kwenye ushindi wa chaguzi. Hii hatuwatendei haki Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amani hii tunayotaka kuichezea sasa kwa ajili ya tamaa ya madaraka, tamaa ya kuogopa kuachia nchi wakashika Chama kingine wakatawala, ni kitendo kibaya ambacho Bunge hili tunatakiwa kwa pamoja tukikemee kuhakikisha tunailinda na kuitetea amani ambayo imeshajengwa na waasisi wa Taifa letu. Heshima tunapata Watanzania hata tunapotoka nje ya Tanzania kwa amani iliyopo ambayo iligharamiwa, Wazee hawa Waasisi walivumilia mambo mengi tu wakaacha haki itendeke hata kama kwa maumivu, lakini walihakikisha kwamba wanapigania haki kwa masilahi yetu sisi ambao sasa tunafanya siasa katika nchi yenye amani ambayo imetengenezwa kwa gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona nizungumze hili kwa mkazo sana. Propaganda za kisiasa ni kitu kibaya sana, ni sawasawa na shetani unamkaribisha ndani ya nyumba. Sasa hivi viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo wanafanya kazi katika mazingira magumu, wanatishiwa kuuawa na wamesema wazi...

**SPIKA**: Hayo maneno ondoa kwa sababu utatakiwa kufanya vitu visipokuwepo. Maneno mengine umesema vizuri, sasa hayo mengine ya nini? Maneno uliyoyasema nyuma tumeelewa, lakini haya mengine nakuomba uachane nayo.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Spika, sawa, ilikuwa katika kutilia mkazo. Mimi sitaki kubishana na kiti chako, na siku zote huwa napenda kuwa na heshima. Mimi ni mama, natakiwa kuonyesha mfano wa nidhamu. Lakini kikubwa ninachokisema, tutende haki, Serikali iliyopo madarakani ijue lazima iko siku wataondoka, lazima! Hiyo haina ubishi! Hauwezi kutawala miaka yote katika maisha yote dunia hii mpaka iishe kiama, haiwezekani! Lazima tukubali kuingiza fikra kwamba iko siku tunaweza kuondoka, lakini ili tusiondoke, tutende haki, tutekeleze yale ambayo yanalalamikiwa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukitenda haki, mkitekeleza mambo yanayolalamikiwa na wananchi mtaondolewa kwa nini? Wananchi si wataendelea kuwakubali! Lakini sasa mnafikia hatua kwamba haki haitendeki! Kwa sababu haki haitendeki kwa kiwango kinachostahili, mnadhibiti hata ile hali ya wale watu wachache ambao wanajitokeza kuelimisha Umma ili utendewe haki, hiyo siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina ugomvi sana na Chama cha Mapinduzi, mimi sijawahi kushitakiwa, sijawahi kufungwa, sijawahi kupata tatizo lolote kusema labda nina chuki ya kusema kwamba Serikali hii labda ilinifanyia kitu kibaya, lakini ninachosemea ni ile hali halisi ya kujenga Taifa letu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

## TAARIFA

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpe taarifa kidogo Msemaji aliyemaliza punde hivi kwamba hapa tuko Bungeni, huu siyo Mkutano wa Hadhara. Lakini pili, nilitaka nimkumbushe pia kwamba uchaguzi uliopita Chama kilichoshinda ndiyo kilichochaguliwa na wananchi na ndicho Chama kilichokubalika na wananchi wakakipa ridhaa. Lakini kusema kwamba Chama chake hicho sasa hivi kinakubalika na wananchi, uchaguzi bado. Uchaguzi uliopita walishindwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Msabaha atafuatiwa na Mheshimiwa Natse. Samahani kidogo kuna watu wamesema hapa walionekana kwenye orodha. Jana naona watu wangu walifanya makosa, orodha tuliyotumia ni hii na hiyo ndiyo tuliifanyia mpango wa hesabu za namna ya kufanya kazi siku ya leo. Kwa hiyo, wale wote walioomba nje ya orodha iliyokuwepo jana, majina yao hayakuja hapa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Msabaha tafadhali.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipatia nafasi hii nichangie Wizara ambayo ni nyeti kwa Taifa letu. Kabla ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniamsha salama na kunipa afya hii.

Nachukua fursa hii kuwatakia Mfungo Mtukufu wa Ramadhani Masheikh wote wa Zanzibar na Pemba na Wanazuoni wote wa Zanzibar na Pemba na Tanzania Bara na wazidi kuombea Taifa letu kwa sababu Taifa letu linapokwenda ni kubaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu viongozi wengi sasa hivi wamekuwa wanasahau maadili ya uongozi. Kwa hiyo, naomba Masheikh wote pahali popote mnakonisikia, muwaombee viongozi wetu na Mheshimiwa Rais wetu amalize awamu hii kwa salama na amani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Msabaha pamoja na wewe, maana yake ni kiongozi. *(Kicheko)*

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, na mimi mwenyewe. Baada ya kusema hayo, nirudi katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara nyeti na Wizara hii inabeba mambo nyeti. Lakini ukitizama humu humu kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ndiko huku huku kunatoka usalama wa Taifa. Lakini nasema, maadili ya Mapolisi, maadili ya Viongozi wa Usalama wa Taifa sasa hivi yanakwenda vibaya.

Nasema hivi kwa sababu gani? Ni kwa nini nyaraka za Serikali zinakuwa zinatoka pasipokuwa na idhini maalum? Unamkuta mtu yeyote nyaraka za Serikali anazipata. Hii inapelekea hata kufanya hata wale ambao wasioitakia mema Tanzania kupata

nyaraka za Tanzania na kujua udhaifu wa viongozi wetu. Nasema hivi kwa makusudi kabisa.

Mheshimiwa Spika, nirudi katika suala la Mapolisi. Kuna watu ambao niseme Askari wetu sio waadilifu katika fani hii ya Uaskari. Wengine wamekuwa wakivaa sare za Polisi na sare hizi wamekuwa sasa wanajisahau hata wanapoingia kwenye sehemu za kunywa vinywaji. Unakuta mtu anakwenda sehemu ya starehe, yeye ni Askari, amekwenda na sare yake ya Polisi pale, huku kabeba silaha. Askari huyu anakunywa pombe pale, anajisahau na pale anahatarisha maisha. Hawa wanachafua Jeshi la Polisi. Nasema hivi kwa sababu, Maafisa Polisi wako hapa na ni Maafisa wakubwa wako hapa, hawa vijana wetu ambao wanadhalilisha Jeshi hili la Polisi, wachukuliwe hatua za kinidhamu, waheshimu Sheria na Taratibu za Askari Polisi.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa nini? Kuna wengine hata wanakwenda kufanya matukio kwa kutumia sare za Polisi. Wanashirikiana mitaani na hili, ndio maana sisi Wabunge tunasema, Maaskari wote wajengewe nyumba Kambini, wasiishi uraiani kwa sababu, huko uraiani ndiko kunakotoka vyanzo vya maovu kwa askari wetu.

Mheshimiwa Spika, nasema kwa sababu, nina ushahidi. Kuna Askari ambaye, alijiingiza kwenye vitendo vya wizi. Tena vitendo vyenyewe ukikuta, ni kwenda kuiba bati; bati kweli, Askari unakwenda kudhalilisha Maaskari wenzako kwa kuiba bati? Hii sio nidhamu ya Askari. Askari yeyote ambaye amepita

Chuo cha Mafunzo na ukapata joto ya jiwe katika chuo hiki, mimi mwenyewe naweza kusema nilipita Jeshi, lakini kupita Jeshi kutokana na maradhi yangu sikuendelea. Lakini machungu yale ambayo niliyaonja mle, mpaka leo ninayo. Ni kwa nini, Askari ambaye, anakwenda *CCP* Moshi kusoma, anapata uadilifu wa Askari, anakiuka Sheria na Kanuni ya Uaskari na kuwadhalilisha Maaskari wenzake?

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye suala la *Traffic* barabarani. Kuna ma-*Traffic* ambao wanachafua sifa ya u-*Traffic.* Nirudi hasa kwa akinamama ma-*Traffic* barabarani. Nasema ile njia ya u-*Traffic* barabarani ya kusimamisha magari, sio njia ya kupata pesa za kwenda kununua vipodozi mle. Nasema hivi kwa nini? Kwa sababu, wanasema wana vipimia mwendo, tochi zile, zile tochi jamani nyie kama mnatoka Dar-es-Salaam mpaka Dodoma, unasimamishwa na Maaskari wangapi? Unakuta abiria wangapi ambao wamesimamishwa mle barabarani?

Mheshimiwa Spika, anakwambia kabisa, namwambia Mheshimiwa Pereira ni kaka yangu, na Mheshimiwa Pereira, asije akataka kuja kuchafuliwa kwenye Wizara hii, ashughulikie matatizo haya. Wazanzibari, sisi ni wakarimu, msituone ukimya wetu humu ndani, sisi tuna busara na hekima zetu. Hatutaki sisi mambo ya Miongozo na sisi hii Miongozo pia, tunajua kuisoma. Lakini sasa nasema, msiwaone hawa Mawaziri ambao wanatoka Zanzibar na hawa Wabunge wanaotoka Zanzibar, mkawaona kwa ukimya wao, kila mtu aliyekuja hapa katoka kwenye fani yake ndio akaletwa hapa. Namwona hata bosi

wangu Sada, nae kaletwa hapa; Sada, alikuwa bosi wangu mimi Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa uchungu. Hawa ma-*Traffic* wanawake, wanadhalilisha wanawake wenzao. Kwanza, hawa ndio wanaongoza kwa kuchukua rushwa, ni kwa nini wanawake ma-*Traffic* mnapenda rushwa? Nakemea hili jambo na hili jambo limenikuta na limewakuta wengine na leo nawasemea wote waliokutwa na mambo haya. Haapa kidogo hata sijui niwaseme vipi hawa wanawake kwa sababu, ni wanawake wenzangu; unakuta wewe mwanamke ni *Traffic,* kweli kile cheo ni cha kwako, ni kwa nini usiwe na lugha nzuri kwa Viongozi? Wewe unaweza kumsimamisha mtu kama ni Mbunge, unamwambia kwanza Kiti chenyewe cha kupewa? Hakuna Kiti cha kupewa, kile Kiti kimepigiwa kura, Wabunge wa Viti Maalum, wamepigiwa kura.

Mheshimiwa Spika, sasa hizi kauli za ma-*Traffic* wanawake mimi huwa najiuliza, ni kwa nini, wanaume wanapokusimamisha wanakupa kauli nzuri? Lakini wanawake wakikusimamisha wanakupa kauli za kukukejeli, sijui wanakukejeli, hata sijui niseme vipi *Yarabi l-alamina*. Ni kwa nini msiwe na kauli ambazo na sisi tukikaa humu ndani tuwatetee ma-*Traffic* wanawake? Lakini leo nimesimama kwa ajili ya ma-*Traffic* wanawake, kuweni na kauli nzuri mnaposimamisha Viongozi, hata wakiwa ni Wabunge wa Viti Maalum, muwajibu vizuri, msije mkasema hivi viti ni vya kupewa. Hakuna mtu aliyepewa Ubunge hapa, kila mtu kapigiwa kura. Nimeondoka hapo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naingia katika Magereza. Jamani Magereza, watu wanaopelekwa mle sio wote wana hatia. Au wote wanaopelekwa jela, sio wana hatia. Lakini na hata viongozi wamepelekwa sasa hivi Magerezani, wanaona joto ya jiwe mle. Jamani angalieni sasa hivi, wanaume wengine wanatoka Magerezani, wakirudi wanakuja kujiua ni kwa sababu, gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo mtu anatoka Gerezani, anafika nyumbani kwake, kawaacha mke na watoto, anaamua kujiua. Ukiangalia wanaume wanakaa mle, labda chumba wanalala watu 10; hawa ni wanaume, wamekaa mle hata miaka mitano, miaka sita, miaka saba, mtu yuko Gerezani, mtu yule aliyeacha mke wake na mtoto au na watoto, sasa yule mama anaishi vipi? Yule baba naye anaishi vipi? Ni kwa nini, Sheria hii msibadilishe na wafungwa nao wakapata haki zao? Wapate haki zao kwa sababu, ni binadamu. Wewe binadamu kama unakula unashiba, hiki chakula unachokula kinakwenda wapi? Kinakwenda mwilini na kina kazi yake. Kwa hiyo, hawa wafungwa muwafanyie taratibu, wanandoa wapate haki zao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, na tuangalie, hata kwenye Magereza sasa hivi kuna biashara haramu zinazofanyika. Wewe unaona mtu kama kapelekwa Gerezani, lakini mfungwa yule yule, anapata bangi mle Gerezani anavuta. Mfungwa yule yule anapata gongo mle Gerezani anakunywa. Tujiulize, hivi vitu vinatokana

na nini? ni kutokana na Maaskari wa Magereza, hali zao ni duni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hata kama una kitu chako unataka kumpenyezea, unamwambia jamani chukua kitu kidogo, nataka nimpe mfungwa wangu angalau naye sigara avute; hili tuliangalie kwa makini. Tuangalie kwa makini, wala msiseme Msabaha, anachekesha Bunge, sichekeshi Bunge, wafungwa wapate haki zao kama nyie mnavyopata haki zenu. Tukifanya hivi tutaepusha gonjwa la UKIMWI. Kwa sababu, ukiangalia Magerezani UKIMWI unaongoza.

Mheshimiwa Spika, sasa wewe kama watu wana, aah, mimi mengine hata sitaji kwa sababu, huu ni mwezi Mtukufu naanza kuupokea na leo niko kwenye swaumu. Sasa nasema hivi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, amekaa pale na Mheshimiwa Spika, Sheria hizi zibadilishwe, hizi ambazo zimepitwa na wakati, ziondoshwe ziletwe Sheria ambazo kila mtu anapata haki yake kama binadamu anavyopata haki yake, wengine wakiwa uraiani na wengine wakiwa Magereza, wapate haki zao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa nimeondoka hapo, naenda kwenye suala la Wahamiaji. Tunashangaa kila siku, kwanza toeni mfano mdogo tu, mimi natoa mfano kwa *TBC*. Pale *TBC* kuna Wachina, wale Wachina leo hii tukienda kuwakagua pale, wote wana vibali vya kuishi hapa Tanzania? Leo hii, tukienda Kariakoo ambazo wanaweza kuzifanya vijana wetu wa Kitanzania, wanazifanya Wachina. Tuseme kwa mfano, Kariakoo, ukifika hata Mchina anauza Karanga.

Huyu kijana wa Tanzania atauza nini *Yarabi*? Huyu kijana wa Kitanzania, atafanya biashara gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TBC* pale wapo wengine, wala sisemi kitu cha uwongo, nilikuwa mle kwa sababu, mwanangu alikuwa na kesi mle, ndio nikaenda. Sasa tuwaangalie hawa wahamiaji haramu, wanapita kwa njia gani? Nasema kwanza wahakikishe katika Wizara hii ya Uhamiaji, wanaajiriwa Vijana wenye taaluma, wenye elimu zao. Sasa hivi Tanzania, tuna vijana wasomi. Tusifanye choyo na husuda katika sehemu za ajira, ndio maana tunapata viongozi wabovu. Tuangalie anayefanya madudu kwenye Wizara ile, ahamishwe moja kwa moja na afukuzwe kazi, apewe mtu mwingine. Leo hii ndio maana tunakuta mpaka Warundi wanatuingilia sijui wa wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala moja nilikuwa nataka nisahau, lishe kwa Maaskari jamani. Hawa Maaskari wanapambana na majambazi wazito. Leo Askari anakwenda kupigana na jambazi, ukimtazama afya yake sio nzuri. Yule jambazi ana silaha nzito, ameshiba, lakini askari huyu hana chochote; akienda yeye na silaha yake, ile silaha kwanza akiishika, mwenyewe anayumba. Kwa hiyo, tuiangalie Wizara hii, watenge fedha za kutosha kwa ajili, ya lishe ya hawa Askari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wala siungi mkono hoja, mpaka nipate ufumbuzi wa wale raia ambao wako Magerezani. *(Makofi)*

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kwa Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwanza, nipende kuwasihi Maaskari wote nchini, pamoja na malalamiko mengi ambayo yametolewa hapa na Wabunge, kuhusu maisha yao, mazingira wanamoishi, posho wanazopata, lakini waone kazi yao ya msingi Kikatiba, kulinda wananchi na mali zao. Huo ni msingi wa kazi yao, waendelee kutenda kazi hiyo kama inavyopasa. Niwapongeze Maaskari wetu, pamoja na hali hiyo kwamba, bado wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema hivi, Askari, yeye anaamriwa na kwa maadili, anabaki kutii. Sasa, tatizo ni kwa yule anayemuamrisha, anayetoa *order;* je, anatenda haki katika kufanya hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na Jeshi la Polisi. Nitaomba Waziri, anapojumuisha, maana nikiangalia Jeshi la Polisi na Mafungu yote katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Uhamiaji na Wizara yenyewe, inatia shaka kuona kwamba, wahamiaji hawa haramu, kwa mfano, Waethiopia kuja mpaka Kongwa, vyombo vyote hivi vya ulinzi vya nchi yetu havina taarifa, mpaka wanafika Kongwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri, akijumuisha, atuambie ni hatua zipi zinachukuliwa na Serikali, katika kuja kwa wahamiaji wote hawa kutoka mpakani mpaka Kongwa. Tunavyo vyombo vingi sana barabarani na ni kwa nini hilo halikutendeka? Hili linatia

mashaka kwa ulinzi wetu. Tunayo majeshi mengi sana, usalama uko mashakani, kama kweli maharamia wanaweza wakaja mpaka katikati ya nchi, ndipo wafahamike.

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo, nirudi katika Jimbo langu la Karatu. Karatu, haina Kituo cha Polisi. Kilichopo ni Ofisi iliyokuwa ya Mkuu wa Wilaya zamani, mabanda madogo madogo; ni lini Serikali itajenga Kituo cha Kisasa cha Polisi pale Karatu? Tukijua kwamba, mji ule una wageni wengi sana, Mji wa kibiashara, wa kitalii, hakuna nyumba za Askari. Hiyo imesemwa mara nyingi, hakuna mafuta pamoja na kwamba, kuna magari, hakuna mafuta. Wahalifu ambao Polisi wanatakiwa wakawafuate, ndio wanawapa mafuta. Sasa kweli, itawezekana? Hayo ni matatizo makubwa kwa Jeshi la Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwa Jeshi la Polisi, tena. Waziri, atusaidie akishirikiana na Wizara pia ya Maliasili na Utalii. Kule Karatu, kama mwananchi atapatikana na tuhuma, hasa katika Hifadhi ya Ngorongoro, Askari wa Wanyamapori huwakamata na kuwatesa na kuwapeleka Loliondo Kituo cha Polisi na si Karatu. Tena, wakipita pale Geti la Ngorongoro, wanatoa *order,* asipite mtu yeyote anayetaka kwenda kuweka mdhamana kwa hawa tuliowachukua; sasa hawa wanatupa mashaka, hii nchi ni moja au ni mbili? Tunacho Kituo cha Polisi pale Karatu. Nitaomba Waziri, hilo aliangalie sana, kutokana na mateso wnaayopata wananchi wa Jimbo lile la Karatu.

Mheshimiwa Spika, niondoke, niende kwenye Jeshi la Magereza. Ni kweli, Askari wanafanana na wafungwa, ni kazi ngumu sana; mvua inanyesha uko huko na wafungwa, jua kali uko huko na wafungwa. Gereza Kuu la Mang'ola pale Karatu, ni Gereza la uzalishaji; nataka Waziri anisikilize, maana Serikali, imeagiza matrekta mengi *SUMA JKT,* yamekaa katika *yard* kwa muda mrefu na tunalo Gereza la uzalishaji pale Mang'ola, halina matrekta, halina vifaa. Sasa najiuliza Serikali hii sikivu, vyombo vyake hivi inachukua hatua gani?

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu wa maandishi pia nimesema hili, kama Jeshi la Magereza, Serikali, itawekeza vya kutosha, ni suluhisho tosha kwa matatizo ya chakula katika nchi hii. kwa hiyo, nitaomba Waziri, uje na majibu ni kwa nini yale matrekta yanakaa kwenye *yard,* yanachakaa pale, hayakupelekwa Mang'ola. Kule pia hakuna nyumba za Askari, ziko nyumba za udongo, majiko ya nyasi, maisha ya Askari Magereza pale Mang'ola ni ya shida mno. Nitaomba Waziri, apange kwenda Mang'ola ajionee hali ile ya Gereza la Mang'ola.

Mheshimiwa Spika, ni kweli, pamoja na matatizo yote, katika Gereza la Mang'ola ambalo ni la uzalishaji Serikali, ilipeleka zaidi ya 300,000,000/= kwa ajili, ya kuchimba bwawa, ili wakati wa kiangazi wapate kumwagilia. Shilingi milioni zaidi ya 300 zimekwisha, bwawa halikukamilika, hakuna maelezo. Kwa hiyo, nitaomba Waziri, aje na maelezo ni kwa nini, bwawa lile hadi sasa halifanyi kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika nchi hii tunayo majanga mengi, kwa mfano, majanga ya moto, maafa, mafuriko, na kuendelea. Tunajenga majengo marefu yanakwenda juu, lakini katika bajeti ya Fungu 14, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, halikutengwa fedha ya maendeleo. Maana yake nafikiri, huku tunakokwenda yakitokea majanga ni jinsi gani Jeshi hili la Zimamoto na Uokoaji litaweza kufanya kazi yake sawasawa kama halina Fungu? Siku zote tatizo likitokea, utaambiwa hakuna gari...

*(Hapa Kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Ni ya kwanza?

**SPIKA:** Ndiyo Mheshimiwa, endelea.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, hakuna gari, hakuna maji, maeneo mengine tunaambiwa kwamba, sasa hilo bomba halifiki kule ghorofa ya 18, 20, 30, kwa hiyo, maji hayawezi kufika. Kwa hiyo, nafikiri kwa sababu, tunajenga majengo marefu katika Miji yetu sasa, ni lazima Kikosi hiki kiimarishwe, maana majanga bado yatakuwepo. Kwa hiyo, naomba Serikali, ifikiri katika bajeti imetengwa fedha kidogo sana, ifikiri na ione ni jinsi gani jeshi hili linaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, yamesemwa mambo mengi kuhusu maisha duni ya Askari wetu, vikosi vyote hivi ambavyo vimetajwa. Ifike mahali kwa kuwa, Askari hawagomi, Serikali, ione haja ya kuwatunza Askari hawa ipasavyo. Kuna tatizo kubwa, tukilifanya kwa

ushabiki na kwa siasa hapa Bungeni, haitatusaidia; tatizo la mauaji, mauaji ya kutisha, ya hovyo, kule Tabora. Acha haya ambayo yana harufu ya kisiasa, ambayo tumesema Bungeni, yaliyoko huko tuyaache; lakini kuna tatizo la msingi la mauaji ya kutisha ya ajabu. Katika Jeshi la Polisi, tuna Kitengo cha Intelijensia, ni nini kiini cha mauaji haya na ni nini *solution* ya mauaji haya?

Mheshimiwa Spika, tunavyo vyombo, vifanye kazi, ili Watanzania waishi kwa amani.

ndiyo maana nafika mahali pa kuhoji utendaji wa Jeshi la Polisi ukoje, kwa nini. Mheshimiwa Waziri na jeshi lako viongozi wote, mara nyingine zimetokea lawama, tukio linaripotiwa au taarifa inaripotiwa mapema, lakini hakuna ufuatiliaji wa haraka mpaka matukio yanatendeka, ndipo polisi wetu wanakwenda. Sasa hili hatupi imani wananchi na jeshi letu.

Wengine wanaogopa kuchukua hatua hasa maaskari wa ngazi ya chini, wanaweza kuona uhalifu wakakamata wakababaisha na yule mhalifu, mwisho mhalifu atasema hebu ongea, maana atapiga simu ongea, atampa ataongee, kumbe ni bosi wake na bosi ataagiza acha. *(Makofi)*

Sasa hili halitupi matumaini kwa jeshi letu, niombe majeshi yetu, tunawaamini tendeni haki kwa weledi ili nchi hii wananchi wafurahie, kuwepo katika nchi hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN NASSIB OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza tumshukuru Mungu sana kwa neema zake nyingi kwetu na pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii. Lakini vilevile napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, *IGP* makamanda wote pamoja na askari kwa kazi yao nzuri sana wanayoifanya, wao ndiyo walileta utulivu na amani katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumpongeza *IGP* kwa kuwa mbunifu, yeye ndiye aliyeanzisha ulinzi shirikishi na ulinzi huu umesaidia sana katika kupunguza uhalifu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nitaingia katika Jimbo langu la Mfenesini, Jimbo la Mfenesi lina kituo ambacho kinaitwa vile vile Mfenesini na kituo hiki kimejengwa miaka 70 iliyopita. Hali ya kituo ni mbaya kidogo, kilishaanza kuchimbika, kimeanza kupasuka na vile vile hakina nafasi ya kutosha, eneo limeongezeka na watu wameongezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hamna chumba cha askari kukaa, hapana ofisi ya kukaa Kamanda na nafasi ya mahabusu ni ndogo mno kiasi kwamba wanaweza wakakaa mahabusu wawili mpaka watatu. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri akalishughulikia suala hili na angalau akajenga banda litakaloweza kusaidia kupata vyoo, vyumba vya kupumzikia askari na sehemu ya mahabusu.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile kituo hiki hakina usafiri wowote, mara nyingi wanatumia baiskeli wanapoitwa kushughulikia masuala ya uhalifu. Kwa hiyo, ningemwomba Mheshimiwa Waziri katika hizo pikipiki ambazo zinakuja basi angalau pikipiki moja ipelekwe katika kituo hiki.

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo, naingia kituo cha Bububu, ambacho vile vile ni kituo ambacho sasa hivi kinashughulikia mpaka maeneo ya mjini na takriban kinashughulikia au kinahudumia Majimbo manne; Jimbo la Mfenesi, Jimbo la Dole, Bububu, na majimbo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takriban kiasi watu 20,000 mpaka 30,000 kituo hiki kinahudumia na kituo hakina gari. Kwa hiyo, wanapohitaji gari inabidi wapige simu Ofisi ya Wilaya, waazimwe gari na mara nyingi gari halipatikani na inabidi waende katika tukio kwa miguu au ikodiwe gari au kwa baiskeli. Namwomba Mheshimiwa Waziri kituo hiki kipewe kipaumbele na wapelekewe gari na pikipiki moja miongoni mwa hizo gari ambazo zitafika.

Mheshimiwa Spika, hapa mkononi ninayo orodha ya watu 46 ambao walikuwa askari waliotumikia Jeshi la Polisi. Wengine wameacha kazi toka 2000 na kuendelea na wote hawa wameshafariki, nambari zao za kazi ziko hapa, tarehe ya kuacha kazi pamoja na tarehe ya kufariki. Inasikitisha kwamba watu wote hawa hawajapata haki zao.

Mheshimiwa Spika, nimebahatika kuwatembelea baadhi ya wajane wa hawa askari na hali kwa kweli ilikuwa mbaya sana. Wengi hawamiliki hata mlo kwa siku, watoto hawawezi kwenda shule au kwenda hospitali. Nitamkabidhi Mheshimiwa Waziri na wewe binafsi ili tuhakikishe hawa watu wanapata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamelitumikia jeshi hili kwa uadilifu kabisa na sasa hivi wamekufa hatujali. Baadhi ya mafaili ya watu hawa yamepotea na nashangaa kwamba Maofisa wa Polisi wanasema hawawezi kushughulikia mafao yao kwa sababu mafaili hayapo, waliopoteza mafaili hayo ni wao na wao ndiyo wa kuangalia mbinu za kuhakikisha kwamba hawa wajane na watoto wanalipwa stahiki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitamwomba Waziri suala hili alishughulikie ili watu hawa wapate haki zao, pamoja na wenzangu wa Zanzibar, basi tutakwenda kwa Kamishna ili aweze kutusaidia watu hawa wapate haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni Kambi ya Ziwani, mara moja niliuliza swali hapa kuhusiana na vyoo vya Kambi ya Ziwani na wewe ukasema kwamba suala hili lisije tena, lakini nasikitika kukueleza kwamba hali ya hapo ni mbaya sana na Mbunge mwenzangu hapa wa Jang'ombe kaniambia nilieleze suala hili. Mbunge wa Jang'ombe pamoja na Mwakilishi wa Jang'ombe wamewahi kujenga vyoo vya ziwani. Hiki ni Chuo cha Polisi na haya ni Makao Makuu ya Polisi, inasikitisha sana hayashughulikiwi yametupwa kiasi kwamba

Mwakilishi na Mbunge waende wakafanye kazi za ndani mle kutengeneza vyoo.

Mheshimiwa Spika, nafikiri *IGP* na makamanda wananisikia, kwa hivyo hatua zichulikiwe. Askari pale inabidi watoke nje ya kambi ili waende haja, jinsi vyoo vile vilivyo haviendeki. Mwenzangu mmoja kasema waya umetoboka, kwa hiyo watu wanaingia ndani na hali ni mbaya mno.

Mheshimiwa Spika, lingine nazungumzia Koplo Machano Mohamed Haji, huyu amekuwa akifanya kazi Wilaya ya Kasulu na alipigwa risasi na majambazi mwaka jana. Nasikitika kusema kwamba vitu vyake vilivyokuwa Kasulu mpaka leo havikukamilika, mafao yake hajayapata. Kwa hiyo, Kamanda wa kule ananisikia hivi sasa, alikuwa na wake wawili na vitu vyake mpaka sasa hivi havijafika Zanzibar. Tafadhili, vitu hivyo vikamilishwe vipelekwe Zanzibar na mafao yake wapewe wajane. Alijitolea nafsi yake kupambana na majambazi na sasa hivi keshafariki hatushughuliki kabisa kuisaidia familia yake.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa ni kuhusiana na magereza. Wenzangu wanaokaa maeneo ya magereza wameniambia kwamba miti mingi sana inakatwa ili kuwapikia wafungwa. Lakini sasa hivi kuna teknolojia ya *biolatrin* yaani *biogas* ambao wafungwa hawa wangeweza kuitumia. Nafikiri baadhi ya Wabunge wamemwandikia Waziri ili alifikirie suala hili baada ya kutumia miti mingi kwa kupikia, basi choo kile ambacho kinapatikana kutoka kwa wafungwa

kitumike kuzalisha gesi ambayo itaweza kutumia kupikia chakula.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hotuba hii endapo nitapata majibu ya kutosha, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SADIFA JUMA KHAMISI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii kwa mara nyingine kuweza kutoa mchango wangu. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri, watendaji wao katika Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi, katika kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Taifa letu. Ni ukweli usiopingika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inafanya kazi kubwa katika kusimamia na kuimarisha usalama na amani ndani ya nchi yetu. Lakini kama walivyosema wenzangu pamoja na kwamba uchapa kazi wao huo mzuri huwa kuna weakness ndogo za kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie dhana moja, sisi wanasheria tunaita *administrative law*. Naomba sana ndani ya Jeshi la Polisi hii dhana ya *Administrative Law* waweze kuitumia. Tunapozungumzia *administrative law* ina maana kwamba, kwanza tufuate sheria ya uongozi, kiongozi katika hii dhana, kuna *rule doctrine* moja tunasema *doctrine against bias*, kiongozi yeyote hutakiwi kuwa na *bias*. Nimeona ndani ya Jeshi la Polisi kunakuwa na *bias* ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, nitolee mfano kule Zanzibar, Jeshi la Polisi wanaliendesha kwa *bias* ya hali ya juu. Upandaji wa vyeo vyao kwa mfano, wanakwenda kienyeji na undugu tu. Kitu hiki sikipendi mimi binafsi kama kijana. Unakuta kuna vijana wazuri ambao wana taaluma, wana *knowledge* ambayo amemzidi yule kiongozi anayemwongoza, lakini hawezi kumtendea haki kwa sababu ameingia juzi tu katika nafasi.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano, mimi nimesoma na watu *degree* ya kwanza toka 2009/2010 mpaka hii leo unamkuta yupo tu pale *private* eeh! Jamani unam-*discourage* na ana *capacity* ya hali ya juu. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu yeyee ni mtu mmoja makini hebu aliangalie hili, nao tuwa-*encourage* kama ambavyo tunavyosema kwamba tuna-*pressurize* waweze kufanya kazi kwa moyo mmoja.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa upande mwingine unakuta *biasness* inakuwepo kwa mfano, katika Jeshi la Uhamiaji, pia ipo, Jeshi la Polisi, ndani ya Wizarani hata zinapoletwa zile ajira, utaona mie napiga debe sana kuhusiana na ajira, kwa sababu katika watu wanaofuatilia mwenendo mzima wa ajira ndani ya Tanzania hii, nadhani nachukua nambari *one, yes* kwa upande wa Zanzibar, nakwenda kweli kweli kila idara.

Mheshimiwa Spika, nasikitika tu siku moja nilikwenda yule Mkuu wa Uhamiaji kule Zanzibar akajifanya ana haraka, ana kikao. Sasa nasema, naomba mtutendee haki ndani ya jeshi hili, zile ajira zinatoka mtoto wa jamaa yangu, mtoto wa fulani, sijui

mtoto wa fulani, mimi sipendi. Kama mtu ana *capacity* mpe, *we need manpower,* hatuhitaji mtoto wa shangazi au mtoto wa mjomba, kama hana taaluma weka pembeni.

Mheshimiwa Spika, suala lingine pia nizungumzie suala hili hili la ajira ndani ya Jeshi la Polisi. Sisi watu wafupi ndani ya Jeshi la Polisi hamtutendei haki, vigezo ambavyo mnavyoviweka katika kuwaajiri wale askari kwa kweli sisi wafupi hamtutendei haki, nazungumza hivyo na ukiangalia ukweli hata ile *fitness,* watu wafupi tuko *smart* kuliko hata watu warefu, lakini nawaomba radhi sana. Tuchukulie mfano tukicheza mpira hapa mimi si mfupi kuliko nyote humu ndani na mbona nawapita kimbio na na-*score* magoli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nitoe mfano kwa hiki ambacho nakiona mimi mwenyewe, naomba vile vigezo mjitahidi angalau na sisi wafupi tupate nafasi, mbona Jeshi la Ulinzi la Wanannchi wa Tanzania nimefanya *course* mwaka 2002, kuna mtu mmoja alikuwa mrefu tena *form six*, kadata, kakimbia kozi, sisi wafupi tukaendelea. Sasa naomba na ninyi mko mtupe nafasi, hii ni haki yetu ya kikatiba siyo kwamba labda nazungumza kama Sadifa, ni haki ya msingi ya kisheria katika *bill of rights,* ukiangalia katika Katiba hiyo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia kifungu namba 12 mpaka 26 utakuta hiyo. Ajira ni haki yangu ya msingi, ukiniwekea kigezo hiki wewe mfupi toka, napaswa nikakushtaki Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, nataka niende sehemu nyingine kuhusu suala la ulinzi shiriki. Nawapongeza sana kwa kweli wamefanya kazi nzuri, lakini *weakness* iliyokuwepo, wale wanaopewa nafasi kuwa wao ndiyo askari wana jamii, huwa wanatumia vibaya. Nimeshuhudia mfano tukio moja pale, mimi naishi Bububu, watu wamepigana mapanga pale kwa sababu yeye anajiona ni askari mlinzi shirikishi, basi anafanya anavyotaka. Naomba sana mjitahidi muwaelimishe na ukweli inatusaidia kwa sababu hata ule wizi nao umepungua lakini kwa upande mwingine japo sabuni. Kwa hiyo, naomba nisisitize hilo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine vitendea kazi, vitendea kazi ni kitu kimoja muhimu na cha msingi ili kuwawezesha hawa askari katika kufanya kazi zao, nazungumza hivyo juzi tu nimeshuhudia na siyo juzi, kabla sijawa Mbunge. Siku moja nilikuta gari ambayo kile kinainai kinachowaka kinam-*escort* Mheshimiwa Waziri Kiongozi, alikuwa Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, *Wallahi* kinasukumwa. Kinasukumwa, kinamsubiri pale Baraza la Wawakilishi, aibu. Juzi nimekikuta tena, nilikuwa nasoma niko, nimekikuta pale darajani, aibu, fedheha, kashifa, uchafu, kinasukumwa na kimeweka mlolongo mrefu pale, kwa hiyo nasema tuangalie sana katika hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala moja lingine ambalo ni muhimu. Waheshimiwa Wabunge tulisikilize, hili suala la maandamano, tutawalaumu ndugu zetu wa Jeshi la Polisi na hapa tutakuwa tunasema kwamba wasitumie silaha, sawa *even though* katika sheria, katiba yetu inaturuhusu

kwamba kuandamana ni haki yetu ya msingi, ni kweli mimi sikatai *is your constitutional right,* lakini fuata utaratibu usivunje sheria. Lakini *without any procedure* unaamua tu kuandamana, kwa mfano, kule Zanzibar kuna ndugu zetu wa Uamsho, *without following any procedure,* mtu anaandama, *at the same time* anasema hii ni haki ya msingi, askari anakuja anakukamata, unalalamika, unalalamikia nini?

Mheshimiwa Spika, naomba sana tufuate sheria, tufuate taratibu za nchi, ukifuata sheria hakuna atakayekuja kukupiga, mimi nasema simuungi mkono mtu ambaye anasema Askari Polisi asipewe silaha. Mimi nimetokea katika Jeshi, katika Jeshi kuna dhana moja tunaita *crowd dispersal* kwa maana ya kwamba kusambaratisha makundi. *Principle* hii unapokwenda kusambaratisha kundi unatakiwa askari utumie silaha ya moto, kwa maana ya kwamba uwe nayo silaha ya moto *even though* hutakiwi kuitumia. Askari Polisi wao wanaambiwa utumie *reasonable force* maana utasema mwenzako katumia *force* lakini je, sisi wanasheria tunaangalia hii force aliyotumia ilikuwa ni *excessive force* au *reasonable* sasa *most of them* askari hawa wanatumia *reasonable force,* sasa utamlaumuje mtu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema wakati naingia jeshini hata kama baba yangu mzazi akiwa anaandamana bila kufuata *procedure* ndiyo kwanza nitaku-*shoot*. Nasema kama mtu anaandamana awe *unreasonable,* bila kufuata ile *procedure,* ashughulikiwe kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Askari itakapostahiki kutumia *force*, atumie *reasonable force* na Mheshimiwa Waziri mie nisije nikasikia kwamba eti askari anakwenda, maana *nature* ya Watanzania siye tunapokwenda kuandamana hatuwi na *good faith*, unaharibu vitu vya watu, unampiga mtu, halafu baadaye umwambie askari yule asiwe na silaha? Tumeshashuhudia askari wangapi wanakufa. Siungi mkono katika hili na nitakuwa wa kwanza kukushtaka kwa nini yule askari asitumie silaha Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hilo, kwa sababu Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la sensa ndani ya kitabu chake…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. bahati mbaya sensa…

**MHE. SADIFA JUMA KHAMISI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Khalfan!

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Mheshimiwa Khalifa siyo Khalfan, *unless* napewa jina jipya leo. Namshukuru Mwenyezi Mungu kunipa nafasi ya uzima nikasimama hapa na na nakukushuru wewe kwa kunipa fursa na mie niungane na wenzangu katika kusema machache juu ya Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, kimsingi mie napenda niseme nimesikiliza kwa makini watu wanalaumu sana Jeshi la Polisi, lakini mie nataka niamini kuwa Jeshi la Polisi chini ya Kamati mpya huyu *IGP* Saidi Mwema lina maboresho na mabadiliko makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubali wako polisi wenye maovu na hiyo ndiyo kawaida ya binadamu hawawezi kuwa sawa wote. Natumia fursa hiyo basi, kumwomba *IGP* na kumwomba Waziri hawa hawa wachache ambao wanaharibu sifa nzuri ya Jeshi la Polisi waangalie na wawachukulie hatua zinazofaa vinginevyo itakuwa wanasemwa kwa ujumla wao, kumbe waovu ni wachache tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na suala zima la mishahara na posho. Posho iliyotajwa kwa mfano ya shilingi 150,000/= si jambo geni kwani limetajwa tokea bajeti iliyopita. Sasa unataja kile kile halafu ndiyo unakitoa, unachukua mwaka mzima unataja kitu mwaka wa pili ndiyo unasema unatoa kitu kipya, hapana! Mimi nafikiri tungekuwa wakweli katika hili.

Mheshimiwa Spika, pili, nizungumzie suala la *pension*. Tunaposema pensheni tunasema mambo mawili. Nimesikiliza kwa makini asubuhi Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Saada Mkuya alipokuwa anajibu, alikuwa anajibu kitaalam zaidi, lakini ukweli wa mambo ni kuwa nyongeza zinatajwa lakini haziwafikii walengwa, hiyo ndiyo issue! Unataja pensheni unaongeza lakini mtu hatii pesa mfukoni.

Mheshimiwa Spika, sasa haya maneno mazuri ya kitaalam na kadhalika, mwisho wa siku watu wanalala njaa hawakuelewi. Kama wanaongeza basi waongeze wawape na wengi tunaposimama Bungeni kwa mfano, kutoka Zanzibar tukazungumzia wastaafu mara nyingi wanakuwa ni wa vikosi tu ama Polisi ama Jeshi ama vingine kwa sababu hivi ndiyo vikosi vya Mungano na ndiyo vyenye waajiriwa wengi wa kutoka upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, sasa hili nasema waliangalie kwa umakini kwa sababu Waziri wa Fedha katika bajeti iliyopita mwaka jana aliahidi nyongeza ambayo hakuitoa, hii ni aibu! Hata yeye alipokuwa akijibu asubuhi ali- *quote data* za mwaka 2009, lakini tupo mwaka 2012. Sasa wanawaambia watu wanawapa fedha halafu hawawapi, wakilalamika mnasema hawa watu wanalalamika, kwa sababu mwisho wa siku mtu ana njaa asilalamike vipi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu wahamiaji haramu. Tunasema kuwa mkazo juu ya mkazo wa wahamiaji haramu kwa sababu inanidhihirikia lazima watendaji wa Serikali wa sehemu za mipakani wanashiriki, *otherwise* watatokaje watu wafike Kongwa, watafikaje Kongwa bila ya kuwa wamepita barabarani? Lakini inaonekana kuna *trip* zinafanywa, watu wanafumba macho, matokeo yake mtakuja kuitia nchi hii kwenye matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, sisemi kila mhamiaji kuwa ni mharamia, wengine ni watu wana njaa tu wanatafuta namna ya kwenda kutafuta kijiwe mbele kwa mbele. Lakini wapo wengine ni wabaya na wanaweza wakatumia mwanya huu wakaifikisha nchi hii mahali pabaya sana. Sasa watu hawa ambao ni watendaji, ni vizuri mkawa-*screen* inakuwaje? Hivi kweli mtu anatoka Ethiopia afike mpaka Mbeya bure bure tu? Lakini mbaya zaidi inafikia mahali tunaonekana watu wa ajabu sana, watu 30 au 40 au 60 wanakutwa wamekufa, hivi kama ni Watanzania tungesikia wamekufa kwa wingi namna hiyo nchi za nje sisi tungeonaje? Haiwezekani hata siku moja!

Mheshimiwa Spika, tunaruhusu vitu vya ajabu ajabu namna hii, matokeo yake inaingia doa nchi nzima na inaingia doa Serikali nzima, kwa sababu gani? Ni watu wana dhiki, dhiki zipo kwa wenzetu kubwa tusione sisi hapa tunakaa wenzetu wana dhiki na ndiyo maana yake wanalazimika kuhama. Pengine wanakosea njia, lakini wanapokosea tusitumie unyonge wao tukawatoa pesa kijingajinga, tukawaua na tukawasababishia vitu vya ajabu. Watendaji hawa ni lazima tuwaangalie kwa umakini sana.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukilalamika kuhusu suala zima la msongamano wa wafungwa magerezani, ni aibu sana! Hivi katika hali ya kawaida mtu anakuwa mtuhumiwa miaka tisa Gerezani, miaka kumi anakuwa Gerezani anatuhumiwa tu? Sasa utamfunga miaka mingapi baadaye? Mahabusu miaka kumi? Halafu inaonekana kama kuna mzaha mzaha hapa, wanachukulia mzaha,mzaha, lakini

ninayesema ni miongoni mwa watu ambao kwa bahati mbaya siasa za nchi hii zimeshanipeleka huko Gerezani.

Mheshimiwa Spika, kule kuna hali mbaya msione ni Sheraton, watu wakizungumzia kuwa wanadhalilishwa wanadhalilishwa kweli, Gerezani watu wanavuliwa nguo, Gerezani watu wanafanyiwa vitu vya ajabu ajabu, lakini watu hapa kwa sababu havijawafika wao watu wanachekacheka, wanaona mzahamzaha tu. Lazima magerezani paangaliwe kwa sababu mambo yanayofanyika ni kinyume na ubinadamu kabisa.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani hata siku moja leo mwanamke unamvua nguo Gerezani, *why*? Halafu tunakuja tunasema Bungeni, Serikali haiji na majibu, hebu zikitoka *challenge* hizi nendeni mkafanye utafiti, mkija hapa mje muwaeleze wananchi kupitia Bunge hili kuwa kweli lilifanyika na tumelishughulikia hivi na hili halikufanyika, ni maneno ya watu ili wananchi waamini, lakini mnachukulia kirahisi rahisi tu mambo yanakwenda, yaani *business as usual* kama alivyosema Mchungaji Msigwa siku moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo hasa katika Gereza la Segerea. Kuna *mix up* ya wafungwa yaani watoto, watu wazima, majambazi na watuhumiwa wanachanganywa pamoja, hii ni hatari! Hivi kweli tu-*imagine* hapa angekuwa Mbunge yeyote ana mtoto wake wa miaka kumi au kumi na moja au tisa kafanya kosa akachanganywa kwenye kikosi cha watu wabaya namna ile angeonaje?

Mheshimiwa Spika, matokeo yake watoto wanafanyiwa vitu vya ajabu sana, tusingetumia Bunge hili kwa ajili ya kutumia maneno ya kudhalilisha, lakini wanafanyiwa vitu ambavyo ni kinyume na utaratibu wala havikubaliki. Kosa ni kwa sababu ya kuwachanganya, lakini ungewabagua na kuwaweka peke yao haya yasingetokea. Lazima tuwe na huruma kama wazazi, kama wazazi litukere hili, lituumize na mtu aone kuwa naona jambo hili linasemwa nilifuatilie ili kuliondoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala zima la ajira na hapa nataka niseme kwa uchungu sana. Toka mwaka 1995 tumeanza mfumo wa Vyama Vingi. Nakubali hamasa na tuhuma juu yetu toka mwaka 1995 pale mwanzo mwanzo zilikuwa ni nyingi, lakini sasa inaonekana imekuwa kama *syndrome,* yaani ni tatizo na ni ugonjwa na Mandwele umo ndani ya mwili, hatujirekebishi. Suala la ajira bado lina utata na labda zaidi nisemee kwa upande wa kwetu Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, tunafikiri kuwa ajira zinazokuja zinakuja kama *camouflage* ionekane vijana wanaajiriwa, lakini ukifanya mahesabu nafasi zilizoletwa na wangapi wamepata, kuna tatizo! Zinarudi kwa wakubwa wenyewe, yaani mtoto wangu, mtoto wa mjomba wangu na kadhalika, *no*! ni vizuri tukawa *transparent* katika hili kwani tunahitaji vijana 50, vijana 50 basi tangaza, unaogopa nini kutangaza watu wakaja kwenye *interview* hata 1000, wewe si unataka watu 50, basi *choose 50 out of 1000, choose the best* uchukue. Lakini unapeleka kwenye watu wanafanya

vitu vya ajabu ajabu, tena inakuwa mbaya sana katika uajiri wa Jeshi uliopita, nasikitika sikuwepo hapa.

Mheshimiwa Spika, katika uajiri wa Jeshi uliopita kuna watu Wete wametolewa pesa shilingi milioni moja au milioni moja na nusu wazee wanyonge eti vijana wao wapate ajira na ajira hiyo hawakuipata na sasa wananung'unika, ni aibu! Hatuwezi kwenda hivyo! Hili Jeshi linahitaji lipate vijana waadilifu na waaminifu watafuteni kwa njia ya wazi, kwa nini unakuwa na ujanja ujanja huu, unaleta nafasi 10 halafu tano unachukua mwenyewe, *why*? Mlishasema kuwa vijana hao watoke katika ama JKT au JKU, *why they are coming out of that?* Kwa nini wanatoka katika nafasi nyingine zaidi wanatoka majumbani kwa kisingizio eti wamesoma *form six* na wala si kweli, hakuna *form six* wala *form three*, ni ujanja ujanja tu. Hatuwezi kwenda hivyo, tunasema mambo haya kwa uchungu kwa sababu sisi tunakaa na watu na tunakaa na vijana na haitupendezi.

Mheshimiwa Spika, sisemi umchukue huyu mtoto wa *CUF* kwa sababu humtaki lakini huyo wa CCM umchukue kwa uhalali, usimtoze pesa zake halafu usimchukue. Hii ni dhuluma ya ajabu sana, mnyonge wa Pemba maskini ya Mungu unamwambia atoe shilingi milioni moja na nusu ili mwanawe apate ajira mwisho wa siku hukumchukua na pesa yake imekwenda na maji anakaa ananung'unika halafu anasema huyu fitina tu, fitina gani kama ni wewe ungenyang'anywa fedha hiyo katika unyonge ungekubali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgao wa mafuta. Mkoa wa Kaskazini wamepewa shilingi milioni 175 mkoa mzima, sawa! Lakini hetu tuangalie shilingi 400,000/= unazozipanga kwa siku nzima kwa mkoa mzima katika hali ya kawaida, sawa, lakini tazama pana magari mangapi na yanafanya safari gani, hapo halijatokea tatizo la dharura, kweli hiyo pesa inatosha?

Mheshimiwa Waziri, nafikiri jaribuni sana kuangalia kwa sababu unapopunguza Petroli na Diseli kwa Askari maana yake unapunguza *efficiency* yao kwani pakitokea tatizo hawatakwenda na ikiwa hawatakwenda yatakuwa ndiyo hayo sasa, kama kuna tatizo inabidi dereva wa Polisi akatoe pesa zake akatie mafuta, hana pesa za kwenda kula na watoto wake atapata pesa za kutia mafuta?

Mheshimiwa Spika, mambo mengi ni mazuri katika nchi yetu, lakini kuna matatizo madogo madogo ambayo ni ya aibu. Ni vizuri yakarekebishwa ili haya malalamiko ya Wabunge kwa niaba ya wananchi Bungeni yakapungua. Tukiwa *transparent* katika mambo yetu na tukiwa *fair* katika mambo yetu, basi malalamiko yatakuwa madogo sana.

Mheshimiwa Spika, narudia kuhusu pensheni, pensheni mnazowaahidi watu kuwapa, basi wapeni, posho zao. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kidogo katika Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kupitia Jeshi la Polisi. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge mnakumbuka katika Bunge la Bajeti la mwaka 2011 nilizungumzia suala la mtoto Hamza ambaye alikuwa amepata majeraha makubwa sana tumboni ya kupigwa risasi na Polisi wakiwa doria usiku katika Kata ya Keko.

Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali ilinisikia, nikakutana na Mheshimiwa Balozi Kagasheki kipindi kile akiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, pia nikawa nimekutana na Mheshimiwa *IGP* Said Mwema, nikakutana na Mheshimiwa Kamishna Chagonja, pia nikakutana na Kamishna Tweve, wote kwa pamoja tukakaa meza moja, tukaangalia ni kwa namna gani mtoto huyu tunaweza tukamsaidia ili kuokoa maisha yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwa sababu Wabunge wengi wamekuwa wakiniulizia imefikia wapi, lakini ni kwamba mtoto huyo baada ya kikao kile siku hiyo hiyo alianza kupata matibabu ya uhakika. Hapa ninapozungumza mtoto huyo ni mzima, anaendelea vizuri, anasoma shule na yuko na afya njema. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimshukuru *RPC* wa Mkoa wa Temeke yaani Mkoa wa Kipolisi, Temeke Kamanda Misime kwa ushirikiano mkubwa sana aliouonesha wakati wa kipindi hicho kwani alitoa pesa yake mfukoni kugharamia baadhi ya vyakula sambamba na kununua sare za mtoto huyo. Ikumbukwe kwamba mtoto huyo alikuwa akiishi hapa

Dodoma akisoma Shule ya Msingi Makole na alikuwa amekwenda Dar es Salaam kutembea ndipo ilipomkuta zahama hiyo. Kwa hiyo, Jeshi la Polisi liliingia gharama ya kumtafutia sare, shule na chakula, kwa kweli nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Balozi Kagasheki kipekee kabisa, alinikabidhi pesa kwa ajili ya kununulia godoro la huyu mtoto ili aweze kulala sehemu ambayo ni nzuri kwa sababu pia maisha yake kule ni duni na godoro lilipatikana. Kwa mara nyingine tena na kwa niaba ya wazazi wa mtoto huyo kwa kweli tunapenda kutoa shukrani za dhati kabisa na wananchi wa Keko leo hii nafikiri watakuwa wamefurahi kwa kufikisha salamu hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niende moja kwa moja kwenye mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hili suala tutalizungumza tu na itabidi utuvumilie kwa sababu hatuna namna ni lazima tuendelee kusema hayo hayo kwa sababu sisi Wabunge tumepitia katika maeneo mbalimbali katika nchi hii. Kwa hiyo, kila mtu ni lazima atazungumza ama kuhusu Magereza ama Polisi kufuatana na jinsi alivyojionea mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, binafsi nimepita kuangalia nyumba za Magereza, Dar es Salaam, nimeangalia katika Wilaya ya Kibondo, nimeangalia katika Wilaya ya Muheza na baadaye nikawa nimekwenda Bukoba. Nyumba za Askari Magereza zinatia aibu kote huko

nilikopita. Zinatia aibu ya hali ya juu utafikiri ti hawa watu hawafanyi kazi katika nchi hii ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri katika hilo, Waziri huyo ni kijana na ana nguvu, ahangaike kokote kule atakakoweza na vyovyote vile itakavyokuwa itafutwe pesa ili Askari Magereza wetu wa nchi hii wajengewe nyumba zenye hadhi.

Mheshimiwa Spika, nikianzia na Wilaya ya Kibondo, nimefika kule na kama nilivyosema mwanzoni kwenye mchango wangu wakati nachangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu nili-*declare interest* kwamba kule ndiko nyumbani ninakozaliwa. Nimefika kule Magereza ya Kibondo nyumba wanazokaa Askari jamani utafikiri wanaishi mbuzi! Mheshimiwa Waziri, hali ni mbaya sana, ni mbaya mno! Madirisha yameegeshwa kwa matofali!

Mheshimiwa Spika, kuna hizi nyumbawanasema wanakaa Maofisa, kweli inatia huruma. Tunaomba sana Serikali iangalie kwani nchi hii wanakuja watu wengi kutoka nje, wanakuja kuona tunavyoishi wanatembelea maeneo mbalimbali, ni aibu hivyo tunaomba hili mliangalie ili Kibondo wapate nyumba nzuri Askari Magereza kwa ujumla wanafanya kazi nyingi kama alivyosema mwenzangu aliyenitangulia. Hao hao mfungwa akiwa juani na yeye analimwa na jua, mvua ikinyesha na yeye ananyeshewa, hebu tutambue mchango wa Askari Magereza kwani hali ni mbaya sana katika Magereza Kibondo, mbaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikafika Muheza, sasa kule ndiyo kichekesho maana hata hiyo nyumba ya Mkuu wa Gereza yaani Afisa Magereza imekandikwa kwa udongo, imeezekwa kwa makuti, jamani! Inavuja! Sasa jamani hawa watu tunawadhalilisha. Kwa hiyo, naomba Waziri kama vile alivyohangaika Polisi hawa kidogo wakapata nyumba nzuri za kisasa basi na Magereza iingie kwenye historia na wenyewe wapate nyumba, tunaomba iwe hivyo! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bukoba jengo la Magereza lina miaka mingi karibu linawaangukia, litawavunja migongo Askari na familia zao, tangu enzi za Mkoloni mpaka leo! Nshamba kule nako nyumba za *FFU* zina hali mbaya, karibu zinadondokea watu, hali ni mbaya! Tunaomba Serikali ilisikie hili na Mheshimiwa Waziri narudia tena yeye ni kijana na si mgeni katika Serikali hii, tunaamini anaweza akaleta mabadiko katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pia nyumba za Askari Magereza na *FFU* zinatia aibu, wengine wanaziita ni *full suit,* joto mtindo mmoja. Kama Dar es Salam basi ndiyo unakuta baba na mama wote ni Maaskari asubuhi huyu anaondoka anakwenda na genge hili na yule na genge lile, watakutana jioni, nyumba ni joto kali hakuna hata kuambizana habari ya *school fees* ya motto, hali ni mbaya watakaa wapi? Watazungumzia wapi? Tunaomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumesema kwamba hawa Polisi kwa ujumla, Askari Magereza au tuseme

kada hii ya Askari waboreshewe mafao yao na stahiki zao kwa sababu hili ndilo linalowafanya wakati mwingine wanapokea rushwa pamoja na kwamba wakati mwingine ni tabia ya mtu, lakini huku rushwa imekithiri, hali ni mbaya! Mshahara wa shilingi 200,000/= mtu utaishije kama Dar es Salaam jamani? Ah! Hata mimi ningepokea hiyo hela, sasa nitaishije? Watu hawa wana watoto, wameoa, wana familia zao zinazowategemea, lakini mshahara shilingi 200,000/= wataishije katika hali ya kawaida?

Mheshimiwa Spika, tunaomba tuiangalie Wizara ya Mambo ya Ndani ili wapate hela ya kutosha ili Askari wetu waweze kulipwa vizuri wafanye kazi kwa moyo. Tunajua wapo wenye udhaifu ambao hawawezi kuvumilia hata kama wangelipwa mamilioni, lakini naamini tukiboresha mafao na maslahi ya Askari wetu watafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia kwa kifupi sana kuhusu msongamano wa wafungwa katika Magereza zetu. Naomba hizi huduma za *Parole* basi zipanuliwe ili hawa watu wanaokwapua simu, ameiba kuku, wamepigana kwa sababu ya wivu wa mapenzi au wamefumaniana na kadhalika, hakuna haja ya kuwaweka mahabusu maana wanaongeza tu msongamano wa watu ila wapewe kazi za kijamii na wasimamiwe.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Dar es Salaam ni mji mchafu, wakipatikana watu kama hawa, wakapangwa sehemu fulani, leo wanaingia Manzese wanavamia Manzese kunawekwa ulinzi wa kutosha

sehemu ile itakuwa safi kuliko kuwarundika humo ndani tunaongeza tu gharama ya kuwalisha, hawajifunzi kitu bali wanajifunza mambo mengine ya ajabu, kwa sababu wakirudi huko wengine wamenogewa na mambo fulani kule wanakuja kufanya tena ili warudi.

Mheshimiwa Spika, naomba hilo tuliangalie kwamba watu wenye makosa madogo madogo wasikae sana huko, ikishagundulika kama kosa lake ni dogo basi arudishwe uraiani au watu wa *Parole* waongezewe nguvu ili hawa watu wafanye kazi za kijamii.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine naomba sana kuchanganya hawa watu wazima na watoto Magereza ni hatari. Vitoto vyenyewe vikirudi vinasema na mambo mengine hayasemeki hapa. Kwa hiyo, tunaomba watu hawa wasichanganywe.

**SPIKA:** Afadhali usiseme hayo! (*Kicheko*)

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja kama Waziri ataniambia kwamba nyumba za Magereza zitajengwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nawashukuru sana jamani na muda umekwisha na nashukuru sana kwa nidhamu ya kuongea kwa sababu hivi ndivyo watu wanapenda kusikia mawazo yenu, siyo kusikia fujo zenu, zile haziwasaidii.

Kwa hiyo, asubuhi nilikuwa nimemtangaza Bwana Bashir Abdallah kutoka Tarime nikasema sijui amekuja kufanya nini. Kumbe ni Mweka Hazina wa Wilaya wa CHADEMA, Wilaya ya Tarime. Kwa hiyo, nashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu mmesema sana na mpaka hivi sasa wamechangia watu 36 na mmezungumzia vitu vidogo vidogo kama nyumba na kadhalika.

**SPIKA:** Kwa hiyo, tukirudi jioni nitampa dakika 25 Naibu Waziri na Waziri tutampa dakika 50 na mchana huu wakafanye majumuisho angalau waone wanaweza kuwajibu namna gani.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Naombeni jamani Kanuni, kuna hatua za kufuata, mkianza kusimama, sasa hatuelewi tutafanya nini. Naomba Mheshimiwa ukae kwanza, tafadhali! Nikishamaliza mimi ndiyo nakaa, halafu mtu mwingine anasimama na mimi namwona. Haya Mheshimiwa Hamad!

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kutumia Kanuni ya 47 kutokana na ajali ya Meli iliyotokea Zanzibar hivi sasa ambapo watu 200 inasadikiwa wamekufa na miongoni mwao kuna watoto wasiopungua thelathini (30).

Mheshimiwa Spika, naomba kwa idhini yako na busara zako turuhusu Bunge lako lipitishe tu matumizi ya Waziri, hii *session* ya ku-*wind up* hii tumsamehe. Tunaomba Wabunge wenzetu watuunge mkono ili tupate nafasi sisi wengine tutoke tukaangalie ni kwa namna gani tunaweza tukashiriki katika msiba huo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba utumie busara zako na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Naomba mkae sasa. Naomba mkae!

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni hii aliyosema ambayo ni ya dharura, unapoitumia hii Kanuni ni kwamba, unasema tuahirishe shughuli tujadili jambo la dharura. Bahati mbaya tumeitumia hii Kanuni vibaya wakati wote. Madhumuni ya Kanuni hii yalikuwa, kwa mfano, sisi tunaendelea na shughuli zetu hapa, mwenzetu mmoja anakuja anatwambia pale Chamwino kuna ajali imetokea, watu wengine wamekufa, wengine wanahitaji damu na wengine

wanataka usafiri. Tunaamua sasa jamani, tuahirishe shughuli twende huko tukawasaidie, wenye kutoa damu waende na wenye kutoa magari yao waende. Ama kuna moto mahali hapa hapa tunaamua ili tuondoke.

Sasa suala hili lililotokea, kweli ni kubwa sana na linatisha, hata Serikali yenyewe ukubwa wake haiujui. Sasa nafikiri kwamba, tumalize kazi hii wakati huo Serikali inafanya jitihada za kutafuta habari sahihi zilizoko kule. Halafu tutafanya maamuzi kama wenzetu humu inabidi wasafiri kesho au usiku huu, tutaona. Vinginevyo inaitwa nini, tunafanya kitu ambacho hatuna uwezo nacho.

Hivi sasa tumetoka kuongea na Waziri anayehusika na mambo ya dharura, kwamba wekeni mtu wenu atwambie nini kinaendelea kule, nini kimetokea, ili kusudi tuweze kufanya maamuzi. Pengine nyie Waheshimiwa Wabunge wa kutoka Zanzibar mtatakiwa kwenda, hilo litafanyika na ofisi yangu itabidi iwasaidie kwenda. Lakini kwa hili tunalofanya sasa, tunafanya nini? Mkienda mnakwenda kukaa tu au mnafanyaje? Mnapiga simu tu au inakuwaje? Ukweli wenyewe ndiyo huo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi tumemaliza kuzungumza na kwamba, Serikali inawasiliana na kule ili kujua kilichotokea ni nini kusudi niweze kufanya maamuzi hapa na kama mtakwenda itabidi niwasaidie kwenda. Hilo ndilo ninalosema.

Sasa Waheshimiwa Wabunge naomba tuendelee. Mheshimiwa Naibu Waziri, dakika 25!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara yetu ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, nikupongeze wewe binafsi kwa kuongoza mjadala huu kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Bunge na Wabunge wote kwa michango yao katika masuala mbalimbali yanayohusu Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Huu ni uthibitisho wa imani yake kwangu na namuahidi kwamba sitomwangusha.

Mheshimiwa Spika, aidha, niishukuru familia yangu kwa kunipa moyo katika majukumu yangu ya kuwatumikia wananchi. Nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Chumbuni kwa kuniamini na kunichagua kuwa mwakilishi wao katika Bunge hili Tukufu. Ni matumaini yangu kwamba, wataendelea kunipa ushirikiano ili kwa pamoja tuweze kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya Jimbo letu na Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuunga mkono hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja, naomba sasa nichukue fursa hii kujibu baadhi ya hoja zilizoletwa mbele ya Bunge hili ikiwa ni sehemu ya michango ya Wabunge wakati wa mijadala ya hotuba hii. Hata hivyo, hoja nitakazotolea ufafanuzi ni zile zinazohusu Jeshi la Magereza au Fungu 29; Jeshi la Zima Moto na Uokoaji, Fungu 14 na Makao Makuu ya Wizara ya Mambo ya Ndani, Fungu 51.

Mheshimiwa Spika, labda kwanza niseme kwamba kama mwakilishi wa Wizara, naomba nishukuru michango yote na kuwathibitishia wachangiaji kwamba, michango yao tumeisikia ile ambayo imetupongeza tumepokea pongezi hizo, ile ambayo imetupa pole tumezipokea na wale waliotoa ushauri ni kwamba, ushauri huo tutaufanyia kazi baada ya kupitisha bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naelekea kwenye hoja ambazo nataka nizifafanue. Hoja ya kwanza ilikuwa ni hoja kuhusu tatizo la msongamano magerezani.

Mheshimiwa Spika, hoja hii imechangiwa na Wabunge wengi tena kwa uchungu mkubwa. Kwanza, nataka nikubaliane na wachangiaji kwamba, ni kweli hili ni tatizo na kama Wizara tumeshaliona kuwa ni tatizo. Naomba nitoe taarifa kwamba, ni tatizo mtambuka katika kusababishwa na katika kutatuliwa.

Tatizo hili linahusu wadau wengi na kila mmoja wetu ana wajibu na mchango katika hili ili tuweze kulitatua.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa kwamba, magereza yetu ambayo yana uwezo wa kuchukua mahabusu na wafungwa 29,000 hivi sasa kwa wastani wake yanahifadhi mahabusu na wafungwa 39,000. Hii ni hesabu kubwa sana kutokana na uwezo ambao upo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, naomba nitoe taarifa kwamba, jitihada za Serikali katika hili zimeanza na kuna mwelekeo wa kuwa tayari linaweza likapata mwelekeo wa kutatuliwa. Katika hatua ambazo Serikali imezichukua ni pamoja na kuunda kikosi kazi ambacho kiko chini ya *DPP* kama Mwenyekiti. Kikosi hiki kinaundwa na wadau kutoka taasisi zinazohusika na Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, *DPP*, Polisi, *CID*, TAKUKURU na Magereza.

Mheshimiwa Spika, mambo ambayo wanayashughulikia hasa ni kulitazama hili tatizo lilivyo na kujaribu kuishauri Serikali nini cha kufanya. Katika kazi ambazo zinaendelea kufanyika kwa muda huu mfupi ni kwamba, kuna hatua za kuziwezesha Kamati za kusukuma kesi katika maeneo tofauti ya nchi yetu na kuharakisha upelelezi, kuna jitihada za Rais katika utoaji wa misamaha kila pale ambapo nchi yetu inaingia kwenye sherehe tofauti, kuongeza Magereza na kukarabati ambayo yapo. Lakini kubwa zaidi ni kutafuta utaratibu mwingine wa kutoa hukumu, yaani

hukumu mbadala. Pamoja na haya kuna baadhi ya sheria pengine zinaweza zikalazimika kubadilishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara itashirikiana na wadau wote niliowataja pamoja na wengine watakaojitokeza ili kuhakikisha kwamba, tatizo hili linakuwa historia katika magereza yetu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ambayo nayo ilizungumzwa sana ni kuhusu watoto wadogo kuchanganywa na wahalifu wakubwa na wahalifu wazoefu. Hili pia limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na kwa masikitiko makubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa kwamba tatizo hili pia tunalishughulikia baada ya kuliona. Sheria za Kitaifa na hata za Kimataifa haziruhusu hili na kwa hiyo, hatuwezi tukakaa nalo likaendelea. Jitihada za hapa na pale zimechukuliwa katika kufanya *severity* ya hili tatizo isiwe kubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Wizara kwa kushirikiana na *UNICEF* inafanya utafiti kupitia mradi maalum ili utoe taarifa za kitaalam na hatimaye tuweze kupata *system* ya kuwashughulikia watoto ipasavyo. Huu utakuwa ni mwongozo katika Mahakama ya Watoto, Mahabusu ya Watoto na hata shule za Watoto kwa lengo la kutoa maadili kwa watoto watukutu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kulikuwa na hoja kuwa Jeshi la Magereza liongeze uzalishaji hasa katika Kilimo kwa lengo la kujitosheleza kwa chakula. Hili ni

wazo zuri na tayari limeanza kufanyiwa kazi katika *circles* za Magereza na Wizara. Jeshi la Magereza limeainisha mashamba kama 17 kwenye eneo la Kongano la Kusini la Kilimo ambapo jumla ya hekari 17,000 zimeshatengwa na tayari kupitia *TIC* Magereza inatafuta wabia katika kuhakikisha kwamba, upanuzi wa uzalishaji unafanyika. Magereza ambayo yatahusika na maeneo yao ni ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, Mbeya, Rukwa na Kigoma ambayo yako kwenye eneo la Kongano hili.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine ya maslahi duni ya askari, vitendea kazi, ikiwemo mishahara na posho duni na kulimbikizwa kwa posho. Hili nalo lilichangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ambao kwa uchungu mkubwa walihisi kwamba, askari Magereza hawatendewi haki ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili nalo tumelifanyia kazi na naomba nitoe taarifa kwamba, kuanzia tarehe 1 Julai, 2012, posho ya chakula kwa ajili ya Askari Polisi na Magereza imepandishwa kutoka 100,000/= kwa mwezi hadi 150,000/=. Hata hivyo, kwa mujibu wa suala hili lilivyoshughulikiwa na kwamba ndiyo kwanza mchakato wake unamalizika hakutakuwa na malimbikizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja pia ndogo ya kwamba, baadhi ya askari hawapandishwi vyeo na wanabaki wakisota. Vyeo hutegemea tabia, elimu na utendaji wa mtu. Pia kwa mujibu wa sheria, Jeshi la Magereza linaendelea kupandisha vyeo askari wake na maafisa kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya ubovu wa magereza na nyumba za wafanyakazi. Hili kweli ni tatizo na kwamba kuna uchakavu wa miundombinu hasa ya nyumba na magereza ambayo *infact* ina *back date* kwenye ukoloni. Hata hivyo, Serikali kupitia Jeshi la Magereza imekuwa ikiendelea kuzikarabati nyumba pamoja na magereza hayo kila wakati uwezo unapokuwa umepatikana.

Aidha, kuna upungufu mkubwa wa nyumba, hilo nalikubali kwamba nyumba ambazo zipo ni kama 4,092 wakati mahitaji halisi ni nyumba 14,000. Suala hili limeshughulikiwa kwenye mpango mkakati wa maboresho ya Jeshi la Magereza na miundombinu pamoja na huduma zake na utekelezaji wa mpango huu utakuwa ni mwarobaini wa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa kuongeza watendaji wa magereza ili yaweze kumudu gharama na madeni. Ajira katika jeshi la Magereza zinaendelea kutolewa hatua kwa hatua. Aidha, kuhusu suala la madeni ni kweli kwamba, kwa sababu ya ufinyu wa bajeti kuna madeni yanayohusu watumishi, wazabuni na kuna madeni yanayohusu umeme, maji, ambayo Wizara hii pamoja na *CAG* wanayafanyia kazi ya uhakiki na yatakapokamilika yatalipwa kwa mujibu wa taratibu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba iongezwe kasi ya kutumia TEHAMA kwenye jeshi na usimamizi wa wahalifu. Kuna mpango maalum wa mtandao wa usimamizi wa wafungwa unaitwa *OMIS* ambao umekwishaanzishwa katika magereza ya Dar

es Salaam. Ni lengo la bajeti hii kwamba, mwaka huu upanuzi wa mtandao huu ufanyike kuja Dodoma na Tabora.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kujenga Magereza mapya na kuimarisha huduma za maji safi, umeme na majitaka katika magereza yaliyopo. Jitihada za ujenzi zinaendelea kwa kuchimba visima na kusambaza umeme katika magereza tofauti. Aidha, Serikali ina mpango wa kujenga magereza mapya 36 katika Wilaya ambazo hadi sasa hazina magereza. Hili litategemea pia utekelezaji wa mpango mkakati ambao niliusema hapo kabla.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na Wabunge, Mheshimiwa Said Mtanda na Mheshimiwa Amos Gabriel Makala, ambao walisema *specific* kwenye maeneo yao. Kuna gereza linaitwa Kigurugundwa ambalo liko kwenye Jimbo la Mheshimiwa Said Mtanda na alisema kwamba, liangaliwe kuhusu uwezekano wa kupeleka maji na umeme. Kuhusu maji kisima kimechimbwa, lakini kina matatizo na jitihada za kufanya maji yapatikane zinaendelea. Vile vile, kwenye gereza la Wami ambalo liko Mvomero kwa Mheshimiwa Makala.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme ni kwamba, magereza haya hasa Kigurugundwa na Urambo yako mbali sana na eneo ambalo umeme wa gridi ya Taifa umepita. Hata hivyo, jitihada zinafanywa ili kuhakikisha kwamba kwa kutumia *REA* nishati mbadala inafikishwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya ukamilishaji wa magereza ambayo wananchi wameanza kuyajenga katika maeneo tofauti ikiwemo Kibaha, Mbarali na maeneo mengine. Magereza haya yataendelea kukamilishwa katika mpango ambao awali niliusema.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja nyingine inasema magereza ichangie katika kupunguza uhalifu. Hii aliitoa Mheshimiwa Leticia Nyerere. Naomba nimtaarifu tu kwamba Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na *UNDP* tayari limefanya utafiti na kuandaa mitaala kwenye vyuo vyake kwa lengo la kuhakikisha kwamba *correctional sciences* zinapewa nafasi katika kubadilisha wahalifu ili wanaporudi kwenye jamii wawe ni watu tofauti na kabla hawajaondoka.

Mheshimiwa Spika, pia kuna huduma za ushauri nasaha, kijamii, kisaikolojia na kiroho ambazo huwa zinatolewa magerezani ambazo zinawasaidia pia wahalifu kubadilisha tabia na kujiandaa katika maisha ya uraiani.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi kuna utaratibu wa kutoa elimu katika ngazi tofauti, elimu ya kawaida na kazi za ufundi kwa lengo pia la kuwatayarisha wahitimu wa vyuo hivi ambao ni wahalifu kwa wakati huu au wafungwa waweze kuingia kwenye jamii wakiwa wamerekebishika.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja na ushauri wa kutumia nishati mbadala kutoka kwa Mheshimiwa Waride Jabu. Mpango huu tayari unafanya kazi na magereza tayari yanatumia makaa ya mawe kama gereza la Mbeya na pia *biogas* kwa Dar es Salaam kwa ajili ya kupikia chakula cha wafungwa na mahabusu. Lengo ni kuhakikisha kwamba mtandao huu unapanuka ili tuweze kuwa sehemu ya kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu mpango wa kuwapima UKIMWI mahabusu au wafungwa. Naomba nitoe taarifa kwamba hakuna Mpango ambao umeandaliwa kwa ajili ya kuwapima UKIMWI isipokuwa kuna waelimisha rika ambao wametayarishwa na tunao kama 560 na baada ya kuwaelimisha wenzao wafungwa wanaamua wenyewe kwa hiari zao kupima UKIMWI. Baada ya kupima UKIMWI wale ambao watakuwa wameathirika wanapata huduma kama inavyotakiwa kutegemea na *CD4* anaweza kupata *ARV's* na wengine wanabadilishiwa aina ya chakula ambacho wanakula wakiwa magerezani.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kwamba ajira hazitangazwi. Naomba niseme kwamba ajira zote hutangazwa kwenye magazeti, redio na *TV,* kwa mtu ambaye anafuatilia basi ni rahisi kujua kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na pendekezo kutoka kwa Mheshimiwa Sabreena Sungura kwamba, hawa waliohukumiwa kunyongwa wanyongwe kweli,

na huu ni ushauri ambao tumeupokea na tunaendelea kuufanyia kazi kwa mujibu wa Sheria na utatekelezwa ukionekana una *merit*.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la kupekuliwa wafungwa au mahabusu wa kike ambalo limefikia kuitwa ni kudhalilishwa. Magereza yote ni maeneo ambayo kuna sheria ambazo lazima zitawale. Kuna vitu vinaruhusiwa, kuna vitu vingine haviruhusiwi. Upekuzi ni jambo ambalo linafanywa kwa mujibu wa sheria na linaruhusiwa katika magereza yote duniani. *Level* ya namna ya kupekua inategemea ushirikiano anaoutoa mpekuliwa. Mara nyingi unaweza uka-*declare* kwamba mimi nina hiki na hiki na ukatakiwa uviweke ikawa kazi imekwisha. Lakini ikiwa kuna shaka sasa basi inalazimu hatua za ziada katika upekuzi zichukuliwe na hapo ndipo ambapo pengine udhalilishaji unaosemekana unaweza ukafanyika.

Mheshimiwa Spika, naingia kwenye Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Kulikuwa na hoja kwamba Jeshi hili liimarishwe, lipatiwe vitendea kazi na elimu itolewe kwa wananchi kwa sababu kuna hisia kwamba lina uwezo mdogo wa kazi hii. Ni kweli kwamba hivi sasa Jeshi ndiyo kwanza linaanza kama ni utekelezaji wa Sheria Namba 14, lakini tayari vikosi vyote ambavyo vinahusika na kazi ya zimamoto pamoja na uokoaji katika Halmashauri na Viwanja vya Ndege na Jeshi dogo ambalo lilikuwepo vimeunganishwa kuanzia tarehe 1 Julai, mwaka huu na tayari vinafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, wameteuliwa makamanda 60 na tayari wamepata mafunzo kwa ajili ya kuchukua nafasi kwenye Mikoa. Serikali kwa kutaka kuliongezea uwezo Jeshi hili imeruhusu makusanyo yawe *retained* kwa ajili ya kuendeleza Jeshi na kujenga uwezo. Aidha, ajira 2,613 zimeshaombwa kwa ajili ya kuongeza uwezo. Jeshi pia, limefanya makubaliano na *TRA* katika ukusanyaji wa maduhuli ili kuacha Askari wachache waliopo kuhakikisha kwamba wanatumika katika kazi za Jeshi hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uokoaji *in particular,* hili bado uwezo ni mdogo kabisa na wakufunzi wanatarajia kuja mwaka huu ili kujenga uwezo ambao unatakiwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la Jeshi la Zimamoto kuchelewa kufika kwenye matukio. Naomba niseme kwamba, kitu kinachosababisha kuchelewa mara nyingi inakuwa ni taarifa. Kwa sababu wananchi baada ya kutokea matukio ya moto kwanza wanachukua hatua wao wenyewe waone kama wanaweza kuzima na hii ndiyo inaweza ikasababisha kuchelewa kufika. Aidha, uchache wa vitendea kazi, mara chache inakuwa ni tatizo ambalo linasababisha wachelewe kufika na wakifika pengine watu wanakuwa wameshakasirika.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la uwezo wa Jeshi kwamba ni mdogo na kwamba pengine vifaa vyake haviwezi kuzima moto kwenye miji ambayo ina majengo marefu. Hili ni kweli uwezo tulionao kwa sasa ni kufika kwenye ghorofa 18. Hata hivyo, Jeshi

linawashauri watu wanaojenga majengo zaidi ya hapo kuweka *automatic systems* kwa ajili ya kuzima moto.

Mheshimiwa Spika, naomba niende sasa kwenye fungu namba 51, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hapa hoja ya kwanza ilikuwa ni kusimamia matumizi. Wizara imepokea ushauri na italifanyia kazi kupitia Kamati yake iliyokuwepo Wizarani.

Hoja ya pili, ilikuwa wafungwa watoke kwa Mpango wa Huduma za Jamii, mpango huu unafanyika na tayari kuna wafungwa kama 1,400 wameshapata *benefit* ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba wakimbizi wa Mishambo na Katumba walikuwa watawanywe kwenye Mikoa 16 ya Tanzania. Hata hivyo, zoezi hili lilisimamishwa baada ya wadau hasa Wakuu wa Wilaya na baadhi ya Wabunge kuhisi kwamba jambo hili tulitafakari upya. Jambo hili limepelekwa katika Baraza la Mawaziri na tunasubiri mwongozo mpya utakaotoka huko.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo lilizungumzwa ni kwamba kwa nini Jeshi la Zimamoto na Uokoaji halikupangiwa fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linahitaji maendeleo na linahitaji fedha. Hata hivyo, baada ya Serikali kuruhusu kufanya *retention* kwa mwaka huu inahisi kwamba *retention* hiyo itasaidia katika kuipatia vifaa vya kufanyia kazi ambayo wanaifanya na kama itakuwa pengine

haitoshelezi vile tunavyotarajia basi wazo hili tutaliingiza kwenye makisio ya mwakani na *inshallah* fungu litawekwa kwa ajili hii.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba kuna wakimbizi ambao wanatoroka kwenye makambi na kwamba wanapokamatwa wanashtakiwa na hufungwa kwenye magereza ndani ya Kambi za Wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, mkimbizi anadhibitiwa na Sheria ya Ukimbizi ya mwaka 1998 na kwamba sheria hiyo inataja aina ya adhabu na utekelezaji wake moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa mtoa hoja!

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 58(5) cha Kanuni za Kudumu za Bunge kinachoruhusu mtoa hoja kuweza kuomba Bunge liondoe hoja yake mezani. Naomba kwa idhini yako nikisome kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Hebu kisome vizuri kifungu hicho.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Kifungu cha 58(5).

**SPIKA:** Endelea.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** “Endapo hoja imefikishwa Bungeni, mtoa hoja anaweza tu kuiondoa hoja yake kwa kusimama mahali pake na kusema naomba ruhusa kuondoa hoja na papo hapo Spika ataliuliza Bunge kama linaafiki hoja hiyo kuondolewa na inapotokea Wabunge walio wengi watakubali, Spika atasema hoja inaondolewa kwa idhini ya Bunge na hoja hiyo itakuwa imeondolewa na Bunge litaendelea na shughuli inayofuata.”

Mheshimiwa Spika, utakumbuka muda mfupi kabla hatujaingia kwenye ukumbi wa Bunge ulituita mimi na Naibu Waziri ukataka kupata maelezo kuhusu hatua za uokoaji zinazoendelea Zanzibar, nilikupa taarifa ya kazi inayoendelea na nilikujulisha kwamba Kamishna wa Polisi, Zanzibar tayari yupo katika eneo la tukio na anaendelea kutupa taarifa ya kinachoendelea. Ulitupa maelekezo kwamba tutoe taarifa kwa muda mfupi inavyowezekana ili tuweze kuwahi kushughulikia tatizo hilo, lakini pia wewe uweze kushughulikia usafiri wa watu wa Zanzibar watakaokwenda kusaidia.

Baada ya kuona mtiririko wa utoaji mada wa Naibu Waziri nimegundua kwamba muda ulioelekeza tutumie hatuwezi kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakuomba ukubali kwamba tuahirishe kikao hiki ili tuweze kushughulikia jambo hili na kuweza kusaidia wenzetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Naona wote wameafikia. Kwa hiyo, Waheshimiwa naahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. Lakini wakati huo huo naomba Kamati ya Uongozi kwa maana ya Wenyeviti wa Kamati zote wakutane sasa hivi katika Ukumbi wa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.33 jioni, Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 19 Julai, 2012 Saa Tatu Asubuhi kutokana na dharura iliyojitokeza)*